WARUMI

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi Mkuu: Dr. Stephen K. Gibson

Hakimiliki © 2022 Shepherds Global Classroom
Ilitafsiriwa kutoka Toleo la tatu Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB®)." Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

Taarifa kuhusu vibali:

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

Tafsiri ya chapisho la Kiingereza kwenda katika Kiswahili imefanywa na:
Askofu Wilbert Alfayo Ngowi,
Arusha, Tanzania, East Africa.
E-mail: revwangowi@gmail.com
Uhariri umefanywa na John Tuu.

Yaliyomo

Mtazamo wa Kozi 5
Muhtasari wa Kitabu cha Warumi 9
(1) Utangulizi wa Barua 11
(2) Kosa la Wamataifa 23
(3) Kosa la Waisraeli 35
(4) Hali ya Ulimwengu Wote 45
(5) Njia na Maana ya Kuhesabiwa Haki 55
(6) Ushindi dhidi ya Dhambi 67
(7) Mtenda Dhambi Mwenye Hatia 83
(8) Maisha katika Roho 95
(9) Uteuzi wa Mungu 105
(10) Ujumbe wa Haraka 113
(11) Huduma na Mahusiano 125
(12) Maono kwa Ajili ya Umisheni 137
Maswali ya Mapitio ya Masomo na Mtihani wa Mwisho 145
Usomaji Unaopendekezwa 149
Kumbukumbu ya Mazoezi ya Kufanya 151

Mtazamo wa Kozi

Maelezo ya Kozi

Barua ya Paulo kwa Waamini wa Kirumi inaelezea kuhusu umisheni na ujumbe wake. Alielezea kuhusu teolojia ya Injili kwa kusudu la kuelezea ni kwa nini kila mtu anaihitaji. Barua hii imekuwa na mgoso mkubwa kwa muda wote wa historia ya kanisa. Imani nyingi zenye kutatanisha zimekuwa na mizizi yake kutokea hapo. Kozi hii inachunguza Kitabu cha Warumi na kisha kayawezesha yatumike kwenye Maisha ya kuishi Kikristo.

Malengo ya Kozi

1. Kuona utoaji wa Mungu wa wokovu na hitaji lake la imani.
2. Kujadili kuhusu masuala ya kimisheni kuhusiana na watu ambao bado hawajawahi kuisikia injili.
3. Kuelewa ushindi dhidi ya dhambi ambalo ni jambo linalowezekana na la kawaida kwa mtu aliyeamini.
4. Kujifunza kuhusu uhusiano kati ya Israeli na na kanisa kwenye mpango wa Mungu.
5. Kuelewa muktadha wa taarifa ambazo zimekuwa ndio msingi wa ubishani au mashindano ya kiimani katika kanisa.
6. Kupata shauku kwa ajili ya umisheni wa kanisa wa kufanya uinjilisti duniani pote.

Muundo wa Masomo

Masomo yameandaliwa kufundishwa kila moja kwenye kipindi kimoja, lakini muda unaohitajika kutumika kwa kila somo unaweza ukawa masaa mawili au hata zaidi. Kama vipindi vifupi vitahitajika, masomo yanaweza kugawanywa kwenye vifungu vidogo vidogo.

Maelekezo ya kiongozi wa darasa katika somo yako katika mwandiko wa *kulala.*

Darasa linapaswa kila mara kurejelea kwenye "muhtasari wa kitabu cha Warumi" ambao somo la 1 linafuatia baada yake. Darasa linaposoma kila kifungu, wakumbushe wanafunzi jinsi kifungu kinavyoendana na muktadha wa sehemu hiyo ya kitabu, na muktadha wa kitabu kizima.

Maswali ya Mapitio yametolewa kwa ajili ya kila somo. Kwenye kila mwanzo wa kipindi cha darasa, kiongozi wa darasa ni lazima aulize maswali ya mapitio ya somo lililopita na maswali machache kutoka katika masomo mengine yaliyopita. Hakikisha kwamba unasaidia katika kumwezesha kila mwanafunzi kushiriki katika kutoa majibu. Kama mtu ataonekana kuwa hayuko tayari kushiriki katika kujibu maswali, elekeza swali moja kwa moja kwake kwa kumtaja jina. Huu ni muda muafaka wa kusahihisha yale ambayo yalikuwa hayajaeleweka

katika somo lililofundishwa. Maswali ya mapitio ndiyo hayo hayo yatakayotumika kwenye mtihani wa mwisho. Fanya mapitio na masahihisho ya majibu yako kwa kadiri itakavyowezekana. Viongozi wa madarasa wanaweza kuangalia majibu ya maswali haya kutoka kwenye jedwali la majibu katika shepherdsglobal.org.

Alama ya ► ni kiashirio cha maswali ya kujadiliana na mazoezi ya darasani.

Katika maswali ya kujadiliana, kiongozi wa darasa anapaswa kuuliza swali husika na kuruhusu wanafunzi kadhaa kutoa majibu kwa kifupi. Mara nyingine swali litakuwa linarejelea kwenye mambo yaliyokuwa yamefundishwa wakati huo huo. Wakati huo, wanafunzi wanapaswa kuwa na uwezo wa kutoa jibu sahihi. Ikiwa kuna mkanganyiko, kiongozi wa darasa anapaswa kuelezea habari kwa undani zaidi. Katika nyakati nyingine, wanaweza kuingiza mambo mengine mapya yanayoendana na somo hilo. Halafu, siyo lazima mwanafunzi aweze kujibu kwa usahihi kabisa, na siyo lazima aweze kufikia kwenye hitimisho. Swali linawaandaa tu wanafunzi katika kujifunza mambo mapya yanayohusiana na somo.

Siyo lazima kuangalia kila rejeo la Maandiko kutoka katika mabano. Marejeo yametolewa kwa ajili ya kuunga mkono taarifa zilizooanishwa.

Wakati mwingine, rejea itaonyesha wapi pa kupata nyenzo nyingine katika somo au sehemu nyingine ya kozi. Siyo lazima kwenda kuangalia jambo hilo linalohusiana na somo labda kuwepo na hitaji kwamba darasa linahitaji maelezo ya ziada kwa haraka wakati huo huo.

Kiongozi wa darasa anaweza kumwuliza mwanafunzi atoe maelezo kuhusiana na nukuu zilizoko kwenye michoro ya maboksi yanayoenda sambasamba pembezoni mwa masomo.

Masomo mengi yanayo michoro ya maboksi yenye picha na nukuu za kihistoria kuhusiana na Rumi. Rejea hiyo haihusiani na somo. Si lazima kujumuisha rejea ya kihistoria katika uwasilishaji wa somo.

Kwenye mwanzo wa kila kipindi cha darasa, kiongozi wa darasa anapaswa kukusanya kazi za kufanya zilizoandikwa kutokana na kipindi kilichopita na kuongoza kikundi katika kujadili yale waliyoandika.

Kazi za kufanya kwa Wanafunzi

Hili ni darasa la kujifunza Biblia. Wanafunzi watapaswa waweke Biblia zao wazi kwa ajili ya kuangalia kutoka hapo ile sura wanayojifunza.

Chati imewekwa kwa ajili ya kuweka **kumbukumbu za kazi za kufanya zilizokamilika**. Chati hii imechapishwa nyuma ya kitabu cha kozi hii.

Kwenye wiki za mwendelezo wa kozi hii, mwanafunzi`atapaswa aandae mahubiri matatu ya kuhubiri au masomo yanayohusiana na sura yeyote kutoka katika kitabu cha Warumi na kuyawakilisha kwenye makundi mengine yasiyokuwa ya darasa moja. Baada ya kila uwasilishwaji, mwanafunzi atapaswa kuwauliza baadhi ya wasikilizaji wake wamweleze ni

kwa jinsi gani anaweza kuboresha uwasilishaji wake. Atapaswa amkabidhi kiongozi wa darasa nakala ya maelezo yake aliyowasilisha, maelezo ya kikundi na tukio wakati alipokuwa akiongea, na mipango yake ya kuboresha zaidi.

Mwanafunzi atapaswa kuandaa angalau majadiliano na waamini wawili kutoka katika makanisa ambayo yana mafundisho ya imani tofauti na aliyo nayo yeye. Atapaswa awatake wamweleze ni kwa nini wanashikamana na mafundisho ya imani waliyo nayo. Atapaswa awafafanulie kuhusu sura zinazotokana na Kitabu cha Warumi zinazohusika na mada yao. Atapaswa aandike maelezo yanayotokana na majadiliano hayo na ayakabihi kwa kiongozi wa darasa. Itakuwa ni jambo jema sana kama kazi hii ya kufanya itakamilika baada ya kuwa wamejifunza somo la 9.

Kila somo lina **kazi za kufanya kwa kuandika,** Isipokuwa somo la 12. Kila mojawapo katika haya yatapaswa yakamilike kabla ya kipindi kingine kinachofuata kuanza. Kazi za Matendo zitapaswa ziwakilishwe kwa kiongozi wa darasa wakati kipindi cha darasa kinapoanza. Kiongozi wa darasa atapaswa aongoze majadiliano mafupi kuhusiana na kazi za matendo za kufanya za kuandika zilizowakilishwa kwake na wanafunzi.

Kwenye mwisho wa kozi kuna kufanya **mtihani wa mwisho**. Kila mwanafunzi atapaswa akamilishe kufanya mtihani peke yake bila ya kupewa msaada au kuangalia kumbukumbu zozote zilizoandikwa. Orodha ya maswali imeandikwa karibu na mwisho wa kitabu cha kozi hii. Wakati wa kufanyika kwa mtihani wa mwisho unaweza ukawa kwenye kipindi kingine cha darasa kitakachofuata au ukapangwa kufanyika katika wakati mwingine ulio muafaka. Ili kufupisha muda unaohitajika kufanya mtihani, kiongozi wa darasa anaweza kuchagua maswali 20 ya kufanya. Katika kuandika majibu ya maswali 20 kunaweza kuhitajika muda wa saa moja kwa baadhi ya wanafunzi. Wanafunzi hawapaswi wajue ni maswali gani yatakayotumika kwa ajili ya mtihani, na watapaswa wajifunze maswali ya marejeo ya masomo yote.

Wanafunzi wanapaswa wawepo kwenye kila kipindi cha darasa. Kama mwanafunzi atakosekana katika kipindi, atapaswa ajifunze kile kilichokuwa kimefundishwa, afanye marejeo na kiongozi wa darasa, na aandike kazi ya kufanya yaliyotolewa.

Muhtasari wa Kitabu cha Warumi

Sehemu ya 1: Salamu na Utangulizi wa Dhamira (Warumi 1:1-17)

Sehemu ya 2: Umuhimu wa kuhesabiwa haki kwa Imani (Warumi 1:18-3:20)

Kifungu 1: Kosa la Wamataifa: Kumkataa Mungu kwa kuabudu sanamu (Warumi 1:18-32)
Kifungu 2: Kosa la Israeli: Kuwa na maarifa bila ya utii (Warumi 2:1-29)
Kifungu 3: Haki ya Hukumu kwa ajili ya Ulimwengu wote (Warumi 3:1-20)

Sehemu ya 3: Njia na Maana ya kuhesabiwa Haki (Warumi 3:21-5:21)

Kifungu 1: Njia ya Haki ya Mungu ya kuhesabiwa haki (Warumi 3:21-31)
Kifungu 2: Mfano wa Ibrahimu (Warumi 4)
Kifungu 3: Upatanisho wa Kristo (Warumi 5)

Sehemu ya 4: Utakaso wa Waliohesabiwa Haki (Warumi 6-8)

Kifungu 1: Ushindi dhidi ya dhambi (Warumi 6)
Kifungu 2: Hali ya mtu kuwa mwenye hatia (Warumi 7)
Kifungu 3: Maisha katika Roho (Warumi 8)

Sehemu ya 5: Mamlaka ya Mungu kwenye mpango wa Wokovu (Warumi 9-11)

Kifungu 1: Haki ya Mungu katika kupanga Njia ya Wokovu (Warumi 9)
Kifungu 2: Mwitikio wa Imani kama Sharti la Kukubalika (Warumi 10)
Kifungu 3: Kukataliwa kwa Wasioamini; Kukubaliwa kwa Walioamini (Warumi 11)

Sehemu ya 6: Maelekezo ya Vitendo (Warumi 12:1–15:7)

Kifungu 1: Unyenyekevu na Huduma Takatifu katika mwili (Warumi 12:1-8)
Kifungu 2: Mwenendo dhidi ya watu wengine (Warumi 12:9-21)
Kifungu 3: Utii kwa Mamlaka za Kiraia (Warumi 13:1-7)
Kifungu 4: Ukamilifu wa Upendo (Warumi 13:8-10)
Kifungu 5: Kuishi ndani ya Nuru (Warumi 13:11-14)
Kifungu 6: Kukubali tofauti zilizopo katika vitendo vya Kidini (Warumi 14:1–15:7)

Sehemu ya 7: Hitimisho: Maono kwa ajili ya Umisheni mbali mbali (Warumi 15:8-33)

Sehemu ya 8: Salamu (Warumi 16)

Somo la 1
Utangulizi wa Barua

Kitabu cha masuala mengi yaliyofanyiwa Mjadala

Mambo mengi ya kiteolojia yamefanyiwa mijadala katika kanisa kwa karne nyingi zilizopita. Kitabu cha Warumi kinashughulika na masuala tata ya kiteolojia labda kuliko kitabu kingine chochote cha Biblia. Hapa kuna mifano ya maswali yaliyopata majibu katika barua hii.

Maswali ya kiteolojia yaliyopata majibu katika kitabu cha Warumi

Angalizo kwa kiongozi wa darasa: Somo kila swali na toa nafasi ili kuruhusu wanafunzi kadhaa waweze kutoa majibu. Kikundi hakipaswi kitumie muda wake mrefu kwenye kujibu swali lolote na hakipaswi kijaribu kufikia kwenye hitimisho. Kusudi la orodha hii ya maswali ni kuonesha kwamba kuna maoni mengi kuhusiana na maswali haya.

1. Je, mtu anapaswa aamini kitu gani ili aweze kuokoka kwa njia ya imani?
2. Je, inamaana gani kwamba Mkristo hawezi kuupata wokovu wake kwa njia ya njia ya matendo?
3. Je, Mungu aliamua kuokoa baadhi ya watu, na akaamua kuwaacha wengine?
4. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anachagua mtu aliyeokoka na ambaye hajaokoka.
5. Je, ni jambo gani litakalotokea kwa watu ambao kamwe hawajawahi kuisikia injili?
6. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anaweza kuwa mwenye haki kama anasamehe baadhi ya watenda dhambi na wengine kuwaadhibu?
7. Je, mtu aliyeamini ataweza kuwa bado mwenye dhambi?
8. Je, ni ushindi gani wa kiroho unaowezekana kwa ajili ya maisha halisi?
9. Je, kuna uwezekano kwa mtu aliyeokoka kupoteza wokovu?
10. Je, Mungu bado anao mpango kwa ajili ya Israeli?

Kusudi la Waraka kwa Rumi

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 1:11-15 na 15:24 kwa ajili ya kikundi. Je, Paulo alitoa sababu gani za kumfanya atake kwenda Rumi?

Kusudi la barua hii lilikuwa ni kumtambulisha Paulo na teolojia yake ya wokovu kwa waamini wa Kirumi, ili kwamba:

1. Aweze kuwatambelea na kuwatia moyo waamini (1:11-12) na kuihubiri injili katika Rumi (1:15).

2. Aweze kuanza matendo mpya ya umisheni kwa kuungwa mkono na wao (15:24).

Paulo alikuwa ametumia miaka ya 47-57 B.K. akifanya uinjilisti kwenye mataifa yaliyokuwa karibu na bahari ya Aigea. Aliandika barua kwa Warumi katika kama mwaka wa 57 B.K.[1] Alipanga kufanya safari ya kwenda Yerusalemu, kisha Rumi. Paulo alitaka kulitumia kanisa katika Rumi kama kituo chake cha kuzindulia jitihada zake za umisheni za kuingia Hispania (15:24), ambayo zamani ilikuwa koloni la Waruni katika upande wa magharibi na kitovu cha ustaarabu wa Warumi katika sehemu hiyo ya dunia.

Kwa kuwa Paulo alikuwa hajawahi kabisa kuitembelea Rumi, barua ilitumika kama utambulisho wake binafsi na maandalizi kwa ajili ya ziara yake. Labda hii ndiyo sababu ya salamu nyingi alizotoa zilizoko katika Warumi 16.

Ziara ya Paulo katika Rumi haikufanyika kama alivyokuwa amepanga. Alikamatwa akiwa Yerusalemu. Ilipoonekana kwamba hataweza kuipata haki yake, alikata rufaa kwa Kaisari. Baada ya safari yake ngumu na ya hatari ambayo ilikuwa ni pamoja na kuvunjika kwa merikebu yao, aliwasili Rumi kama mfungwa kama mwaka wa 60 B.K. Ingawaje alikuwa ameshikiliwa na kuzuiliwa, alikuwa na uhuru wa kupokea wageni na kuwahudumia pamoja na kuhudumia kupitia wao (Matendo 28:30-31). Paulo alisema kwamba matukio haya yalikuwa yanatokea kwa ajili ya injili kuendelea (Wafilipi 1:12). Kulikuwa na waongofu hata ndani ya nyumba ya Kaisari mwenyewe.

Baadhi ya wanahistoria wanamini kwamba Paulo aliachiliwa baada ya miaka miwili ya kuwa kifungoni. Aidha iwe au isiwe kwamba alifanya safari yake ya kwenda Hispania haifahamiki. Tunachojua ni kwamba hatima yake aliuawa huko Rumi, lakini hii inaweza ilikuwa ni kwenye safari yake ya pili kwenye jiji hilo.

Kwa kuelezea teolojia ya wokovu katika kuonyesha msingi wa matendo yake ya umisheni, Paulo alionyesha msingi wa matendo ya umisheni kwenye maeneo yote na kwa wakati wote.

> "Kwenye ufahamu wa Paulo ilikuwa na kufahamu kwa ufupi katika waraka huu katika ujumla wake kujifunza injili ya Kristo na kuandaa utangulizi kwa yote yaliyohusiana na Agano la Kale."
> - William Tyndale,
> "Prologue to Romans"

Kwa kawaida maswali kadhaa yatainuka kuhusiana na ombi la Paulo alilotaka asaidiwe katika kuzindua safari yake ya umishenari. Baadhi ya watu wanaweza wakauliza, "Je, kwa nini iwe wewe ndiye unayekwenda?' Kwa hiyo, Paulo alianza barua yake kwa kutaka kuelezea kujitoa kwake kwa ajili ya matendo ya injili (1:1) Baadaye akaelezea kuhusu wito wake maalumu na mafanikio yake kama mtume kwa Mataifa (15:15-20).

Mtu mwingine anaweza akauliza, "Kwa nini kila mtu ahitaji kuisikia injili? Inawezekana ujumbe huu wa injili hauhitajiki kila mahali." Lakini Paulo alielezea umuhimu na uzito wa injili kwa wanadamu wote ulimwenguni kote. (1:14, 16, 10:12) na umuhimu wa matendo

[1] Tarehe hizi ni kwa mujibu wa maoni ya wanazuoni, na hatujui kama wako kwenye usahihi kabisa.

ya umishenari (10:14-15). Alionesha kwamba ujumbe wa injili unahusika kwa kila mtu aliyeko duniani, na kwamba kila mtu anahitaji sana kuusikia.

Kifungu cha kujifunza – Warumi sehemu ya 1

Sasa tuangalie kwenye sura ya kwanza – kuhusu Paulo katika salamu na utangulizi.

► Mwanafunzi atapaswa asome Warumi 1:1-17 kwa ajili ya kikundi.

Roma

Jina la jiji la Roma linatokana na jina Romulus. Hadithi ni kwamba wana mapacha wa mungu wa Mars, aitwaye Romulus na Remus ambao walilia wakiwa Watoto wachanga. Walilelewa na mbwa mwitu. Walipofikia uzima, waliamua kujenga jiji. Walikuwa na ushindani, na Romulus akamwua Remus.

Maelezo kuhusu Muundo

1:1-17 inaelezea wito wa Paulo na uhamasishaji wake wa kuineza injili. Baada ya hapo, 1:18-3:20 inaelezea ni kwa nini injili ni muhimu, kwa sababu wenye dhambi ambao hawajaokoka wako chini ya laana ya Mungu. Hata hivyo, 1:15-19 kuna kufanyika kwa mpito kati ya sehemu hizi mbili. Yenyewe imejitengenezea hatua, ikielezea injili kwa ufupi: kwamba watenda dhambi wana hatia kwa sababu wanajua zaidi, na kwamba, wako chini ya ghadhabu: lakini mtu aliyeamini ameokolewa.

Jambo kuu katika 1:1-17

Paulo aliitwa na kuhamasika kuieneza injili kwa sababu ni ujumbe wa wokovu kwa kila anayeamini.

Muhtasari wa 1:1-17

Kila kitu kwenye 1:1-14 kinaelekea kwenye taarifa iliyoko katika 1:15. 1:16-18 zinaelezea kwa ufupi injili ni nini na ni kwa nini kila mtu anaihitaji. Kwa kuwa wokovu ni uweza wa Mungu uletao msamaha na watu wanaupokea kwa imani. Sababu ya watu wote kuwa wahitaji wa ujumbe huu ni kwamba wako chini ya ghadhabu ya Mungu.

Kitabu chote cha Warumi ni mwendelezo wa maelezo ya taarifa zilizoko katika 1:16-18.

Maelezo ay Aya-kwa-Aya

(Namba zilizo katika mabano ni namba za kuonesha aya zinazojadiliwa.)

(1:1) Paulo alitoa taarifa tatu zinazohusiana na yeye mwenyewe.

- Kwamba alikuwa ni mtumwa wa Yesu Kristo.
- Kwamba alikuwa ni mtume kwa sababu wito wa Mungu kwake ulimfanya awe hivyo.
- Kwamba alikuwa sehemu ya kazi ambayo alikuwa ameitiwa.

Paulo hapo kwanza alikuwa Mfarisayo, lakini sasa alikuwa amejitolea kwa ajili ya huduma. Paulo alikuwa na uraia wa Kirumi, lakini hakutaja ukweli huo kama sehemu yake ya

utambulisho. Kama angefanya hivyo, haingeweza kumsaidia kuchangamana na waamini wengi wa Kirumi. Watu wengi waliokuwa wanaishi Rumi hawakuwa na uraia kwa sababu walikuwa ni wageni au watumwa. Kama ingetokea Paulo akataja uraia wake, ingepelekea yeye kuwekwa katika daraja la juu katika Rumi: ilikuwa ni muhimu kwake kutambulisha jukumu lake la kiroho.

(1:2) Injili haikuwa ni mpya kabisa lakini ilikuwa ndani ya ujumbe wa manabii wa Agano la Kale. Warumi 4 inaonesha hasa kwamba injili ilikuwa inaeleweka kwa Ibrahimu na Daudi.

(1:3-4) Katika hali yake ya asili, mwana wa Mungu alikuwa ni wa uzao wa Daudi kwenye mtiririko wa kifalme ambao ulikuwa umetabiriwa kwa ajili ya Masihi.

Kristo ni neno la Kigiriki linalotokana na neno la Kiebrania *Masihi*.

Neno *Bwana* linarejelea uungu wake. Umuhimu wa neno *Bwana* katika nyaraka za Agano Jipya zinaweza kuonekana zikifanana ukilinganisha Wafilipi 2:10-11 na Isaya 45:23. Ni marejeo kuhusu mmoja aliye mkuu sana juu ya mamlaka nyingine zote. (Ona pia Matendo 2:36.)

Neno *Bwana* halina ulazima wa kumaanisha kitu kile kile katika Injili za Agano Jipya, wakati ambapo watu wangeweza kumwita Yesu "Bwana" kama neno la heshima bila ya kuelewa kwa uhakika kwamba alikuwa ni Mungu.

Katika Nyaraka za Agano Jipya, neno "Yesu Kristo Bwana wetu" linatoa utambulisho wa aina tatu tofauti. Linasema kwamba yeye ni mtu wa kihistoria aliyeitwa Yesu, yeye ni Masihi wa Kiyahudi, na yeye ni Mungu.

Ufufuo ulithibitisha uungu wa Yesu. Katika Yohane 10:18, alijinadi kwamba anaweza akaurejesha uhai wake tena. Aliufanya ufufuo kama alama ya kizazi kile, na mashuhuda wa ufufuo waliufanya kama ni alama kwa ajili ya vizazi vyote. Mtu ambaye siyo Mungu hawezi akajifufua mwenyewe kutoka katika wafu; aidha Mungu hangeweza kumfufua mtu anayejinadi kwa upotofu kwamba yeye ni Mungu, hasa mtu anayejinadi kwamba ufufuo utathibitisha utambulisho wake.

► Watu wengine waliwahi kufufuliwa kutoka katika wafu, lakini hawakuwa Mungu. Ni kwa jinsi gani utaweza kuelezea kwamba ufufuo ulithibitisha uungu wa Yesu?

(1:5) Wito na karama za kiroho za kitume zilitolewa kwa kusudi la kuwaleta watu wote wa mataifa yote kwenye utiifu kwa Kristo. Njia pekee ya matumizi sahihi ya karama za kiroho ni kwa ajili ya matendo ya Bwana. Lengo pekee la matendo ya huduma ni kwa ajili ya utukufu wa jina la Kristo. Malengo kama ya mafanikio binafsi au umashuhuri wa binafsi ni mambo yasiyofaa kwa mtumishi wa Mungu.

Upekee wa Wito wa Utume

► Je, siku hizi wako mitume walio hai?

Neno *mtume* wakati mwingine linatumika katika Biblia katika maana yake ya ujumla ya "mtu anayetumwa." Katika Matendo 14:14, Paulo na Barnaba wanaitwa mitume, ingawaje Barnaba hakuwa mmojawapo katika mitume halisi kumi na mbili wa awali. Katika Wagalatia 1:19, Paulo alisema kwamba katika safari yake moja maalumu hakuwahi kumwona mtume yeyote Zaidi ya Kefa (Petro) na Yakobo nduguye Bwana Yesu, Kwa hali hiyo, alimtaja Yakobo kama mtume, ingawaje hakuwa miongoni mwa mitume kumi na mbili wa awali.

Hata hivyo, mitume kumi na mbili wa awali kwa kawaida walichukuliwa kama ni kundi maalumu, ambalo hakuna mtu mwingine atakayeongezwa katika kikundi hicho. Katika Mathayo 10:2 panasema, "Na majina ya hao mitume kumi na wawili ni haya…" (Angalia pia katika Luka 6:13). Yesu aliwaambia mitume kwamba wataketi katika viti vya enzi, huku wakiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli, (Luka 22:30). Ahadi inaonekana kuwa ni zawadi maalumu kwa mitume kumi na mbili pekee. Majina ya mitume kumi na mbili yako katika misingi kumi na mbili ya jiji la Mungu, jambo linaloonyesha upekee wa kundi hili la mitume kumi na mbili (Ufunuo 21:14).

Yuda aliyekuwa nduguye na Yesu hakujiita mwenyewe mtume lakini alirejea kwenye mamlaka yao (linganisha Yuda 17 na 2 Petro 3:2). Mitume walikuwa na mamlaka ya kipekee, na lolote waliloandika kwa ajili ya makanisa lilichukuliwa kama ni ufunuo (2 Petro 3:15-16).

Kanisa lilimteua Mathiasi kuwa badala ya Yuda, kwa kutegemewa kwamba kungekuwepo na mitume kumi na mbili (Matendo 1:26); lakini hatuoni kutoka katika historia kwamba kanisa la mwanzo lilikuwa linaendelea kuweka mitume badala ya wale waliokuwa wakifariki.

Paulo aliitwa kuwa mtume (Rum 1:1). Paulo anaashiria kuwa mojawapo ya sifa yake ya kuwa mtume ni kwamba alikuwa amemwona Yesu. (1 Wakorintho 9:1). Hali hiyo inaweka ukomo wa utume kwenye kizazi cha kwanza cha kanisa.

Kifungu cha kujifunza – Warumi sehemu ya 1

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(1:6) "Kuitwa" kunahusika na wito wa kuokoka, kuwa watu watakatifu, kama inavyoonekana kwenye aya inayofuata. (Ona pia 8:30). Paulo alikuwa amesema kwamba mitume wana huduma kwa ajili ya mataifa yote; na sasa anaonesha kwamba Wakristo wa Rumi ni waamini waliotokana na ujumbe wa mitume. Kwa hali hiyo anaonyesha kwamba wanapaswa na wanawajibika kuzingatia kwa umakini sana mamlaka yake ya kitume. Waraka huu haukuwa umetokana na mmisionari wa kawaida waliokuwa wamewahi

kumsikia. Walikuwa makini katika kumsikiliza na kumheshimu, ingawaje hakuwa mwanzilishi wa kanisa lao.[2]

(1:7) Kuitwa kwenye wokovu ni kuitwa kuwa mtakatifu. Taarifa hii inalinganishwa na iliyoko kwenye aya ya 1, ambapo Paulo alisema kwamba alikuwa ni mtume kwa sababu ya kuitwa kuwa mtume. Haina maana kwamba alikuwa anajaribu au anategemea kuwa mtume, bali alikuwa amefanywa kuwa mtume kwa njia ya wito. Waamini wa Rumi walifanyika kuwa watakatifu kutokana na wito wa kuwa watakatifu. Kama ilivyo kwa wito wa kuwa mtume kuambatana na karama za kiroho na uwezo kwa ajili ya huduma hiyo, wito kwa ajili ya kuwa watakatifu unaambatana na uweza na utakaso unaotufanya sisi tuwe watakatifu. Wito wa Mungu siku zote unaambatana na neema ya kuwezesha kutekeleza huo wito.

Utakatifu uanzapo wakati wa kuokoka huwa haujakamilika katika nyanja zake zote. Mtu aliyeamini anapaswakuwa na mabadiliko endelevu ya maisha yatakayofanania ukweli wa Mungu jinsi atakavyokuwa anaendelea kujifunza ukweli huo. Utakatifu siyo mkamilifu wakati mtu anapookoka; bali utakatifu unaanzia kwenye kuokoka wakati mwenye dhambi anapotubu, anapojiachilia kabisa kumtii Mungu na kufanywa kiumbe kipya (2 Wakorintho 5:17).

(1:8) Neno *dunia* lilikuwa linatumika kikawaida katika kurejelea kwenye dunia iliyokuwa inajulikana na ambayo ilikuwa ya kistaarabu na siyo ulimwengu wote. Injili ilikuwa bado haijaenda kila mahali ulimwenguni.

(1:9) "Neno *latreuo* [Ninatumika] liko ndani ya Agano Jipya na siku zote linatumika kwenye huduma za kidini… Huduma hii inaweza ikahusisha aidha kuabudu au kwenye shughuli nyingine za utendaji za nje zinazohusiana na mambo ya kidini."[3] Paulo alimtumikia Mungu siyo kwa jinsi ya shughuli za kidini tu, bali kwa roho yake.

(1:10-12) Hapa Paulo aliwaambia kwamba amepanga kuitembelea Rumi. Alitaka kuwajenga kiroho na alijua kuwa imani ya kila mtu ingefarijiwa.

Maelezo ya Paulo yanatuambia kwamba waamini wanafaidika kiroho kutokana na kushirikiana wenyewe kwa wenyewe. Roho Mtakatifu hukamilisha matendo yake makubwa ndani ya waamini kupitia kwa waamini wengine. Mtu anayepuuzia uhusiano wake na waamini wengine anapoteza neema ya uwezeshwaji inayokuja kupitia ushirika wa pamoja. (Paulo alizungumzia kwa mapana sana kuhusu hitaji alilo nalo kila Mtu aliyeamini kwa ajili ya waamini wengine katika 1 Wakorintho 12.)

(1:13) Paulo alizuiwa katika mpango wake wa kwanza wa kuwatembelea – siyo kutokana na matatizo, bali kutokana na kipaumbele chake cha kuhubiri injili katika mahali ambapo ilikuwa haijawahi kuhubiriwa au kusikika (ona 15:20-22). Kwa kuwa injli ilikuwa tayari imeshahubiriwa katika Rumi, Paulo alikwenda kwanza katika maeneo mengine. Hata hivyo,

---

[2] Ona kidokezo katika 1:14-15.
[3] Charles Hodge, Maelezo ya Warumi, Waefeso na Wakorintho wa Kwanza, https://www.studylight.org/commentaries/eng/hdg/romans-1.html#verse-9

ujio wake wa sasa haukuwa kinyume na kipaumbele chake kwa kuwa ziara yake ingekuwa ni hatua moja katika kufika kwenye eneo lingine ambalo halijawahi kufikiwa na injili. (15:23-24).

(1:14) *Wayunani* walikuwa ni watu wa utamaduni na waliokuwa wamestaarabika kutokana na ushawishi wa Kiyunani. Neno *mshenzi* linamaanisha "mgeni," likihusisha mtu aliyetoka kwenye utamaduni wa kijahilia zaidi ambao ulikuwa bado haujaguswa na utamaduni wa Kiyunani. Wayunani waliwachukulia hawa washenzi kama watu wasiokuwa na ustaarabu na tena ni wajinga.

Neno *hekima* linahusika na watu waliokuwa wameelimika, hasa katika falsafa ya Kiyunani; Watu *wasiokuwa na hekima* walikuwa ambao ni bado hawajaelimika kwa kiwango cha juu. Paulo alionesha kwamba huduma yake haikuwa na ukomo kwa ajili makundi malumu ya watu. Hali hii ilimwezesha kuandaa huduma yake kwa ajili yao, pamoja na kuonesha jukumu lake kama mmishenari.

Paulo alisema kwamba alikuwa na deni kwa kila mtu aliyekuwa na hitaji la kuisikia injili. Paulo hakuwa na deni kwa sababu wenye dhambi walistahili kusikia, bali ni kwa sababu alikuwa amepokea neema na alikuwa na wajibu wa kuitoa neema hiyo.

Kielelezo: Kama endapo mtu atampatia Elifuraha fedha ili ashirikiane na Yohane, Elifuraha sasa anadaiwa deni na Yohane hata kama Yohane hakufunya jambo lolote katika kujipatia fedha hizo. Katika hali kama hii, tunalo deni kwa wale ambao hawajawahi kuisikia injili, kwa sababu Mungu ametupa sisi jukumu la kushirikishana injili hiyo pamoja nao.

► Je, kila Mkristo analo deni analodaiwa la kushirikisha injili kwa wengine?

(1:15) Paulo alikuwa amehubiri kwa wayunani na washenzi, na sasa alikuwa anatamani kuhubiri injili kwa watu wa Rume vile vile.

Anaanza kutoa hoja yake kwa kusema, "mimi ni tayari kuihubiri Injili hata na kwenu," kisha akaelezea kwa kifupi injili ni nini na ni kwa nini dunia inaihitaji. Ufafanuzi huu kwa ufupi umepanuliwa vizuri katika waraka wote.

1:14-15 inatuonyesha tena ni kwa nini Paulo alikuwa na sifa za kuja kwao. Alikuwa na ujumbe uliomhusu kila mtu katika ulimwengu huu.[4]

(1:16) Injili ni kwa ajili ya Wayahudi na Wayunani, na mada hii inatambulisha kichwa cha habari juu ya Wayahudi na Wamataifa na msimamo wao mbele ya Mungu. Mada hii inaendelea hadi kwenye Warumi 3. Paulo haionei haya injili hata ingekuwa katikati ya mamlaka ya dola, kwa kuwa injili ni uweza wa Mungu.

Nguvu ya Mungu inatenda kazi katika ujumbe wa injili, ikiufanya ujumbe huo uwe na uwezo wa kuokoa. Amri za Mungu siku zote zinaambatana na nguvu inayohitajika katika

[4] Ona maelezo 1:5-6.

kuzitekeleza. Nguvu ya Mungu iko katika matendo wakati yanaposemwa maneno yake.[5] Wapelekaji wa injili wanategemea nguvu iliyoko ndani ya injili kwa sababu wanapokuwa wanawakilisha ujumbe, Roho Mtakatifu huufanya ujumbe huo uwe na ushawishi na uwezeshaji kwa wasikilizaji.

Kwa Paulo, kusimama kwa ajili ya injili hakukuwa na maana tu ya kuitetea injili kama ukweli halisi, lakini pia kuihubiri kama ukweli unaobadilisha. Aliitangaza kwa ujasiri kwamba itawabadilisha wasikilizaji wake.

► Je, kwa nini tunapaswa kuwa na ujasiri wakati tunapohubiri injili?

(1:17) **Mtu anafanywa mwenye haki kwa Imani na ataishi kwa imani.**[6] Huu ni ukweli mkuu na muhimu katika kitabu cha Warumi.

Waraka wote wa Warumi unashughulika na jinsi ambavyo mwanadamu anaweza kufanywa mwenye haki (kuwa na haki itokanayo na Mungu). Umuhimu wa suala hili unaoneshwa katika aya inayofuata, kwa maana ghadhabu ya Mungu iko tayari kwa wale wanaobakia kuwa wenye dhambi.

> "Warumi ni sehemu kuu ya Agano Jipya na ni injili halisi."
>
> - Martin Luther

Haki ya Mungu inayozungumziwa hapa siyo "ile sifa yake ya kuwa mwenye haki… bali haki inayotiririka kutoka kwake na kukubaliwa na yeye,"[7] haki ya Mungu inayofanya kazi ndani ya wanadamu kupitia katika imani yao. Wazo linalofanana na hili liko katika Wafilipi 3:9: "Haki ile itokayo kwa Mungu, *(ek)* kwa imani." Watu hawahesabiwi kuwa wenye haki tu kwa sababu ya msamaha, lakini wanaanza kuwa wenye haki kwa ukweli kwa sababu Mungu amewabadilisha.

> "Nia ya jumla ya barua hii ni kuutangaza umilele, kusudi au amri ya Mungu isiyobadilika, ambayo ni: 'Kila aaminiye ataokoka: Kila asiyeamini ataangamia.'"
>
> - John Wesley, "Predestination Calmly Considered"

Ukiendelea zaidi kwenye hiyo barua (Warumi 3:21-22), Paulo alisema kwamba wenye haki wa Mungu ambao ni kwa njia ya imani katika Yesu ni kwa ajili ya wale wote ambao wataamini. Katika Warumi 5:17-19 tunasoma kuhusiana na karama ya haki ambayo hufanya watu wengi kufanyika wenye haki.

Maneno "kutoka imani hadi imani" yanasisitiza kwamba imani ndiyo njia peke yake ya kupata haki. Msisitizo huu unaendana na dhana ya Kiprotestanti ya imani peke yake kama hitaji la kupata wokovu.

Katika kitabu cha Warumi, neno *kifo* linahusika na hukumu ya Mungu. Wale tu wanahesabiwa haki kwa Imani wataishi – hiyo ni kusema wataepuka hukumu (angalia 1:18)

---

[5] Ona pia 1 Petro 1:23 & 25, Warumi 1:16, Waebrania 4:12, 1 Wakorintho 1:18, Ezekieli 37:7-10 na Isaya 55:11.

[6] Paulo alikuwa akinukuu Habakuki 2:4.

[7] Henry Alford, *The Greek Testament Critical Exegetical Commentary* (*Agano ya Kiyunani*), Warumi 1:17 https://www.studylight.org/commentaries/eng/hac/romans-1.html

Laana ya Mungu itamwagwa juu ya watu wote isipokuwa tu kwa wale watakaoepuka kwa njia hii.

► Je, inamaanisha nini kwamba mtu anafanywa mwenye haki kwa imani?

► Kwenye kifungu hiki, je, inamaanisha nini kuishi? Kifo ni nini? Inamaanisha nini kuishi kwa njia ya imani?

Wanateolojia watatu waliobadilishwa na Kitabu cha Warumi

Waraka bado unahifadhi kusudi lake la awali la kutoa msingi wa matendo ya umishenari. Hata hivyo, waraka huu unafanya zaidi ya hapo. Wakati Paulo alipokuwa akielezea ni kwa nini kila mtu anapaswa asikie ujumbe, alielezea kwa kinagaubaga kwamba ujumbe ulikuwa ni nini na kwa nini watu wanaweza tu kuokolewa kupitia njia hii. Alijihusisha na baadhi ya vipingamizi vya kawaida. Maelezo haya na utetezi wa ujumbe aliouhubiri unachukua sehemu kubwa ya kitabu na unathibiti muundo wake.

Warumi ni maelezo kuhusu teolojia ya wokovu. Teolojia ya wokovu ya Paulo ilitoa utetezi wa haraka dhidi ya Wayahudi,[8] na unatumika pia kufanya masahihisho yaliyopo wakati huu wa sasa kwenye mafundisho ya imani kuhusiana na wokovu.[9]

> "Kila mtu akielewa waraka huu, tayari anapata njia ya kuelewa Maandiko yote."
>
> - John Calvin

Kupitia historia, Mungu amekuwa akitumia waraka huu wa Warumi katika kurejesha kweli nyingi muhimu za msingi katika wakati ambapo zilikuwa zimesahaulika.

Akiwa kijana, Augustine alitafuta kuridhika katika uhusiano wa uovu na falisafa na masomo ya taaluma. Aliitafuta kweli na akaipata katika ukristo. Lakini bado kuipenda dhambi kwake kukamfanya kuwa mateka. Akajiona kuwa yeye ndiye mtu anayeelezewa katika Warumi 7. Aliijua kweli lakini akawa hana uwezo kabisa wa kuishi maisha yenye haki.



Augustine

Mwaka 386 BK, baada ya kusoma Rum 13:13-14, katika umri wake mwanzoni mwa miaka thelathini, Augustine aliamua kuacha maisha yake ya dhambi. Mungu alimfungua kutoka vifungo vya dhambi na kumwezesha kuishi maisha ya utauwa katika Yesu Kristo.

Katika miaka iliyobakia ya uhai wake, Augustine[10] Mungu alimtumia Augstine kwa nguvu. Maandiko yake yalitetea mafundisho ya kweli dhidi ya falisafa za uongo. Wazo maarufu lililokuwapo wakati huo ni imani kuwa watu ndani yao wana uwezo kuwa wenye haki na kwa hiyo wanaweza kuchagua kutokuwa wenye dhambi. Kutoka Warumi 5, Augustine

[8] Wayahudi wanaelezewa baadaye katika fundisho hili.

[9] Warumi na Wagalatia mara nyingi wanawekwa katika fundisho la pamoja, kwa sababu Wagalatia kwa kiwango kidogo wanahusika kwa kina na baadhi ya mambo ya kufanana ya dhamira mbalimbali za injili.

[10] Picha: "Saint Augustin", na Jusepe de Ribera, Goya Museum, imepakiwa na Aristoi, imepatikana kutoka https://commons.wikimedia.org/wiki/index.php?curid=72972944, mali ya umma.

alifundisha kuwa watu wanazaliwa wakiwa na dhambi ya asili ambayo huwafanya kutomtii Mungu. Asili hii hufanya kuwa vigumu mtu kumpendeza Mungu kikamilifu usipohitaji neema yake. Augustine alifundisha na akashuhudia neema ya mungu kwamba huwafanya watu kuwa wenye haki mbele ya Mungu.

Martin Luther

Katika mwaka 1515 B.K., Martin Luther alielewa maana ya Warumi 1:17 baada ya kuwa ametafuta kwa miaka mingi kuhusu uhakika wa wokovu.[11] Luther alikuwa ameshajaribu kutafuta amani ya kiroho kwa kufuata maisha ya utawa kwa bidii ya ziada. Aliomba kwa kufunga, alifuata ibada zote za Ukatoliki, na hata alijipiga mwenyewe. Ni wakati alipokuwa akitambaa kwa magoti yaliyokuwa yakivuja damu kwenye ngazi za kuingia kwenye Kanisa la Mtakatifu Petro katika mji wa Roma alipopokea kwa ghafla ufahamu wa neema kutoka kwa Mungu kwa njia ya imani.

Aliona kwamba mtu ambaye ataepushwa na hukumu ya Mungu ni yule tu ambaye anaamini ahadi ya Mungu ya kusamehe. Uhakika huu ulifanyika ni msingi wa ujumbe wake kwamba imani peke yake ndio njia inayoweza kutufanya tuokolewe.



John Wesley

Kwenye mwaka wa 1738 B.K., John Wesley alipata uhakika binafsi wa wokovu aliokuwa ameutafuta kwa miaka mingi.[12] Wesley alikuwa mwanazuoni wa Biblia mwenye bidii kubwa na aliyeishi kwa uangalifu katika Maisha yake ya kidini. Alishawahi hata kwenda kwenye umishenari kwa miaka miwili kwa wenyeji wa Kihindi wa Amerika lakini hakuwahi kupata uelewa sahihi wa injili yeye mwenyewe. Akiwa kwenye meli wakati kukiwepo na mawimbi baharini, aliona familia ya Kimoraviani ambayo ilikuwa imekaa kwa amani kabisa ikimtumainia Mungu na haikuwa na hofu ya kifo, na Wesley alitambua kwamba alikuwa hana imani ya aina hiyo.

Wesley aliona katika Maandiko kwamba kubadilika ni kitendo kinachofanyika kwa haraka. Pia alikutana na ndugu wawili wa Kimoraviani ambao walimshuhudia kwamba walikuwa na uhakika binafsi wa wokovu. Alianza kutambua kwamba alihitaji kupata uzoefu kamili wa kuongoka. Mabadiliko yake yalitokea alipokuwa kwenye kikao nyumba fulani kwa ajili ya kujifunza na kuomba. Wakati mtu fulani akisoma kile Martin Luther alichoandika kuhusu kitabu cha Warumi, Wesley alisikia moyo wake "ukiwaka moto kimaajabu." Akasema, "Ninajisikia kuwa mtu niliyemwamini Kristo, Kristo peke yake kwa ajili ya wokovu wangu: na nikapewa uhakika kwamba amezichukua dhambi **zangu** na ameniokoa kutoka katika sheria ya dhambi na kifo."[13]

---

[11] Picha: "Martin Luther, 1529" na Lucas Cranach the Elder, imepatikana kutoka https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Martin_Luther,_1529.jpg, mali ya umma.
[12] Picha: "Bildnis des John Wesley", na John Greenwood, imepatikana kutoka Leipzig University Library https://www.flickr.com/photos/ubleipzig/17059576182/, mali ya umma.
[13] John Wesley, *The Works of John Wesley, Vol. I* (Kansas City: Nazarene Publishing House), 103

Kutokana na watu wote hawa watatu, kuelewa ujumbe kulileta uhamasisho wa bidii sana ya uinjilisti. Kitabu hiki bado kinaendelea kukamilisha kusudi lake na kutoa msingi wa huduma za umisheni kwa kuelezea teolojia ya wokovu.

► Je, kuna athari gani unazoweza kufikiria ambazo kitabu cha Warumi kinaweza kuwa nazo kwenye maisha na huduma yako?

Maswali ya Mapitio Somo la 1

(1) Je, kwa nini Paulo aliandika waraka kwa Warumi kwa waamini wa Rumi?

(2) Je, kwa nini Paulo alipanga kwenda Rumi?

(3) Je, Maana ya msemo *Yesu Krsito Bwana wetu* una maana gani katika nyaraka za Agano Jipya?

(4) Je, ufufuo unathibitishaje uungu wa Yesu?

(5) Elezea msemo *wasio wayunani* (Warumi 1:14).

(6) Kwa nini Mwinjilisti Paulo ana deni la kuhubiri injili?

(7) Je, ni kitu gani kikuu na ukweli muhimu katika kitabu cha Warumi?

(8) Je, kifo kina maana gani katika kitabu cha Warumi?

(9) Kulingana na Warumi, ni nani analindwa asipate hukumu ya Mungu?

Kazi ya kufanya Somo la 1

(1) Kwa kutumia kifungu kutoka katika somo hili, andika ukurasa mmoja kuhusu huduma ya injili. Elezea kuhusu wito kwenye huduma, deni alilo nalo mwinjilisti kwa ajili ya wale wenye hitaji la kuisikia, na kuhusu nguvu ambayo Mungu hutoa kwa ajili ya ujumbe unaotolewa.

(2) Kwenye wiki kadhaa za kozi hii, utaandaa masomo ya mahubiri matatu yenye msingi wake kutoka katika kitabu cha Warumi na uyawakilishe kwenye vikundi vingine visivyokuwa darasa lako. Kila baada ya kuwasilisha, utawauliza wasikilizaji wako ni kwa jinsi gani uwakilishwaji huo unaweza ukaboreshwa. Utapaswa umpe kiongozi wa darasa nakala ya kumbukumbu ya yale uliyowasilisha, maelezo ya kikundi na tukio ulikofanyia uwasilishaji, na mipango yako ya kuboresha uwasilishaji ulioufanya.

Somo la 2
Kosa la Wamataifa

Kanisa la Rumi

Jiji la Rumi

Wakati ule wa Paulo, jiji la Rumi ndilo lililokuwa kubwa kuliko yote duniani, likiwa na wakazi zaidi ya milioni moja.[14] Kulikuwa na mchanganyiko wa makundi mbalimbali ya kikabila, lugha, na dini. Wengi wa watu walikuwa ni watumwa.

Wamisionari wa kwanza katika Rumi

Hatuwezi kujua ni mtu gani aliyekuwa wa kwanza kupeleka injili katika Rumi. Kwenye siku ya Pentekoste, Wayahudi walikuwepo kutokea Rumi (Matendo 2:10). Wale waliokuwa wamebadilishwa na au kuokoka kwa hakika walichukua ujumbe wa injili wakati wa kurejea Rumi. Tangazo lao kwamba Masihi alishakuja lilisababisha mshangao na utata. Injili iliisambaa kwa haraka miongoni mwa Wamataifa ambao tayari walikuwa wanaiheshimu dini ya Kiyahudi.

Kanisa la Wamataifa

Ingawaje Wayahudi wanatamkwa kwenye sehemu za barua hii, kanisa lililokuwa Rumi lilikuwa na wingi wa watu wamataifa. Paulo aliwaita wamataifa (1:13-15) na akasema kwamba kwa sababu alikuwa ni mdeni kwa Wayunani na watu wote waliojulikana kama washenzi, alikuwa tayari kuhubiri kwa Warumi. Hata hivyo, ushawishi wa Kiyahudi katika kanisa la Rumi ulikuwa wenye nguvu sana, kwa kuwa waamini wa kwanza katika eneo hilo walikuwa ni Wayahudi. Inawezekana kwamba injili ilikuwa bado haijaelezwa kwa ufasaha katika njia ambayo ingewaonesha waamini uhuru wao wa kutoka katika sheria za Kiyahudi.

Kifungu cha kujifunza – Warumi sehemu ya 2

Kwa kuwa kusudi la Paulo lilikuwa ni kuendeleza kazi ya kimisheni, swali ambalo kwa kawaida ni lazima lingejitokeza ni, "Je, kila mtu kweli anahitaji kuhesabiwa haki kwa njia ya imani?" Pamoja na hayo, kuna mambo ambayo siyo kila mtu anayahitaji. Watu walioko sehemu za maeneo ya barafu ya Arctic hawahitaj mtu yeyote awaletee barafu, na watu wanaoishi kwenye majangwa hawahitaji mchanga.

Labda mtu anaweza akafikiria kwamba kuhesabiwa haki kwa njia ya imani siyo kitu ambacho kila mtu katika dunia hii ni lazima ahitaji; inawezekana baadhi ya watu wamekuwa wakiishi kwenye maisha ya haki na tayari wamekubaliwa na Mungu. Sehemu ya 2 ya barua

[14] Bruce Wilkinson & Kenneth Boa, *Talk through the New Testament*, 375

(1:18-3:20) imeandikwa ili kuonyesha kwamba kila mtu anahitaji kuhesabiwa haki kwa njia ya imani na, kwa hiyo, wanahitaji ujumbe unaohusiana na hilo.

Jambo kuu katika 1:18-3:20

Kila mtu katika ulimwengu huu amekiuka matarajio na mahitaji ya Mungu na yuko chini ya laana. Hakuna mtu yeyote anayeweza tena kuokolewa kwenye msingi wa kutimiza matarajio na mahitaji ya Mungu kwa sababau kila mtu tayari alishakuwa mkiukaji wa mambo yote.

Muhtasari wa 1:18-3:20

Kwanza, Paulo anaelezea hali ya Wamataifa wapagani waliokuwa hawana neno la Mungu lililovuviwa kwao na inaonesha kwamba walikuwa wamekataa kuwa na ufahamu wa Mungu aliowaonesha kwenye uumbaji. Kisha, anaelezea hali ya Waisraeli, ambao walikuwa na neno la Mungu lililokuwa limeandikwa lakini hawakulitii. Anahitimisha kwa kuelezea hali ya ujumla ya dhambi ya dunia. Hitimisho ni kwamba dunia yote ina hatia mbele za Mungu. Injili inahitajika kwa sababu hakuna mtu yeyote anayeweza kuokoka kwa kuwa ana stahili mwenyewe.

Kwa ajili ya masomo haya, sehemu ya 2 (1:18-3:20) itagawanywa kwenye vifungu vitatu. Kwenye somo hili, tutajifunza kifungu cha kwanza (1:18-32).

Kifungu cha kujifunza – Warumi sehemu ya 2, kifungu cha 1

1:18 ni aya ya mpito kati ya kifungu hiki na kifungu kilichotangulia.

Jambo kuu katika 1:18-32

Mataifa walikuwa na msingi wa ufahamu wa Mungu, lakini wakaukataa huo ufahamu na kugeukia kwenye kuabudu sanamu, wakawa watu waliokengeuka sana.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1:18-32 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(1:18) Mungu amewapa ufahamu wa msingi kuhusiana na yeye mwenyewe. Wanaukandamiza ukweli. Hii inaonesha kwamba walikuwa na sehemu ya ukweli kama aya inayofuata inavyoelezea. Hukumu yao ni kwamba wameukataa ukweli waliokuwa nao. Neno "*Uasi*' linaelezea kosa la kidini na linajieleza lenyewe kama kuabudu sanamu, ibada ya kuabudu zaidi kiumbe kuliko kumwabu Mwumbaji (1:19-23). *"Uovu"* inamaanisha ukaidi wa maadili na inaoneshwa kwenye suala la uasherati na uovu (1:24-32)."[15]

Ukweli walioukandamiza umebainishwa kwenye 1:20. Unahusisha ufahamu wa malaka ya Mungu uliokuwa juu yao. Mfumo wao wa maisha unadhihirisha kwamba wanayakataa mamlaka ya Mungu. Katika ulinganifu, maisha ya kuishi kwa kumfanania Kristo yanaonesha

[15] Imebadilishwa kutoka William Greathouse, "Romans", in *Beacon Bible Commentary*, Vol VIII. (Kansas City: Beacon Hill Press, 1968) 50.

kujisalimisha na kujikabidhi kwenye mamlaka ya Mungu, kwa pamoja katika yale anayoyatenda na yale ambayo hayatendi.

Aina za Ufunuo – Maalumu na wa msingi

► Je, kuna baadhi ya njia gani ambazo ukweli wa Mungu hudhihirishwa kwa watu wote?

Kwa kuwa umedhihirisha ukweli kwa njia nyingi, tunazungumzia kuhusu aina mbili: Ufunuo wa msingi na Ufunuo Maalumu. Paulo anarejelea kwenye hizi aina mbili kwenye kitabu cha Warumi, ingawaje siyo kwa kutumia maneno haya.

Ufunuo wa Jumla ni kile ambacho tunaweza kukifahamu kuhusiana na Mungu kwa kuanagalia uumbaji wake. Tunauona ujuzi wa ajabu na wa kushangaza na nguvu za Mungu katika uumbaji wa ulimwengu.

Tunaona umuhimu wa Mungu katika njia ile ambayo mwanadamu ameumbwa. Ukweli kwamba tunaweza kufikiri na kuwa na sababu, tunaweza kukubaliana na uzuri, na tunaweza kuelezea tofauti kati ya jema na baya, (ingawaje siyo ya uhakika) inatuonyesha kwamba Muumbaji wetu anazo sifa hizo katika kiwango cha juu. Tunajua kwamba Mungu anaweza kufikiri na kuwasiliana kwa sababu tunao huo uwezo (Ona Zaburi 19:1-4 na 94:9).

Kwa kuwa Ufunuo wa msingi unaonyesha kwamba Mungu anaweza kuzungumza, tunatambua kwamba Ufunuo Maalumu unaweza ukatokea. Mungu ni nafsi[16] na mwenye uwezo wa kuzungumza na viumbe wake wenye busara. Hiyo inatusaidia sisi kutambua kwamba kunaweza kuwepo na jumbe mbalimbali kutoka kwa Mungu na hata kitabu kutoka kwa Mungu.

Kwa kupitia Ufunuo wa Msingi, hata bila ya Maandiko, watu wanajua kwamba Mungu yupo, na kwamba wanapaswa kumtii, na pia kwamba tayari walishaacha kumtii (Warumi 1:20). Lakini hautuelezei ni kwa jinsi gani tutaweza kuwa kwenye uhusiano sahihi na Mungu. Unatuonesha hitaji maalumu tunalohitaji kwa ajili ya Ufunuo Maalumu kwa sababu unaonesha kwamba watu ni watenda dhambi na wasiwe na udhuru mbele ya Muumba wao.

Ufunuo wa Msingi unatuonesha kwamba utu wa binadamu umeanguka na una hatia. Ufunuo Maalumu unatoa ufafanuzi ni kwa nini utu wa binadamu umefikia kuwa katika hali hiyo. Ufunuo Maalumu ni ukweli unaodhihirishwa kwenye uvuvio wa Biblia na kwenye kuwa mfano halisi wa mwili wa Kristo. Ufunuo Maalumu unaelezea tabia ya Mungu, unafafanua anguko la mwanadamu na dhambi, na ni kwa jinsi gani tunaweza kupatanishwa tena na Mungu.

[16] Hatusemi hapa kumaanisha kwamba Mungu ni mwanadamu; Yeye ni kama mwanadamu – katika uwezo wa kufikiri, dhamira na kuzungumza – badala ya baadhi ya nguvu binafsi isiyokuwa ya kawaida.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 1

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

► Je, Ufunuo Maalumu unatueleza nini zaidi ya kile tunachokijua kutoka katika Ufunuo wa Msingi?

(1:19) Kwa kuchunguza uumbaji tunauona ukweli kuhusiana na Mungu. Hata wana falsafa wa Kiyunani walikiri kwamba ni lazima kuna aina fulani ya akili za kimungu ambazo zinauongoza ulimwengu. Sehemu muhimu sana ya uumbaji ni ile inayohusiana na asili ya mwanadamu. Tunauona ukweli kuhusiana na uwepo wa asili ya Mungu kwa kuangalia kwamba mwanadamu anao utashi wa kutambua mema na mabaya (Ona 1:32).

► Je, ni jambo gani ambalo tunaweza kulifahamu kuhusiana na Mungu tunapomwangalia mwanadamu?

(1:20) Tangu uumbaji watu wanatambua kwamba wameumbwa na kwamba Mungu anazo nguvu za kiungu na mamlaka juu yao. Huu ni ufahamu wa kutosha wa kufanya kwao kumkataa Mungu kusiwe na udhuru. Watahukumiwa kwa haki ajili ya dhambi zao. Wanajijua kwamba wana hatia kwa ajili ya uasi wao.[17] Ukweli kwamba wanajua mambo haya yote kuhusu Mungu na wao wenyewe kunawaacha bila ya kuwa na udhuru.

Haki ya Mungu inahitaji kwamba dhambi ni lazima ioneshwe kwa uwazi na kwa hiari kabla ya kuadhibiwa. Ni muhimu pia kwamba ufahamu waliokuwa nao ulikuwa unatosha kwa ajili ya wao kuweza kufanya uchaguzi ulio bora zaidi. Kama ingekuwa haiwezekani kwa wao kuchagua kufanya vinginevyo au tafauti na hapo, basi hawangeweza kukaa wasiwe na udhuru. Mungu yuko hapa akijieleza kuhusu yeye mwenyewe.[18]

Takriban kila tamaduni ulimwenguni ina dhana kwamba kuna Mungu mkuu aliyeumba ulimwengu. Kwa kawaida wanaabudu nguvu zingine zisizo za kawaida badala ya Mungu kwa sababu wanajua kwamba wametengwa na Mungu mkuu. Paulo hakujaribu kuthibitisha kuwepo kwa Mungu bali alionyesha kwamba kuwepo na mamlaka ya Mungu yanajulikana katika kila utamaduni. Ujuzi huu unasababisha kuwa na uhakika wa hatia.

Kuna mapungufu kwenye Ufunuo wa Msingi. Kumjua Kristo na injili hakutafahamika ila kwa njia ya Ufunuo Maalumu. Pia, dunia iliyoumbwa haimwoneshi Mungu kwa njia iliyo sahihi kwa sababu iko chini ya laana ya dhambi na haioneshi kabisa muundo wake wa asili. Uumbaji ni kama upakaji mzuri sana wa rangi ambao umewekewa alama ya mguu wa matope juu yake. Umeharibiwa, lakini sehemu yake ya uzuri wa asili bado imebakia, ikionyesha jambo fulani kuhusiana na mchoraji.

(1:21-22) Mungu anastahili kwamba mtu amheshimu kama Mungu (kuabudu) na kuwa na shukrani (sifa). Lakini walikataa mamlaka yake kuliko kuwa na shukrani kwa kile ambacho

---

[17] Ona maelezo ya 1:32.

[18] Kwa majadiliano zaidi kuhusiana na dhana hii, ona sehemu ya angalizo kwenye somo la 9 iliyopewa kichwa cha habari "Haki ya Mungu kwenye Mashitaka."

walikuwa wamepokea kutoka kwake. Walitaka wao wenyewe wawe miungu wakijitwalia sifa kwa yale yote waliyokuwa nayo. Kudai kuwa wao ni miungu ni upumbavu.

Mioyo yao iligeuka kuwa giza. Moyo unawakilisha mapenzi na utiifu wa mtu. Nuru inawakilisha ukweli. Kwa kuwa waliukataa ukweli, walikosa pia na uwezo wa kuuona. Walikosa ufahamu wa kiroho na wa mambo ya milele, kwa hiyo pia hawakuweza kuuelewa ulimwengu wa kimwili kwa usahihi wake.

(1:23, 25) Kujitazama wenyewe na kutazama ulimwengu wa kimwili na kumkataa Muumbaji kuliwasababisha kutengeneza miungu ambayo ilitengeneza asili ya maanguko yao wenyewe. Utukufu uliokuwa unamhusu Mungu pekee, waliuhamishia kwenye viumbe wengine Ili kuepukana na uwajibikaji wao kwa Muumbaji, waliukana uwepo wake na wakaheshimu viumbe. Mtazamo huu hasi ndio msingi wa mageuko (evolution) ya kisasa na ya ubinadamu. Kama watu walijitengeneza wenyewe, basi wanaweza wakajiwekea malengo yao, thamani zao na maadili yao wenyewe.

> "Ikiwa mzizi wa dhambi ya mwanadamu ni upotovu wa kidini, tunda lake au matokeo yake ni ufisadi wa kimaadili."
>
> - William Greathouse,
>
> *Maelezo ya Warumi*

Asili ya ibada ya sanamu ni kutumikia na kuabudu kitu ambacho Mungu amekiumba. Kutumikia kitu ni kule kukipa nafasi ya kwanza katika maisha na kupanga maisha yaende kwa kufuata kipaumbele hicho. Kuabudu kitu ni kukitegemea na kukipa heshima ambazo ni za Mungu peke yake. Ibada ya sanamu hupata utoshelevu wake kutokana vitu ambavyo Muumbaji peke yake anatoa. Hali ya sasa ya kupenda mali na vitu ni ibada ya sanamu. Mtu hawezi akaheshimu mali na vitu bila kupunguza kumheshimu.[19]

►Je, Wamataifa wanajihusishaje na kumfahamu Mungu?

(1:24) Aya hii inatoa utangulizi wa mada ambayo imepanuliwa kwenye 1:26-27. Pendo la kuabudu sanamu kwa kawaida linajielekeza kwenye uasherati, ikiwa ni pamoja na dhambi zote za ngono au kujamiana. Dhambi ya ngono au kujamiana hufanya tamaa za mwili kuwa ni kipaumbele lakini inauvunjia heshima mwili kwa sababu mwili unapaswa uwe mtakatifu na ujikabidhi kwa ajili ya utumishi wa Mungu.

(1:26-27) Uasherati ni matokeo ya asili ya kujitukuza na kuruhusu tamaa za kimwili zitawale. Wakati tamaa zinapotawala, zinakuwa zimepotoshwa. Kwa kuwa mtu hawezi kumpenda mtu mwingine yeyote kwa usahihi au kufurahia kitu chochote kwa usahihi hadi awe amempenda na kumfurahia Mungu kwa hali ya juu sana. 1:24 inatambulisha somo hili na inaonyesha muunganiko ulioko kati ya uasherati na kumkataa Mungu.

[19] Picha: "Athena Pallas austrian Parliament", ilipigwa na Jebulon mnamo Februari 20, 2012, imepatikana kutoka https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Athena_Pallas_austrian_Parliament.jpg, mali ya umma.

Dhambi zote ni upotoshaji wa kitu kizuri alichokifanya Mungu; upotovu wa ngono au kujamiana uko wazi zaidi kuliko baadhi ya dhambi zingine. Kwa jinsi mtu anavyozidi kujiondoa na kuwa mbali na njia za Mungu, hufanyika zaidi kuwa mkatili, mkorofi, na mpotovu. Baadhi ya watu hufikiri kwamba kuna tamaduni na mila zinazoishi maisha mazuri kwa kuwa hazijaingiliwa na ustarabu wa kisasa. Ukweli ni kwamba watu wengi wenye kudumisha mila hizo wanaishi katika hofu ya kifo na mambo ya mizimu; wanatenda matendo ya mila za kikatili; na wanapata mateso ya upotovu yatokanayo na mfumo wa maisha ya upotovu wa dhambi.

Mwanadamu aliumbwa ili atumike kwa ajili ya uhusiano na Mungu. Ikiwa atakuwa ametengwa na Mungu, hawezi akawa vile ambavyo ubinadamu ulikuwa umekusudiwa uwe. Huwa ni mdhaifu hata kwenye maadili yake binafsi. Maadili kuhusiana na uanamume na mwanamke hayawezekani kufikiwa kwa mtu asiye na Mungu. Katika hili upotovu wa dhambi ya zinaa ni wa kupindukia mipaka, lakini kila mtu ameathirika kwa kupotea kwa ubinadamu wa kweli kwa njia nyinginezo pia. **Kumkataa Mungu kama Mungu ni sawa na kumkataa binadamu kama binadamu. Kukataa kumwabudu Mungu ni sawa na kuukataa ubinadamu wako mwenyewe.**

Jambo lililo kinyume ni kwamba, wale wote wanaoabudu kiumbe wameishia kwenye upotovu hata dhidi ya kiumbe mwenyewe, kinyume na kile kilichokuwa cha asili. Kama watu watajiruhusu wnyewe kutawaliwa na tamaa za mwili, tamaa hizo huingia kwenye hatua ambazo si kawaida za hali ya juu sana.

Ni jambo la ajabu kwamba kama mtu atakuwa na tamaa za mwili bila kumtii Mungu ataukosesha mwili wake heshima. Sehemu za mwili ambazo watu huwa wanaziabudu kwenye dhambi ya ngono au kujamiana ni sehemu zile zile ambazo wanazitaja wanapokuwa wanataka kusemea kitu kibaya au kudhalilisha.



Dini ya kirumi

Dini ya Kirumi ilikuwa na tofauti kubwa. Waliamini katika miungu mingi. Walizingatia sana wingi wa mithiolojia ya miungu ya Wayunani, wakibadili baadhi ya majina yao. Wanapokuwa wamepata ushindi na kulitawala taifa, mara nyingi walikuwa wanakubali miungu yao iunganishwe kwenye dini yao. Waliamini kwamba baadhi ya miungu ilikuwa na umuhimu wa kipekee kwenye maeneo kadhaa ya kijiografia. Hawakuamini katika Muumbaji mmoja mwenye nguvu zote kama Mungu wa Uyahudi na Ukristo. Dini ilitumika kwenye kila nyanja ya maisha, ikiwa ni pamoja na kwenye serikali. Wakristo waliteswa na kuuawa kwa sababu walikuwa hawashiriki kwenye matukio ya hadhara za kidini.

Kwa kawaida wanawake siyo wepesi kiasi cha kufikia wanaume kwa ajili ya uasherati na upotovu. Kwa silika yao wanataka kulinda utimilifu wote wa familia. Neno "hata wanawake wao" linaonyesha kwamba uharibifu wa jamii yao kwa ajili ya uasherati ulikuwa umekamilika.

► Je, kuna aina gani za upotovu ambazo ni za kawaida katika jamii yako?

Hali ya dhambi waliyoingia inaitwa malipo. Ndivyo walivyostahiki kwa haki. Hali ya wenye dhambi ni adhabu ifaayo kwa ajili ya dhambi. Wanapata mateso na aibu inayoongezeka. Tamaa zao haziwezi kutoshelezwa. Kuna matokeo mabaya kwa sababu ya ufisadi wao.

Jibu la Kikristo kwa Dhambi ya Ushoga

Hakuna ushahidi kwamba Biblia inatambua uhalali wa kupenda "kufanya vitendo vya ushoga (au usagaji)."[20] Kama ingekuwa ndio hivyo, tungetegemea tukute mafundisho katika Maandiko yote kama ilivyofanyika kwenye kila aina ya mahusiano ya kibinadamu (mfano, waume kwa wake, wazazi na watoto, wananchi na serikali.) Badala yake, hakuna aya hata moja katika Biblia inayoonyesha uwezekano wa kuwepo kwa uhusiano wa aina hiyo ambao unakubaliwa kwenye macho ya Mungu.

Siyo majaribu, siyo hisia za upendo au mvuto kati ya wanadamu wawili, au mapambano katika roho zetu ambayo yamekatazwa kwenye Maandiko. Ukweli ni kuwa, Mungu anatuambia kwamba yuko karibu sana na wanaoumia mioyo yao, waliochanganyikiwa, na walioko kwenye majaribu. Dhambi inajitokeza wakati tunapokarisha ndani mwetu mawazo ya tamaa (Yak 1:15) au tunapojihusisha na tabia iliyo nje ya mpango wa Mungu.

Jibu linalofaa kutoka kwa kanisa kuhusiana na ushoga ni lazima lihusishe na upendo wenye huruma, ukweli wenye upole, na unyenyekevu thabiti. Kuwapenda watu wengine inamaanisha kuwajali, na kuuendeleza upendo wa Kristo hata kama watakuwa wamebadilika au hawajabadilika kutoka kwenye hali ya dhambi zao. Kuwapenda watu wengine inamaanisha ni kuwaona kwa jicho la Kristo, kama vile naye alivyotuona (na bado anatuona) katika dhambi zetu. Mara nyinyi, ni uhusiano wetu na mtu binafsi ambao awali utamwongoza mtu huyo kwenye uhusiano wa Kristo uwezao kuokoa. Kitakachofuata baadaye, ni kazi ya Roho Mtakatifu, ambayo kwa kawaida hufanya kazi ndani ya kanisa, ili kurejesha ule ukamilifu.

Na bado, kumpenda mtu pia inamaanisha kuzungumza ukweli, hata kama ukweli huo itabidi kukutana na ukatili au kutojali. Kushirikisha Neno la Mungu kunaweza kumwokoa mwanamume au mwanamke kutoka maisha yote ya maamuzi mabovu, kuchanganyikiwa, dhambi na mateso. Sio kila mtu anakubali maagizo ya Biblia. Uvumilivu na upole unapasa kuongoza mijadala yetu kuhusu ukweli wa jambo hili. Inatupasa kusikiliza kwa mioyo

[20] Sehemu hii imerejelewa kutoka kwenye makala iitwayo "What Does the Bible Say about Homosexuality: Answering Revisionist Gay Theology" from Focus on the Family. Kwa mahitaji ya Makala nzima tembelea http://media.focusonthefamily.com/fotf/pdf/channels/social-issues/what-does-the-bible-say_final3.pdf?refcd=209501

iliyowazi na kutumia Maandiko kwa upendo na upambanuzi. Tunapaswa kuonesha kwa dhati kumjali mtu, ili waweze kuthamini tunachosema.

Unyenyekevu wa kweli ni muhimu kwa ujumbe wa Kristo. Unyenyekevu hutokana na kuwa na mazungumzo na muda pamoja na Mungu; kukubali, kukiri, na kugeuka kutoka katika dhambi zetu wenyewe; na kukubaliana na upendo ulio wa kina wa Mungu kama ulivyojieleza juu ya msalaba. Ni lazima tuachie upendo na huruma viwe ndio nia yetu kuliko hofu, hasira, na chuki.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 1

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(1:28) Kwa kuwa walikataa kuwa na Mungu katika fahamu zao na katika mfumo wa maisha, akili zao na falsafa ziliharibiwa pamoja na tabia zao. Kuna msemo wa maneno kwa Wayunani unaoonesha kwamba kwa kuwa walimkataa Mungu, Mungu aliwaacha wawe katika ule ufahamu alioukataa – yaani aliachana na kuwashawishi. Mungu alimpa mwanadamu utashi wa bure na akauruhusu ufanye kazi. Baada ya hatua fulani, Mungu akaruhusu wale ambao wanamkataa yeye kuwaacha huru mbali na ushawishi wake. Hapo ndipo fahamu zao hufuata mkondo wa uharibifu usiozuiliwa na Mungu.

Taarifa kwamba Mungu aliwaacha wafuate tamaa na akili zao (1:24, 26, & 28) inaonesha kwamba watu hawa kiuhalisia walikuwa katika hali mbaya na walikuwa wamefanya kuchagua mambo ambayo haingewezekana kuyabadili tena (Linganisha na 2 Wathesalonike 2:10-12).

Akili za watu na mawazo yao vimedhurika na kuathirika kwa upotovu. Upotovu huwazuia watu wakati wa wanapotaka kufanya maamuzi ya kimaadili. Hii husababisha watu kukumbatia na kutetea tabia na vitendo vyao.

> "Ni vigumu sana kuelewa uharibifu wote kwa ukamilifu ambao dhambi inafanya kwenye hadhi ya mwanadamu. Mbali na udhaifu wa dhamira ambayo imezaa matunda na kelele za mihemuko kilichojiinua nyuma yake ni akili ambayo imefifia na kufanywa mtumwa kwenye mambo ya tamaa. Imefundishwa kutoa udhuru badala ya kutoa sababu. Inaamua kwanza, na kisha inafikiria baadaye.
>
> Inaangalia mantiki, badala ya sababu. Mara nyingine inaelezea ukweli, lakini siyo katika hali yenye udhabiti. Haiwezi ikawa inayotegemewa… inanadi ukweli kutoka kwenye uongo, inamnadi Mungu kutokea kwenye ibada za sanamu, hekima kwa ajili ya upumbavu….”
>
> - Wilbur Dayton

► Je, kuna mifano gani ya udhuru isiyo na maana ambayo watu hutumia kwa ajili ya dhambi zao?

(1:29-31) Katika aya hizi tunakutana na dhambi za kutisha. Mila na serikali vimezuia tabia hizi, lakini zipo ndani ya moyo wa dhambi wa mwanadamu. Kama vizuizi vya mila na serikali vingekuwa vimeondolewa, watu wengi ungekuta wangegeukia kwa haraka kwenye mambo ya ushenzi na ukatili.

Dhambi na maelezo ya wenye dhambi zilizoorodheshwa hapa hazina utofauti mkubwa kwa kila moja. Lakini hapa kuna baadhi ya mawazo makuu yaliyotajwa.

Udhalimu – ni neno la ujumla, ambalo pengine limebeba dhambi nyingine zote.

Uasherati – aina yeyote ya tendo la uasherati.[21]

Uovu – pia ni neno la ujumla linalohusiana na matendo mabaya na tabia mbaya.

Tamaa – Neno linalotumika zaidi katika maandiko ya Kiyunani likirejelea ubinafsi wa ukatili. Linaelezea mtu anayefuatilia mambo yake mwenyewe tu, akiwa na nia ya kutaka kuharibu mambo ya wengine. Hii inahusisha pamoja na matumizi mabaya ya nafasi ya mamlaka kwa ajili ya kujipatia faida.

Ubaya - ni hali ya kuwa mbaya, tabia ya ukatili, uovu, au mwenendo usiofaa.

Husuda – Kutamani vitu vya watu wengine, pamoja na kuwa na chuki kwa wale watu walio na vitu vinavyotamanisha.

Uuaji – kuvunja sheria, kuua mtu kwa kupanga ambayo ni matokeo ya hali ya juu sana ya hasira na chuki.

Fitina – ugomvi, pengine kutokana na ushindani.

Hadaa – ulaghai au udanganyifu, unaweza ukawa chambo cha kuponza mtu aingie kwenye mtego.

Watu wa nia mbaya – kuwa na chuki, tayari kuumiza watu wengine pasipokuwa na sababu yeyote.

Wenye kusengenya– wenye kukashifu kwa siri.

Wenye kusingizia– tabia ya kudhuru hadhi yaw engine kwa kusema mabaya au mambo maovu juu yao.

Wenye kumchukia Mungu – wanamwona Mungu kama adui kwa sababu sheria zake zinawahukumu.

Wenye jeuri –Mtu aina hii ni mwenye kiburi na ukatili. Mtu mdhaifu aliye na tabia hii hupenda kuwatusi watu wengine ambao alistahili awaheshimu. Mtu aliye katika nguvu kubwa ya tabia hii ni mkatili kwa watu wengine na huchukua malipizi ya kupitilza kwa wale wanaoshindwa kuonyesha kwake ile heshima anayoitaka.

Kutakabari – Kiburi ni mtazamo wa mtu kujiinua mwenyewe. Ni shina la maovu yote kwa sababu humshawishi mtu kutawala maisha yake mwenyewe kinyume cha Muumba wake.

[21] Maandiko mengi ya Kiyunani hayana neno hili katika orodha hii.

Wenye majivuno – Tabia ya kujiinua au kujikweza. Watu hawa ni wabinafsi. Kama ataonekana hapa kwamba anazo sifa nyingine, hujikuza kwa kujidanganya, kwa gharama ya watu wengine, na kuwaumiza wengine.

Wenye kutunga mabaya – Ni wabunifu kwenye mwendelezo wao wa uovu na mambo ya kuumiza

Wasiowatii wazazi wao – Uharibifu wa familia ni matokeo ya dhambi na unaelekeza kwenye kutengana zaidi kwa jamii. Tabia hii ya dhambi hujidhihirisha mapema kwa mtoto ambaye huasi kwa mamlaka yake ya mwanzo anayoijua.

Wasio na ufahamu – Wasio na ufahamu wa thamani ya maadili. Mtu huyu hashawishiki kwa sababu ambazo zimeendana na maadili. Hali hii siyo kukosa werevu, lakini ni ulemavu wa hisia ya kimaadili ambayo ni matokeo ya moyo wa uovu.

Wenye kuvunja maagano – Kukosa uaminifu. Kuachana na maadili na mamlaka, kuuchukia ukweli halisi ambao haufai kwao, na kufanya umimi au ubinafsi kuwa kipaumbele chao, huku wakiwa wanavunja ahadi zao.

Wasiopenda jamaa zao – Kinyume cha kuwa na kinga na silika ya upendo. Wanaweza wakaachana na familia zao na kufuata tamaa zao wenyewe. Silika za msingi za upendo zinaweza zikavurugwa. Wanaweza wakawanyanyapaa watu ambao ni tegemezi kwa ajili ya ulinzi wao.

Wasiotaka suluhu – Hawataki radhi.[22]

Wasio na rehema – Bila huruma. Wanaweza wakaangalia mateso bila ya kuwa na huruma. Hawabadilishwi kutoka katika njia ya uovu kwa kuona mateso wanayopitia watu wengine

(1:32) Wanajua kabisa kwamba mambo haya ni mabaya. Wapagani au makafiri hawafuati kwa uaminifu hata ule ukweli ambao wanao. Wanajua kwamba wako chini ya hukumu. Siyo tu kwamba wanaifuata dhambi bali wanaidhinisha dhambi kwa watu wengine. Hamasa ya jamii hushuka kwa kiwango cha chini sana kiasi kwamba kiwango kingine cha mwenedo wa tabia hukubaliana na kuidhinisha uasherati.

Mtu ambaye anakubaliana na dhambi kabisa anajithibitisha mwnyewe kama mtenda dhambi na anawathibitisha wengine kama wenye dhambi. Anaweza akavutiwa na dhambi za watu wengine. Watu walipiga makofi kwa kushangilia mauaji kwenye viwanja vya Rumi. Watu wengi katika nyakati hizi wanafurahia kuangalia vurugu na vitendo vya ngono vya uasherati. Wanafurahia kuona watu wanaoendelea kushamiri kwenye viwango vikubwa vya dhambi wanazoweza kufanya.

[22] Maandiko mengi ya Kiyunani hayana neno hili katika orodha hii.

Je, kila asiyeokoka yuko hivyo?

Siyo kila mtu ameweza kufanya kwa ukamilifu dhambi hizi zote. Hata hivyo, ubinadamu uliodidimia umekuwa na tabia ya mwelekeo wa kufanya dhambi hizi zote, na inawezekana kila mtu akawa ametenda mojawapo ya dhambi hizi katika hali tofauti.

Seneca alikuwa mwanafalsafa wa Kirumi na afisa wa serikali ambaye aliishi wakati wa Paulo. Hakuwa Mkristo na alikuwa hana ufahamu na Biblia, lakini alifanya utafiti na akaona kwamba nguvu ya kila dhambi iko ndani ya kila mtu. Alisema, "Maovu yote yako ndani ya watu wote, ingawaje maovu yote kwa nje hayawezi kujulikana kwa kila mtu."[23] Tunaweza tukaona kwamba ufafanuzi wa Paulo kuhusu asiyeokoka unatumika wakati wote na kwenye kila mila.

Serikali na taratibu za kijamii vinazuia tabia ya vitendo vingi vya uovu vya watu binafsi. Watu wengi huijaza mioyo yao na fahamu zao tamaa za dhambi ambazo hazijionyeshi kwa wazi kwa sababu wanataka kukubaliwa na watu wengine. Watu wana tabia za siri za dhambi zilizoorodheshwa katika kifungu hiki na wana hatia ya dhambi hizi katika mioyo yao.

Matumizi ya Kifungu

Kifungu hiki kimsingi ni ufafanuzi wa watu katika jamii ambao hawajawahi kuisikia injili. Walikataa kumjua Mungu ambaye umefunuliwa kwenye uumbaji na katika dhamira zao. Kisha, wakapata kitu kingine cha cha kuabudu ambacho kiliwawezesha kujihusisha na mambo ya tamaa ya mwili; na tamaa zao zikageuka kuwa upotofu. Kifungu hiki kinaelezea ni kwa nini watu hao wanahitaji injili.

Kifungu hiki ni muhimu kwa kila mtu, kwa sababu kinaorodhesha aina nyingi za matendo ya dhambi na kinaonesha kwamba dhambi hizi zinachukiwa na Mungu. Ni onyo pia kwamba dhambi zote zina tabia ya kumpeleka mtu mwenye dhambi mbali zaidi kwenye uovu zaidi. Watu wanaoisikia injili na kuikataa wako kwenye hatari ya kuingia kwenye mchakato unaofanana wa kupoteza ufahamu wa lililo jema na baya.

Kifungu hiki kinaelezea hali tunazoziona katika jamii zetu wenyewe, ingawaje injili imeshahubiriwa huko. Mila hupata nafasi ya kufanya baadhi ya dhambi zikubalike, ikiwa ni kupuuzia kipimo cha Mungu

Ushuhuda

Shmagi alizaliwa katika nchi ya Georgia, katika ulaya mashariki. Wazazi wake walikuwa hawaamini kuwa Mungu yupo, na hakuwahi kuhudhuria kanisani akiwa mtoto. Maana ya jina lake ni "mwepesi wa hasira," na jina lake linaendana na tabia yake. Mara nyingi alijikuta katika matata akiwa kijana. Baada ya kupatikana kuwa ana hatia, alifungwa Uhurusi miaka miwili. Baadaye alifunguliwa na kurudi Georgia wakati wa Georgia ilipojitenga na Urusi.

---

[23] Imenukuliwa na F.F. Bruce, *The Epistle to the Romans*, in *Tyndale Bible Commentaries* (Grand Rapids: William B. Eerdmans Pub. Co., 1963), 87

Ini la Shmagi lilikuwa limeharibika vibaya kutokana na ulevi, daktari alimwambia kwamba asingeishi muda mrefu. Shmagi akawa hana furaha na akaanza kujisikia na kutafuta kumfahamu Mungu. Akawauliza marafiki wakristo kama wangeweza kumpeleka kanisani. Kwa mara ya kwanza, wakamwambia kanisani sio mahali panapomfaa. Ndipo wakamwambia hata hivyo angeweza kwenda, kama atawaahidi kuwa hatakuwa mtu anatafuta kubishana. Alienda na akaokoka akiwa na umri wa miaka 22. Maisha yake yalibadilishwa kabisa.

Shmagi akaponjwa ugonjwa wake wa ini. Hakuwa ametarajia kuoa kwa sababu ya ugonjwa wake, lakini Mungu kampa hatima mpya. Sasa ana mke na watoto mabinti watatu. Shmagi ni mchungaji na ana huduma ya kufundisha.

Maswali ya Mapitio Somo la 2

(1) Je, ni kwa njia gani watu hupokea ufunuo wa Msingi?

(2) Je, watu wote wanajuaje kuhusu Mungu hata bila Maandiko?

(3) Je, Ufunuo maalumu ni nini?

(4) Je, kuabudu sanamu ni nini?

(5) Taja njia mbili ambazo zinaleta madhara ya upotovu wa fikira kwa watu

Kazi ya kufanya Somo la 2

Andika ukurasa mmoja kuelezea hali ya jamii ambayo haijawahi kusikia injili lakini imemkataa Mungu. Wana ufahamu gani wa Mungu? Imetokea nini kwenye kufikiri kwao? Elezea uovu wao. Fafanua ni kwa nini siyo kila mmoja anaonesha aina moja ya kufanana ya uovu.

Somo la 3
Kosa la Waisraeli

Utangulizi wa Maandiko yahusuyo siku za mwisho (Apocalyptic)

Maandiko yanayohusu siku za mwisho yanahusu kutunza imani badala ya kulemewa na uovu na kutotenda haki katika dunia wakati wa siku za mwisho. Yanaelezea muda ambao Mungu kwa ghafla ataingilia kati duniani, akiadhibu uovu na akiwasaidia watu wake.[24]

Neno ambalo mara kwa mara linatumika kwa ajili ya muda wa mwisho wa Mungu kuingilia kati ni *Siku ya Bwana*. Baadhi ya vifungu kwenye Agano la Kale huelezea siku ya Bwana kama ni ule muda ambao Wamataifa wataadhibiwa kwa yale waliyokuwa wameifanyia Israeli.[25] Wayahudi wengi walianza kudhania kwamba Wayahudi hawakuwa na haja ya kuhofia chochote kuhusiana na hukumu ya Mungu. Manabii walijitahidi kuwaonesha kwamba hata wao watapaswa kuhukumiwa kama watakuwa watenda dhambi. (Zefania 1:12, Amosi 5:18-27) na kwamba hawataepuka kwa sababu wao ni Wayahudi; lakini dhana hii iliendelea kubaki.

Ilikuwa ni vigumu kwa Wayahudi kukubali ukweli kwamba walihitaji kuokoka. Kwa mfano, ubatizo ulikuwa ni sherehe waliyoitumia kuwaingiza Wamataifa kwenye Uyahudi. Hawakuwabatiza Wayahudi. Yohane Mbatizaji aliwabatiza Wayahudi, na kitendo chake hicho kiliwaghadhibisha Wayahudi ambao walifikiri kwamba hawakuwa wanahitaji ubatizo au msamaha. Walidhania kwamba walikuwa wamependelewa na Mungu kwa sababu walikuwa ni uzao au watoto wa Ibrahimu (Mathayo 3:9).

Kwenye kitabu cha Warumi, Paulo anarejelea kwenye maneno haya ya "siku ile ya hasira" (2:5) na "katika siku ile Mungu atakapozihukumu" (2:16). Marejeo haya yanatokana na mada iliyoko katika 1:16-18, kwamba injili huleta wokovu unaotuepusha na siku ile ya hasira. Katika 2:2-3 anawashangaza Wayahudi wanaojihesabia haki ambapo ukweli ni kwamba walikuwa pia na sababu ya kuwa na hofu na siku ile ya Bwana. Kwani hata Wayahudi wanahitaji wokovu.

Kifungu cha kujifunza – Warumi sehemu ya 2, kifungu cha 2

Katika somo hili, tutaendelea kujifunza sehemu ya 2 ya kitabu hiki cha Warumi. Katika somo lililotangulia, tulisoma kifungu kinachoelezea kuhusu kosa la Wamataifa. Kifungu hiki cha (2:1-29) kinaelezea kosa la Waisraeli.

Sehemu ya 2 ni 1:18-3:20. Jambo kuu katika sehemu hii ya 2 ni kwamba kila mtu katika dunia hii amekiuka mapenzi ya Mungu na yuko chini ya hukumu. Hakuna mtu anayeweza

[24] Maandiko ya siku za mwisho katika Agano la Kale ni pamoja na kitabu cha Danieli, Zekaria, Yoeli, Ezekieli 37-39, na Isaya 24-27. Kwenye Agano Jipya, tunapata kitabu cha Mathayo 24, Luka 21, Marko 13, 2 Wathesalonike 2, na Ufunuo.
[25] Baadhi ya mifano ni Zekaria 12 na Yoeli 3.

kuokoka kwa kufuata yale anayoyataka Mungu kwa sababu kila mtu tayari ameshayakiuka matakwa hayo.

Kwanza Paulo anatoa ufafanuzi kwamba Wamataifa wamekataa kuwa na ufahamu wa Mungu na wakageukia kwenye sanamu na tamaa za dhambi. Kisha, anaelezea hali ya Waisraeli, amabao walikuwa na sheria ya Mungu lakini hawakuifuata au hawakuitii. Sasa tutajifunza kifungu kinachohusiana na Waisraeli.

Hapa Paulo anabadilika kutoka katika nafsi ya tatu (wao) na kugeukia katika nafsi ya pili (wewe). Anazungumza na mtu yeyote aliyefikiria kwamba injili haikuwahusu kwa sababu tayari walikuwa wamefikia katik kutimiza viwango vya kuwa wenye haki. Wayahudi wengi walikuwa katika kundi hilo, na sehemu hii inazungumza kwa ajili yao (2:17); lakini Wamataifa walio na maadili ya viwango vya juu wanaweza pia wakawa kwenye kosa linalofanana. Anaonyesha kwamba mtu anayejifikiria kwamba ni mwenye haki bila ya neema ni mnafiki na mwenye hatia.

Jambo Kuu katika sura ya 2

Wayahudi wana hatia ya dhambi zinazofanana na wanazofanya Wamataifa na kwa sababu hiyo watahukumiwa vilevile na Mungu.

Muhtasari wa sura ya 2

2:1, 11 ndizo zinazofanya jambo kuu. 2:1 inaelezea kwamba Wayahudi wote kwa pamoja wana hatia inayofanana; 2:11 inaelezea kwamba Mungu hana upendeleo. Sehemu nyingine inayoendelea katika sura hii inajenga hoja inayotokana na taarifa zilizoko katika aya hizo. Yaliyopo hapo hayana kisingizio au udhuru, kama vile ambavyo wapagani au makafiri hawana pia cha kusingizia au udhuru (1:20).

2:13, 17 inaonyesha ni kwa nini Wayahudi wana tegemeo la kupewa upendeleo – kwa sababu walipokea Ufunuo wa Mungu na walikuwa na dini inayozingatia mafunuo hayo. Kwenye Warumi 1, Paulo alieleza ukweli kwamba Wamataifa wanastahili hukumu. Kila Myahudi angekubaliana na hili. Kisha kwenye 2:1, Paulo anawaogofya Wayahudi kwa kuonesha hatia yao. Wao pia walivunja sheria na wanastahili hukumu ile ile kama Wamataifa!. Walitegemea kwamba wangesamehewa kwa sababu walikuwa Wayahudi ambao waliifahamu sheria ya Mungu na walikuwa na dini iliyo sahihi.

Mamilioni ya watu leo wako katika kundi hili. Wanafikiri kwamba wanakubalika na Mungu kwa sababu wanaamini katika Mungu na wanatekeleza taratibu na mifumo ya dini wakati huku wakiendelea kutenda dhambi.

► Je kuna watu wengi katika jamii yako ambao kimakosa wanajifikiria kwamba wao ni Wakristo? Ni kwa nini wanafikiria hivyo?

► Mwanafunzi atapaswa asome Warumi 2:1-29 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(2:1) Kwamba wayahudi hawakuwa na "kisingizio au udhuru" inalingana na hali ya Wamataifa ambao walikuwa hawana kisingizio au udhuru (1:20). Wazo hilo lingeleta mshtuko kwa Myahudi anayejihesabia mwenye haki, kama ambavyo ingekuwa kwa binadamu wa sasa anayejidhania kwamba yeye ni mzuri wa kutosha.[26]

Kwa kuwahukumu wengine, walijihukumu wenyewe pia, kwa sababu walikuwa wana hatia katika dhambi zile zile zinazofanana. Wajibu wao uliongezeka kwa kuwa walikuwa na Ufahamu wa ukweli. Yesu alisema kwamba miji mingine ya Israeli itahukumiwa vibaya kuliko hata ilivyokuwa kwa Sodoma na Gomora (Mathayo 11:21-24).

Aya hii inarejelea kwa mtu anayefikiria kwamba anaweza akawahukmu wengine na kisha akajihesabia yeye kwamba ni mwenye haki. Sehemu nyingine ya sura iliyobakia inamweka Mungu kwenye jukumu la kuwa jaji na inaonesha ni kwa jinsi gani hukumu yake ni tofauti na ya wale wanaohukumu katika njia ya kujipendelea wenyewe.

(2:2-3) Hukumu ya Mungu iko katika viwango vya uhakika. Mungu hatoi hukumu yake kwa kutumia viwango vinavyobadilika na visivyo sahihi vya kibinadamu.

(2:4) Mungu ametoa mwangalizo maalumu kwa Wayahudi, kwa hiyo walifikiria kwamba atapinda haki kwa ajili ya kuwapendelea. Ni kweli, wema wake kwao ulikuwa ni wa kuwaongoza kwenye toba, na siyo kuiondoa haki. Kwahiyo watu wengi "hudharau" wema wa Mungu kwa kuona kwamba ni sawa na suala la kawaida tu la ukarimu na uvumilivu. Kile ambacho mtu wa dunia anataka kutoka kwa Mungu ni mafaniko ya mali pamoja na kumvumilia wakati anaendelea kutenda dhambi. Kuuona wema wa Mungu katika njia hii ni kudharau wema wake. Wale ambao wamesikia habari za Mungu wana hatia zaidi kwa sababu wema wake Mungu uliwapa nafasi ya kutubu.



Nero

Nero alikuwa mfalme kwenye mwaka wa 54-68 B.K. Alikuwa madarakani wakati Paulo alipokwenda Rumi. Alikuwa mkatili sana wa kupitiliza na aliwachukia Wayahudi na Wakristo.Wanahistoria wa mwanzo waliandika kwamba wakati mwingine Nero alikuwa akiwateketeza Wakristo kwa kuwaungza kwa moto kwa ajili ya kuwa nuru katika viwanja vyake.

[26] Picha: "Nero", imepakiwa na David Jones mnamo Desemba 24, 2011, imepatikana kutoka https://flickr.com/photos/cloudsoup/6564103675/, imepewa leseni chini ya CC BY 2.0, imeshushwa rangi na kukatwa kutoka kwenye asili.".

(2:5) Kuchelewa kwa muda wakati wanapoendelea kutenda dhambi badala ya kutubu kulikuwa kunalimbikiza ghadhabu. Kwa kuwa walikuwa wanajua ukweli, wanakuwa watu wa kuwajibika zaidi, na, kwa hiyo, ghadhabu ya Mungu iliongezeka dhidi ya kutokutii kwao.

(sehemu inayofuata ni muhimu sana kwa ajili ya kuelewa sehemu iliyobakia ya sura hii.)

Hukumu ya Matendo

► Tunapokuja kwenye eneo la hukumu, je, mambo tuliyotenda duniani yatakuwa muhimu?

Hukumu ya mwisho itakuwa ni kutathimini matendo. Mungu ataadhibu na kuwazawadia watu kutokana na matendo yao waliyofanya. Kutakuwepo na madaraja ya adhabu na thawabu kwa ajili ya watu wa aina mbalimbali (Waebrania 2:2, Waebrania 10:28-29, Mathayo 10:42, Luka 12:47-48, 2 Wakorintho 5:10).

Wazo kwamba wenye dhambi wanahukumiwa tu kwa ajili ya kutoamini sio la kimaandiko. Katika Ufunuo 20:12, watu wanahukumiwa kutokana na kumbukumbu za matendo yao. Katika 2 Wakorintho 5:10 panasema watu wote, ikiwa ni pamoja na watu waliookoka, watahukumiwa kwa matendo yao. 1Wakorintho 3:12-15 inaonyesha kwamba Wakristo watapokea thawabu tofauti tofauti kulingana na nia, bidii, na ubora ("dhahabu, fedha, mawe ya thamani, miti, majani, manyasi"), wa matendo yao. Wakristo wote watapata thawabu kwa sababu Wakristo wote wa kweli wanafanya matendo mazuri, lakini siyo matendo yao yote yatakayokuwa na usawa unaofanana. Matendo ya watu walioamini ambayo hayatapita kwenye jaribio la viwango vya ubora yatateketezwa kwa moto.

Kwenye Warumi 2 inaonesha kwamba baadhi ya watu ambao hawajawahi kusikia injili ya Agano Jipya hawatahukumiwa kwa ajili ya matendo yao. (ona 2:7, 10, 13, 26-27). Hiyo haimaanishi kwamba kuna watu ambao hawajawahi kutenda dhambi na kwahiyo wanaweza wakakubalika kwa matendo yao bila ya neema; kwa kuwa kwenye 3:19-20 panasema kwamba watu wote wametenda dhambi. Watu ambao matendo yao yanakubalika ni wale ambao wamejionea neema inayoitwa kutahiriwa moyo. Matendo yao yamethibitishwa na Mungu (2:29).

Hii neema ya upasuaji kwenye moyo ilikuwa imeahidiwa kwenye nyakati za Agano la Kale:

> Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai (Kumbukumbu la Torati 30:6).

Kwa hiyo, tunatambua kwamba Wayahudi waliokolewa kwa neema, na siyo kwa matendo yao.

Neema hii ilipatikana pia kwa Wamataifa, aidha wawe au wasiwe wamepokea Ufunuo Maalumu.

> Petro akafumbua kinywa chake, akasema, "Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye" (Matendo 10:34-35).

Matendo ya haki hufuatana na mabadiliko ya moyo, kukiwa na uthibitisho wa utii kwa Mungu. Ushahidi huu ndio msingi wa kuhesabiwa haki ya mwisho uliozungumzwa katika Warumi 2:13, 16, kuhesabiwa haki kwenye hukumu ya mwisho.

Kifungu hiki hakifundishi kwamba mtu ataweza kuokolewa kwa matendo yake, bali utii wa kweli ndio unaohitajika, na siyo tu ujuzi wa sheria. Jambo hli linaungwa mkono nakifungu hiki: kwamba Wayahudi pia wanahitaji wokovu kwa sababu hawakutii.

Kifungu cha kujifunza– Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 2

Mwendelezo wa maelezo ya Aya–kwa-Aya

(2:7) Mungu hutoa uzima wa milele kwa wale wote wanaotafuta kupata heshima itokanayo na Mungu kwa kuishi katika matendo yanayompendeza Mungu.

(2:9) Hapa fursa ya myahudi inaleta uwajibikaji mkubwa. Kwa kuwa injili ilikuja kwake kwanza, anastahili kupata hukumu ya kwanza.

(2:11) Hii ndio aya ya msingi ya sura hii. Wale wote wanaoishi kwa kumwasi Mungu watahukumiwa, bila ya upendeleo kwa sababu wamekuwa ni watu wa dini.

Mtazamo kutoka kwa Yakobo

Yakobo anasema kwamba mwanadamu hahesabiwi haki kwa imani tu, lakini pia kwa matendo yake (Yakobo 2:24). Lakini Paulo anasema katika Waefeso 2:8 kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria. Katika Warumi 3:28 anasema kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani mbali na matendo ya sheria.

Kwahiyo, je, tunahesabiwa haki kwa matendo na imani kwa wakati moja, au tunahesabiwa haki kwa imani tu? Je, Paulo na Yakobo wanajichanganya wenyewe? Ukweli ni kwamba hawakuwa wanazungumzia kuhusu jambo linalofanana.

Paulo anaelezea jinsi mtu anavyohesabiwa haki mbele ya Mungu. **Mtu anakuwa mwenye haki kwa neema kwa njia ya imani.**

Yakobo anaelezea jinsi mtu anavyohesabiwa haki mbele ya watu wengine. **Mtu huonesha kuwa anayo imaini iokoayo kwa kuishi kwa uaminifu**.

Jambo kuu katika Waraka wa Yakobo ni kuthibitisha kwamba imani ya kweli inatumiwa katika maisha ya kila siku. Anasema kwamba Ibrahimu alikuwa "amehesabiwa haki," kwa matendo yake. Mtu anaonyeshwa kuwa mwenye haki kwa imani na matendo kwa pamoja. Tunatambua kwamba mtu ni Mkristo kama anakiri kuwa hivyo na pia kama anaishi maisha yanayofanana na Mkristo.

Paulo anatoa uthibitisho kwamba matendo mema hufuata baada ya imani. Katika Waefeso 2:10, baada tu ya tamko lake kwamba tunaokolewa kwa njia ya imani, Paulo alisema kwamba "tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema."

Yakobo na Paulo hawajichanganyi. Wote wanakubaliana kwamba imani iokoayo humfanya mtu akubalike kwa Mungu, na kwamba matendo hufuata baada ya mabadiliko na kudhihirisha kwamba mtu huyo ameokoka.

Kifungu cha kujifunza– Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 2

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(2:12) Sheria iliyoandikwa haiwezi ikawa ndio kipimo cha hukumu kwa wale ambao hawajawahi kabisa kuisikia. Watahukumiwa kwa sheria ile ambayo Mungu alikuwa ameidhihirsha kwao kwa njia nyingine (Ona 1:20 & 2:15).

(2:13) "Watakao hesabiwa haki" inalenga kwenye hukumu ya mwisho. Baadhi ya watu wanategemea kuhesabiwa haki kwa sababu wameishika sheria. Lakini ufahamu wa sheria bila utiifu haukubaliki.

(2:14) wafanyapo kwa tabia zao yaliyo ndani ya torati Ukweli ni kwamba wanaweza kufanya jambo la haki "kwa tabia zao" haimaanishi kwamba kwa asili ni wazuri bila Mungu. 2:15 inaonesha kwamba ni kwa sababu ya sheria ambayo Mungu ameandika ndani ya mioyo yao na dhamiri zao kwamba wanaweza kufanya jambo lililo jema. "kwa tabia zao" inamaanisha kwamba wanafanya kwa kile Mungu anachowafunulia kwenye asili yao bila ya Maandiko yaliyoandikwa.

(2:15) Wale ambao hawana sheria iliyoandikwa bado wanayo sheria iliyo ya maadili iliyoko dani yao na wanaweza wakafanya maamuzi yao maalumu. Hiyo haina maana kwamba dhamiri ni ya kutegemea kabisa. Dhamiri haiko sahihi kwenye kila jambo kwa kina, ikiwa inashawishiwa na mazingira na elimu; lakini ni mwongozo kwa kile kitu ambacho ni sahihi kwa ujumla. Hata hivyo, watu wote ni watenda dhambi, hata katika kipimo hicho, kwa sababu siku zote hawajaweza kufanya kile ambacho walijua kwamba ni sahihi.

2:15, 16 inaonyesha kwamba hukumu haitakuwa tu ni kwa ajili ya matendo ya nje, bali kimsingi hata nia ya kutenda jambo. (mistari hii inazungumzia mioyo, mawazo, dhamiri, na siri.)

(2:16) Kuhesabiwa haki kunakojadiliwa katika kifungu hiki (Imetajwa kwenye 2:13) siyo mbadala wa kuhesabiwa haki kwa njia ya imani. Ni udhihirisho wa mwisho, wa kuhesabiwa haki katika hukumu ya mwisho.

Kanuni hizi za hukumu ni za msingi kutokana na injili aliyoihubiri Paulo. Habari njema za injili kuhusiana na msamaha siyo muhimu kama hakuna uelewa wa hukumu ya Mungu itakayokuja dhidi ya wale ambao hawana msamaha. Kosa lolote ambalo linadhoofisha mtazamo sahihi wa haki ya Mungu litapotosha pia injili.

Tumaini kwa Wapagani au Makafiri ambao hawajafikiwa.

► Je, ni nini kitakachotokea kwa wapagani au makafiri ambao hawajawahi kuisikia injili? Ni kwa jinsi gani wanaweza kustahili hukumu kwa ajili ya dhambi kama hawajui vizuri?

Kwenye Warumi 2:14-16 panaonesha kwamba kuna baadhi ya watu ambao huchagua kutenda mambo ya haki, na, kwahiyo, hawatahukumiwa. Hata hivyo, tunajua kwamba hakuna mtu atakayeokoka kwa matendo yake. Kila mtu ameivunja sheria na anastahili hukumu. (3:9-10, 19-20). Hakuna mtu anayeweza kuokoka kwa sifa njema za matendo yake. Kwa hiyo, mtu ambaye hajawahi kusikia injili akiokoka, itakuwa ni kwa neema kupitia upatinisho, kama atakuwa hajaisikia injili.

Kama mtu anamcha Mungu, Mungu atamonesha njia ya kumleta kwenye uhusiano naye. Zaburi 25:14 inasema "Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha agano lake." Agano la Mungu linatuonesha kitu kinachohitajiwa katika ushirika naye. Uhusiano na Mungu huhitaji neema kwa sababu watu wote wametenda dhambi.

Kulikuwa na watu kama akina Ayubu, Balaamu, na Nuhu ambao walimjua Mungu ingawaje hawakuwa na Maandiko. Kulikuwepo na Melkizedeki, aliyekuwa kuhani wa Mungu, ingawaje alikuwa hana uhusiano na kile ambacho Mungu baadaye alifanya kwa Israeli. Mungu anaweza akajidhihirisha mwenyewe kwenye utamaduni wa aina yeyote na kwa wakati wowote. (Ona pia Zaburi 19:1-4, Warumi 10:18). Waabudu sanamu katika Warumi 1 hawakuwa katika hali ya kukengeuka kwa sababu kamwe walikuwa hawajawahi kumjua Mungu, lakini kwa sababu walikuwa wamekataa kile walichokuwa wanakijua.

Je, inawezekana mpagani au kafiri akaokoka bila ya kuisikia injili? Kama mtu atafuata ukweli anaoujua, Mungu atamwongoza katika kuelewa zaidi jinsi ya kutafuta na kupata msamaha. Hiyo ndiyo wokovu kwa njia ya neema na siyo kwa matendo. Hii ni tofauti ya ulinganifu wa wokovu kwa njia ya matendo ambao ndio unaoelezwa na dini nyingi.

Hivyo, kama mtu anaweza akaokoka bila ya kusikia injili, kwa nini jambo muhimu kwetu kueneza injili? Swali hili litajibiwa zaidi mbeleni.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 2

Mwendelezo wa maelezo ya Aya–kwa-Aya

(2:17-20) Wayahudi walikuwa wanafiki kwa sababu walikuwa wanafundisha sheria huku wakiivunja wao wnyewe. Walifurahia jukumu lao la kuwa ni watu waliomiliki sheria, watu wanaotambua haki, na waalimu wa wajinga. Kuna maelezo ya kejeli hapa wakati Paulo anapoorodhesha madai yao makubwa.

Biblia inaweza ikawa kitabu kinachouzika hata katika jamii ambayo inaenda kuwa siyo ya kumcha Mungu. Inaonesha kwamba watu wanaona thamani kuwa na sheria za Mungu hata kama hawawezii kuzitii.

Mara nyingi watu wanashikilia namna za kidini kama kisingizio cha kufunika dhambi baada ya kupoteza ukweli wa kiroho kwenye uhusiano wao na Mungu.

(2:21-24) Wayahudi walifurahia kuwahukumu Wamataifa kwa kutumia sheria, lakni wao wenyewe walikuwa hawaitii kwa ukamilifu. Walimvunjia Mungu heshima kwa kujisifu juu ya wema wao huku wakiishi maisha ya dhambi. Vivyo hivyo, kipingamizi kikubwa kwenye Ukristo ni kwamba Wakristo sio mfano mzuri wa kuigwa katika yale mambo wanayojinadi nayo kwamba wanaamini.

(2:25) Hawakuweza kudai kuwa wenye haki mbele za Mungu kwa msingi wa kutahiriwa isipokuwa kama wangeishika sheria yote. Kama walivunja sheria, walikuwa sawa tu na watu ambao walikuwa hawajatahiriwa.

Msamiati wa Kutahiriwa

► Je, kutahiriwa kulikuwa kunaashiria nini?

Kwa fikira ya Wayahudi kulikuwa na aina mbili za watu duniani: wale wenye sifa ya kukaa kwenye agano na Mungu na wale ambao hawakuwa na haki hiyo. Kutahiriwa kulikuwa ni kama ishara ya Agano kati Israeli na Mungu, lakini hatimaye ikaja kuwakilisha msururu mzima wa mahitaji yote kwa ajili ya agano. Kwa hiyo, Wayahudi wakaita hizi aina mbili za watu wa dunia kwamba ni *waliotahiriwa* na *wasiotahiriwa*. Ili uweze kutahiriwa, kwa mujibu wa malezo ya Paulo, kwa kawaida ina maana ya kufuata mfumo mzima wa Uyahudi kama njia ya kuwa kwenye Agano. (Ona Wagalatia 5:2-3 kama mfano wa matumizi ya maelezo hayo). Kutahiriwa katika maana hiyo ya ufahamu ilkuwa ni jaribio la kuokolewa kwa njia matendo kuliko kwa njia ya neema.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 2

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(2:26) Kama mtu asiyetahiriwa akitimiza makusudi ya kweli ya sheria, Mungu hatamhukumu kwa kutotahiriwa.

(2:27) Ulinganifu kati ya Mmataifa mwenye haki na Myahudi mtenda dhambi unaonesha kwamba Myahudi ni mwenye hatia, ingawaje anayo asili ya Uyahudi. Kwa ufahamu unaofanana, Nuhu aliihukumu dunia kwa hali yake ya kuwa mwenye haki kwa sababu alionesha utii wa kweli ni nini (Waebrania 11:7).

(2:28-29) Kutahiriwa kulikuwa ni alama ya utambulisho kwa Myahudi, kwamba alikuwa ni mmoja wa watu wa Mungu. Kwa Mkristo (Katika Kumbukumbu la Torati 30:6 na katika maeneo kadhaa ya Agano Jipya) inaashiria kazi ya Roho Mtakatifu wakati anapobadilisha moyo wa mwenye dhambi kwa kumpenda na kumtii Mungu.[27] Huu ni umuhiku wa tohara kwa mkristo

[27] Kumbukumbu la Torati 30:6, Wafilipi 3:3, Wakolosai 2:11-12

► Mwanafunzi atapaswa asome Kumbukumbu la Torati 30:6 kwa ajili ya kikundi.

Mungu aliwaahidi Waisraeli wa mwanzo kwamba atafanya kazi ya neema ndani ya mioyo yao. Hii haikuwa ni kwa ajili ya uzao wao tu, lakini ni kwa ajili ya watu wote waliousikia ujumbe kwa wakati ule.

Mtu anayezungumziwa katika sura hii ambaye anafanya matendo mema bila ya kujua Maandiko ni mtu ambaye ameipokea neema kwa njia ya imani, kwa kuiamini kweli aliyo nayo.

Mtazamo kutoka kwa Isaya

Mungu siku zote anantaka utii kutoka ndani ya moyo, kuliko urasmi na ushikiliaji mno wa sheria, na anatoa neema kwa Wamataifa wote. Kumbuka mistari hii kutoka Isaya 56:6-7.

> Na wageni, walioandamana na Bwana ili wamhudumu, na kulipenda jina la Bwana, kuwa watumishi wake; kila aishikaye sabato asiivunje, na kulishika sana agano langu; Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala; makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu; kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote.

Maswali ya Mapitio Somo la 3

(1) Je, Maandiko yanayohusu siku za mwisho yanaelezaje?

(2) Je, kwa nini Wayahudi walitarajia kupata Upendeleo?

(3) Je, mtu anahesabiwaje haki?

(4) Je, mtu huoneshaje kwamba anayo imani iokoayo?

(5) Je, tohara ina umuhimu gani kwa Myahudi, na ina mfano gani kwa Mkristo?

Kazi ya kufanya Somo la 3

Andika ukurasa mmoja kuelezea kuhusu kutokuelewa kwa Wayahudi ambao kwa makosa hufikiri kwamba wanapaswa wakubaliwe na Mungu. Elezea watu wengine ambao wana kutokuelewa kama hawa Wayahudi leo.

Somo la 4
Hali ya Ulimwengu Wote

Neema iletayo Wokovu

Hata kama itatolewa dhabihu, mwenye dhambi hawezi kuwa na matumaini bila ya neema ya Mungu kuwa inafanya kazi ndani ya moyo wake. Mwenye dhambi huwa amekufa kiroho katika dhambi yake, akiwa anatawaliwa na tamaa mbaya, na akiwa chini ya utawala wa shetani. (Wafeso 2:1-3). Hana uwezo wowote wa kubadilisha mwenendo wake (Warumi 7:18-19). Je, ni kwa jinsi gani anaweza kukubaliana na injili kwa toba na imani?

Wanateolojia wamejaribu kuelezea jinsi neema ya Mungu inavyotenda kazi kwenye hali ya uenye dhambi ya mwanadamu.

John Calvin aliamini kwamba kwa sababu mwanadamu amepotoka au amekengeuka kabisa hawezi akawa na chaguo la kuwajibika kwa Mungu.[28] Kwa hiyo, Mungu ndiye anayechagua ni nani atakayeokoka na ni nani ambaye hataokoka. Kwa kuwa Mungu huchagua watu wachache tu kwa ajili ya kuokoka, upatanisho unatolewa kwa ajili yao peke yao na siyo kwa watu wote. Watu hawa hawawezi kuchagua. Kwa neema ambayo haiwezi kuzuiliwa, Mungu huwafanya waweze kutubu na kuamini. Kamwe hawawezi wakaanguka na kutoka kwenye wokovu kwa sababu mapenzi yao yako chini ya uongozi wa Mungu. Hii ilikuwa ni dhana ya John Calvin kuhusiana na mamlaka aliyo nayo Mungu.

John Calvin

Calvin hakuamini kwamba neema iokoayo inapatikana kwa ajili ya kila mtu. Aliamini kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kutubu na kuamini bila ya neema maalumu, na aliamini kwamba neema hiyo haikutolewa kwa watu walio wengi.

Calvin aliamini kwamba mtu hawezi akafanya jambo lolote zuri, kama vile kutunza ahadi, kuipenda familia yake, bila ya kupata msaada wa Mungu. Aliamini kwamba Mungu huwapa watu wote neema inayowawezesha kufanya mambo mazuri. Anaiita neema hii "neema ya kawaida." Hakuamini kwamba neema ya kawaida inaweza kumpeleka mtu kwenye kuokoka.

John Wesley alikuwa na mtazamo tofauti kuhusiana na neema ya Mungu. Aliona kwamba Biblia kwa mara zote inawaita watu kuwajibika kwa Mungu. Kwa sababu ya hiyo, aliamini kwamba mwanadamu ana uweza wa kuchagua. Aliamini kama Calvin kwamba mwanadamu amepotoka na hawezi kupokea injili bila ya msaada wa Mungu, lakini aliamini kwamba Mungu hutoa huo msaada kwa kila mtu. Aliamini kwamba Mungu huwapa watu nia na uwezo wa kuwajibika, lakini hawalazimishi kuokolewa. Mungu hufanya chaguo la mwanadamu liwe

[28] Picha: "Portretten van Johannes Calvijn...", kutoka Rijksmuseum, imepatikana kutoka https://commons.wikimedia.org/wiki/index.php?curid=85920383, mali ya umma.

kitu kinachowezekana. Hii ni neema ya mwanzo inayokuja kwa kila mtu. Wanateolojia wameiita "neema ya awali," ikimaanisha kwamba ni "neema inayokuja kabla."

Neema ya Mungu huingia hadi ndani ya moyo wa mwenye dhambi, ikimhukumu kutokana na dhambi zake na ikimwonyesha kwamba yeye mwenyewe ajilaumu kwa kutengana kwake na Mungu. Neema ya Mungu husababisha awe na nia ya msamaha na anampa uwezo wa kumwitikia Mungu.

Bila ya neema, mwenye dhambi hawezi hata kuja kwa Mungu. Neema ya Mungu huja kwa kila mtu kabla hajaanza kumtafuta Mungu, ingawaje huwa hajafanya lolote ili aweze kustahili.

Kumbuka katika Waefeso 2:1-3, je, inatoa maelezo gani yasiyokuwa na matumaini? Lakini angalia aya mbili zinazofuata baada ya maelezo hayo.

> Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; (yaani, tumeokolewa kwa neema) (Waefeso 2:4-5).

Kama mtu akiwa hajaokoka, siyo kwa sababu hakuwa na neema, bali ni kwa sababu hakutaka kuwajibikia neema aliyokuwa nayo.

► Je, ni kipi kinachotangulia kwanza, mwanadamu kumtafuta Mungu au kazi ya Mungu ndani ya mwanadamu? Ni kwa jinsi gani utaielezea hii?

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 2, kifungu cha 3

Kwenye somo hili, tunamaliza sehemu ya 2 ya Waraka kwa Warumi. Tumeona ni kwa jinsi gani Wamataifa walivyokataa kuwa na ufahamu wa Mungu na wakageukia sanamu. Wayahudi walikuwa na sheria ya Mungu lakini hawakuitii. Sasa, mtume anatoa muhtasari wa hali ya ujumla ya watu wa dunia

Jambo Kuu katika sura ya 3:1-20

Kila mtu katika dunia hii ni mtenda dhambi na atasimama kwenye mahakama ya Mungu kwa ajili ya hukumu.

Muhtasari wa sura ya 3:1-20

Kifungu hiki kinatoa muhtasari wa kifungu kikubwa cha 1:18-3:20. 3:19-20 vinatoa muhtasari wa kifungu kidogo, pamoja pia na kifungu kikubwa. Sheria inaonyesha kwamba ulimwengu wote una hatia; kwa hiyo, hakuna mtu yeyote anayeweza kuhesabiwa haki kwa msingi wa matendo yake.

Maana ya kusema hivyo ni kwamba kila kila kinywa kifumbwe (3:19), ikimaanisha kwamba hakuna mtu yeyote ambaye atakuwa na sababu ya kutoa udhuru au sababu ya kujihesabia haki. 3:9 inaonyesha mtiririko wa hoja ya Paulo: Amewaonyesha kwa pamoja Wayahudi na

Wamataifa kwamba wako chini ya dhambi. Kwa kuwa hakuna hata mtu mmoja mwenye sababu ya kutoa samahani, Mungu anashughulika na watu wote kama watenda dhambi.

► Mwanafunzi atasoma Warumi 3:1-20 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(3:1-2) Paulo ameonyesha kwamba Wayahudi hawataokolewa kwa sababu tu wao ni Wayahudi; watahukumiwa kwa matendo yao sawasawa na Mataifa watakavyohukumiwa. Swali la kawaida sasa litakuwa, "Je, kweli kuna faida yeyote kwa Myahudi?" Faida kubwa ni kwamba wao ndio waliokuwa wamepewa Maandiko. Takribani Biblia yote imeandikwa na Wayahudi ambao Mungu aliwavuvia. (Faida nyingine zimeorodheshwa katika 9:4-5.)

Swali hilo hilo lingeweza likaulizwa kuhusiana na aina yeyote ya dini, au maana ya neema, kama vile ubatizo, ushirika wa kanisa, meza ya Bwana, au aina nyingine za mila za kidini. Haviwezi kutoa uhakika wa wokovu, kwa hiyo mtu anaweza akauliza, "sasa vina uzuri gani?" Jibu ni kwamba ni aina za ibada kama hizo zimetolewa kwa ajili ya kutusaidia katika imani yetu. Tunapovitendea kazi kwa imani, tunapokea neema. Lakini kama tutavifanyia kazi pasipo kuwa na imani na kama mbadala wa utii, havina thamani yeyote.[29]

(3:3) Je, itakuwaje kama wengine hawakuwa waaminifu? Je, kutokuwa kwao waaminifu kutaufanya uaminifu wa Mungu uonekane hauna maana yeyote? Swali linaloulizwa linaashiria kwamba kama Mungu hakuwaokoa Wayahudi ambao hawakutii, basi ahadi ya Mungu haikutimizwa.

Walifikiri kwamba upendeleo wa Mungu haungekuwa na masharti kwa Wayahudi. Walifikiri kwamba wangeweza wakamlaumu Mungu kwa kutokuwa mtu aliyeamini fu ingawaje walishindwa kutimiza matakwa yaliyohitajika.

Pax Romana

Pax Romana ilikuwa takriban kutoka 27 B.K. hadi A.D. 180. Maneno hayo yalimaanisha "Amani ya Rumi." Kwa sababu Waroma walichukua mamlaka ya mataifa mengi madogo, vita kati ya mataifa hayo viliisha. Hii ilisababisha biashara kufanikiwa, na watu waliweza kusafiri kwa urahisi zaidi kuvuka mipaka ya kitaifa.

(3:4) Sehemu hii ni kama kuonyesha kwamba Mungu na mwanadamu wanatofautiana katika mahakama. Uaminifu wa Mungu ukilinganishwa na mtu, kutokuwa mwaminifu kwa mtu kunathibitika. Mtume hasemi kwamba hatupaswi kupima haki ya Mungu. Anasema kwamba wakati tunapoyapima matendo ya Mungu, tutatambua kwamba yeye hapendelei na ni mwenye haki katika mambo yote aliyokwishafanya.[30]

Baadaye katika barua, tunaona kwamba kwa sababu wokovu ni wa masharti, haki ya Mungu inadhihirishwa kwa pamoja wakati anapookoa na wakati anapohukumu.

---

[29] Ushauri wa Kusoma: Mahubiri ya John Wesley, "Maana ya Neema" *"The Means of Grace,"* ," inapatikana kutoka https://holyjoys.org/the-means-of-grace/

[30] Ona "Haki ya Mungu katika Kesi" kwenye somo la 9.

(3:5) Mtume anaibua swali kwamba mtu anaweza akauliza: Kama katika dhambi yetu inaonyesha kwamba Mungu hapendelei, basi inatimiza jambo lililo jema. Kisha, je, ni vibaya Mungu kutuadhibu sisi kwa ajili ya hiyo dhambi?”

► Je, ni kwa jinsi gani utajibu swali lililoko katika 3:5?

(3:6) Hapana, kwa sababu kama dhambi ya mwanadamu itabidi iwe udhuru kwa sababu inaonesha haki ya Mungu, hakuna dhambi itakayoweza kuhukumiwa. Hii ingekuwa inakana kuwa kuna hukumu ya mwisho, ambayo ni fundisho muhimu kwa kila mtu anayeamini katika Mungu asiyekuwa na upendeleo. Zaidi ya hapo, haki ya Mungu inadhihirishwa kwenye mwanga ulio wazi wakati anapoadhibu dhambi, lakini hangeweza akaadhibu dhambi kama dhambi inakubalika kwa msingi kwamba inaonesha kuwa na haki yake. Kipingamizi hiki kinajikanusha chenyewe.

(3:7) Tena wazo hilo linapendekezwa kwamba kwa kuwa hata dhambi zetu zitatumika kuleta utukufu kwa Mungu, mwenye dhambi hapaswi kupewa adhabu. Hili ni jaribio la kutaka kutathmini vitendo kulingana na matokeo yake ya mwisho. Hata hivyo, hii ni kinyume na ukweli kwamba hukumu itakuwepo kulingana na sababu ya kutenda jambo (2:15-16). Hata hivyo, wajibu wa kuleta matokea mazuri kutokana na matendo mabaya unahusiana na Mungu peke yake. Mwenye dhambi hawezi kukamilisha mambo mema kwa dhambi yake. Dhambi huleta matokeo mabaya isipokuwa tu pale ambapo Mungu atakuwa ameingilia kati.

(3:8) Paulo anasema tu kwamba wenye dhambi na wale wanaotaka radhi kwa dhambi zao wanastahili hukumu. Pia anakanusha mashtaka ya uongo kwamba wakristo hufundisha hivyo hivyo kwa sababu dhambi zetu zaweza kuleta mema kupitia neema ya Mungu, tunapaswa tu tuikiri na kubakia wenye dhambi. Kukiri tu hali yako ya dhambi haitoshi. Mtu ni lazima atubu; lakini ili aweze kutubu kwa ukweli, ni lazima aione dhambi yake kuwa kweli ni uovu.

(3:9) Neno "Sisi" inarejelea Wayahudi. Hawana hadhi ya kiroho inayojileta yenyewe. Wote wako chini ya dhambi; wametenda dhambi na wako chini ya hukumu yake.

(3:10-18) Aya hizi ni nukuu kutoka Zaburi na manabii wa Agano la Kale.[31] Baadhi ya watu hunukuu 3:10 na kusema inamaanisha kwamba hakuna mtu mwenye haki, hata yule ambaye ni Mkristo. Hata hivyo, 3:10-18 haiwezekani kuwa inamwelezea Mkristo. Kama mtu yeyote atafikiri kwamba hii inamwelezea Mkristo, jaribu kufikiria kuweka jina la Mkristo unayemjua kwenye sentensi hizi. Kwa mfano, kinywa cha Mchungaji Petro kimejaa laana, miguu yake ni miepesi kwenda kuua, na hana hofu ya Mungu.”

Aya hizi zinaelezea hali ya ujumla ya wale ambao hawajaokoka. Ni sawa na maelezo yaliyoko kwenye 1:29-31. Kusudi la Paulo ni kuonyesha kwamba hakuna mtu anayeweza

[31] Zaburi 14:1-3, Zaburi 53:1-3, Zaburi 5:9, Zaburi 140:3, Zaburi 10:7, Isaya 59:7-8, Mithali 1:16, Zaburi 36:1

kupata wokovu kwa matendo yake. Rum 3:10-18 inaonesha kuwa hakuna mtu mwenye haki bila ya kuwa amepata haki ya Mungu.

► Je, ni kwa jinsi gani unaweza kujibu taarifa hii: "Hakuna mtu atakayeweza kujinadi kwamba anaishi kwa ushindi dhidi ya majaribu kwa sababu Biblia inasema kwamba hakuna mtu yeyote mwenye haki"?

3:19-20 hazitoi tu muhtasari wa 3:1-20, bali 1:18 - 3:20.

(3:19-20) Sheria haikuwa imetolewa kwa ajili ya kuwaonesha watu jinsi ya kuhesabiwa haki, bali kuonesha kwamba kila mmoja tayari ni mwenye hatia. Sheria siyo kwa ajili ya kuhesabiwa haki, bali hukumu. "Kwamba kila kinywa kiweze kufumbwa" inamaanisha kwamba hakuna mtu mwenye udhuru au msingi wa kujihesabia haki yeye mwenyewe. Hawezi kujitetea mwenyewe katika mahakama ya Mungu.

Mtu afikiriaye kwamba anapaswa kushika sheria ili akubaliwe na Mungu yuko chini ya sheria. Kuwa chini ya sheria haina maana ya kurejea kwenye kipindi cha historia cha Agano la Kale. Mtu yeyote yuko chini ya sheria kama hatakua amepokea neema inayookoa.; kwa sababu kama ilikuwa aende kwenye hukumu ya Mungu, atakuwa amehukumiwa kwa kuvunja sheria. Mtu huwa hayuko tena chini ya sheria kama anakuwa ameokoka kwa sababu amekubaliwa na Mungu kwa msingi wa neema.

► Je, inamaanisha nini kuwa chini ya sheria?

Kuhesabiwa haki kwa imani

Ni lazima kila mmoja kuelewa jinsi menye dhambi naweza kusamehewa mbele ya Mungu. Hapatakuwa na Amani au kupata furaha tukiwa maadui wa Mungu, ikiwa ni wakati wa sasa au katika umilele unaokuja[32]

Watu waliumbwa kwa sura ya Mungu na walikuwa watakatifu, kama vile Mungu muumba wao alivyo mtakatifu. Kama Mungu alivyo mwenye upendo, ndivyo alivyo mtu mme na mke, wakiishi katika upendo, waliishi katika Mungu na Mungu akiwa ndanbi yao. Walikuwa watakatifu, kama Mungu alivyo, mbali na kila doa la dhambi. Hawakujua dhambi ndani na nje walikuwa bila dhambi. Walimpenda Bwana Mungu wao kwa mioyo yao yote, akili, nafsi na nguvu zao.

Mungu akampa Adamu, mtu mwenye haki na mkamilifu, na sheria kamilifu. Mungu akahitaji kwake utii kamili, ambao Adamu angeuweza. Hata hivyo Adamu na Hawa walimwasi Mungu (Mwanzo 3:6).

Mara moja Adam akahukumiwa kwa hukumu ya haki ya Mungu. Mungu alikuwa amemwonya Adamu kuwa adhabu ya kutokutiii ingekuwa ni kifo (Mwanzo 2:17). Mara Adamu alipoonja tunda lililokatazwa, alikufa. Roho yake ilikufa kwa sababu alitengwa na

[32] Sehemu hii ni sehemu ya hotuba ya Wesley, "Kuhesabiwa haki kwa imani," inapatikana kutoka https://holyjoys.org/justification-by-faith/

Mungu. (Bila Mungu nafsi inakosa uhai). Kadhalika, na mwili wake unakufa. Kwa kuwa amekufa rohoni, amekufa kwa Mungu, na amekufa kwenye dhambi, aliingia katika kifo cha milele; aliingia kwenye hukumu ya milele; kwenye adhabu ya mwili na roho katika jehanamu ya moto, ambayo haizimiki.

"dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi (Warumi 5:12). Dhambi ilikuja kupitia Adam, ambaye alikuwa ndiye baba na mwakilishi wetu sote. Kwa sababu ya hili, watu wote walikufa —wafu kwa Mungu, wafu kwenye dhambi, kuishi katika mwili wa kufa ambao sio muda mrefu unasambaratika, na unakuwa chini ya hukumu ya kifo cha milele. Kwa kutokutii mtu moja watu wote wakafanywa wenye dhambi (Warumi 5:19) na "…kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu…" (Warumi 5:18).

Watu wote wakawa katika hali hii ya uenye dhambi na kuhukumiwa—Mungu akaupenda ulimwengu, hata akamtoa mwana wake pekee, ili kwamba tusipotee, bali tuwe na uzima (Yohane 3:16). Mwana wa Mungu akawa mtu, kichwa cha pili cha familia za wanadamu . kwa namna hiyo akachukua huzuni zetu (Isaya 53:4), Na Bwana akaweka juu yake Maovu yetu sisi sote (Isaya 53:6). alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu (Isaya 53:5). Akafanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi (Isaya 53:10). Alitoa damu yake kwa ajili ya wenye dhambi. Akafanya sadaka kamili na kamilifu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote

Kwa sababu mwana wa Mungu alionua mauti kwa ajili ya kila moja (Waebrania 2:9), yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao (2 Wakorintho 5:19). "…kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima" (Warumi 5:18). Kwa sababu ya mateso ya mwana wake kwa ajili yetu, Mungu sasa anatupa uhakika wa kufuta adhabu ya dhambi tuliyoistahili kwa ajili ya dhambi zetu, ili kuturudisha kwake, na kutufanya upya roho zetu mfu na kuzipa uzima, huku akitupa uhakika wa uzima wa milele. Ahadi hii ina sharti moja, ambayo anatuwezesha kuifikia.

► Je, sharti moja linalotajwa katika aya ya mwisho ni nini?

Neema katika Agano la Kale

► Je, kulikuwa na neema na uzoefu gani wa kiroho uliokuwa unapatikana kwa ajili ya watu walioishi wakati wa Agano la Kale? Kwa nini swali hili ni muhimu?

Baadhi ya watu wanaamini kwamba watu kwenye Agano la Kale hawakuweza kubadilishwa au kuokoka na kupata uzoefu wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, hawaoni umuhimu wa Agano la Kale kwa ajili ya waamini wa leo. Wanafikiri kwamba wokovu kwa njia ya neema kupitia imani ilianza na Agano Jipya. Wanafikiri kwamba watu kwenye Agano la Kale wangeweza wakaokoka kwa kutumia sheria na dhabihu.

Ukweli ni kwamba kamwe hakuna mtu yeyote aliyewahi kuokoka kwa kuishika sheria au kwa kutoa dhabihu (Waebrania 10:4). Kwa hiyo, walikuwa wanaokokaje? Kwa njia ya neema kupitia imani.

(1) Agano Jipya linasema kwamba Injili iko kwenye Agano la Kale

- Agano la Kale linafundisha kuhusu wokovu kwa njia ya imani kupitia Yesu Kristo (2 Timotheo 3:15).
- Ibrahimu alikuwa na injili na alihesabiwa mwenye haki kwa njia ya imani (Warumi 4:1-3; Wagalatia 3:6, 8).
- Daudi alielezea kuhusu kuhesabiwa haki kwa njia ya imani (Warumi 4:6-8).
- Injili ilikuja mwanzo; sheria ikafuata baadaye (Wagalatia 3:17).
- Watu wa Agano la Kale walikuwa na injili ikihubiriwa kwao kama inavyofanyika kwetu (Waebrania 4:2).
- Yesu alionyesha kwamba Nikodemo alikuwa ameshajua kuhusu uzao mpya kutokana na kujifunza kwake Agano la Kale (Yohane3:10).
- Haki hutolewa kwa sababu ya Imani (Warumi 1:17), inashuhudiwa na sheria na manabii (Warumi 3:21).

(2) Elimu nyingi siyo muhimu katika kupokea neema kwa njia ya imani.

Yesu alihubiri kuhusu toba na msamaha lakini hakuelezea kuhusu upatanisho. Watu walikuwa wanaokoka kwa kuamini ujumbe wake (kwa mfano, mwanamke Msamaria pale kisimani, Yohane 4:39-42).

Waamini wa Agano la Kale hawakuwa wanaelewa kuhusu upatanisho, lakini walichokuwa wanahitaji ni kuamini tu kwamba Mungu alikuwa anatoa njia ya msamaha kwa ajili yao. Kisha wangeweza wakaokoka kwa neema kwa njia ya imani, na siyo kwa matendo yao au kwa kutoa dhabihu. Dhabihu zao na utii wao zilikuwa ni udhihirisho wa imani yao, kama ilivyo kwetu.

Endapo mtu atamtii Mungu, Mungu atamwonesha njia ya kumleta kwenye uhusiano naye Zabu 25:14 inasema “Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha agano lake.”

(3) Amri za Mungu hufanya neema iwe muhimu.

Yesu alisema katika Mathayo 22:37-40 kwamba amri zilizo muhimu ni kumpenda Mungu kwa namna yeyote ile ulivyo (Kumbukumbu la Torati 6:5) na kumpenda jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe (Walawi 19:18). Haiwezekani kuzitii amri hizi bila ya neema. Je, Mungu aliamuru mambo yasiyowezekana kwa ajili ya watu katika Agano la Kale, au aliwezesha utii kwa njia ya neema?

Usilipe uovu kwa uovu (Mithali 24:28-29). Watendee mema wale wanaokutendea maovu (Mithali 25:21-22). Ukimwona ng'ombe au punda wa adui yako amepotea mrudishe (Kutoka 23:4-5). Usifurahi, adui yako aangukapo (Mithali 24:17).

(4) Mungu alitegemea watu wa Agano la Kale waishi maisha ya utii.

Kumbukumbu la Torati 27 na 28 pameorodheshwa baraka zinazotokana na kutii na laana zinazoambatana na kutokutii. Laana hizi zinahusisha kila kitu kinachoweza kufikirika. Kama ingekuwa hakuna neema ya kufanya kutii kuwe ni kitu kinachowezekana, watu hawa walitengwa kupokea laana za aina zote na kupoteza baraka zote.

(5) Mungu alitoa kazi ya neema kubadilisha mioyo yao.

Katika Kumbukumbu la Torati 30:6 panasema kwamba kwa pamoja wao na madhuria wao wanaweza wakatahiriwa kwenye moyo, ili waweze kutii na kuishi. Katika 30:11-20 tunaona mambo yafuatayo: Walikuwa hawapaswi kusema kwamba ilikuwa ni vigumu kupokea, kwa sababu ilikuwa ndani ya midomo na mioyo yao – taarifa iliyonukuliwa na Paulo katika Warumi 10:6-8 inarejelea kwenye neema iliyopokelewa kwa imani. Suala litaamuliwa ndani ya mioyo yao (Kumbukumbu la Torati 30:17). Upendo kwa Mungu utaongoza kwenye utii (Kumbukumbu la Torati 30:20).

(Ona pia Kumbukumbu la Torati 10:12, 16.) Alichokuwa anakihitaji Mungu ni upendo mkamilifu na utakaso wa moyo. Kutahiriwa kwa moyo kungefanya hili liwezekane kufanyika.

(6) Watu wa kweli wa Mungu kwa wakati wowote – ni wale wanaompenda na kumtumikia.

Warumi 2:28-29, Wakolosai 2:11-12, na Wafilipi 3:3 kwa pamoja panasema kwamba Myahudi wa kweli ni yule aliye wa kiroho. Mitume walisema jambo kama hilo linalofanana. Wokovu unategemea utii wa moyo, na dhabihu hazikuweza kuhalalisha mioyo ya uovu. Stefano aliwalaumu Wayahudi wa wakati wake kwa kuwa kama mababu zao wa Agano la Kale ambao Walikuwa hawajatahiriwa mioyo yao na masikio (Matendo 7:51). Hakuna wakati ambapo Mungu aliwataka tu watu wafanye namna za ibada.

Daudi aliomba, "Maneno ya kinywa changu, Na mawazo ya moyo wangu, Yapate kibali mbele zako" (Zaburi 19:14).

(7) Kuna mifano mingi ya neema katika Agano la Kale.

- Ayubu alikuwa na hofu ya Mungu na aliukataa uovu (Yobu 1:1).

- Nuhu alikuwa mwenye haki na mkamilifu (Mwanzo 6:9).
- Isaya alikuwa na uzoefu wa kutakasa moyo (Isaya 6).
- Daudi aliomba kwa ajili ya utakaso kwa ajili ya dhambi zake (Zaburi 51).

Ushahidi unaonesha kwamba wokovu na moyo ulio mweupe ulikuwa unapatikana katika Agano la Kale. Hii inamaanisha kwamba Agano la Kale ni muhimu kwetu. Maelekezo ya Mungu kwa ajili ya maisha ya haki kwenye Agano la Kale yalikuwa ni maelekezo kutoka kwa Mungu aliye Mtakatifu kwenda kwa watu wake ambao walikuwa wanapaswa waishi kwenye neema. Bila shaka, amri nyingi zilikuwa ni maalumu kwa wakati na hali ile na haitendi kazi tena nasi kwa njia ile ile iliyokuwa inatumika kwa wakati ule. Katika somo la 7 ni sehemu inayoelezea jinsi ambavyo tutatumia Maandiko ya Agano la Kale kwenye maisha yetu.

Maswali ya Mapitio Somo la 4

(1) Elezea dhana ya Calvin ya "neema ya kawaida".

(2) Elezea dhana ya Wesley ya "neema ya awali" yaani neema inayotangulia.

(3) Katika Warumi 3:19, maneno "kila kinywa kufumbwe" yana maanisha nini?

(4) Je, ni manufaa gani mabwa yanatajwa kwa Wayahudi katika Warumi 3?

(5) Je, aina mbali mbali za kuabudu zinatunufaishaje?

(6) Je, Warumi 3:10-18 inaonesha nini?

(7) Je, ni nani aliyeko chini ya sheria? (Warumi 3:19-20)

Kazi ya kufanya Somo la 4

(1) Andika ukurasa mmoja kuhusiana na mmoja mada zifuatazo:

- Neema ya awali
- Neema katika Agano la Kale
- Sababu zinazopelekea wenye dhambi kuhitaji kuhesabiwa haki kwa njia ya imani

Unaweza ukatumia mchangayiko wa maandiko mbalimbali tofauti na kitabu cha Warumi endapo itahitajika.

(2) Kumbuka kwamba unahitajika kuhubiri mahubiri matatu au kufundisha vipindi vitatu kwa vikundi vingine wakati kozi hii ikiwa inaendelea.

Somo la 5
Njia na Maana ya Kuhesabiwa Haki

Kutoa maana ya Imani Inayookoa

► Je, imani inayookoa ni nini? Kama mtu atakuwa anayo imani inayookoa, hiyo inamaanisha kwamba ameamini nini?

Je, mtu aliyeamini anaamini nini?

(1) Anaamini kwamba hawezi kufanya lolote katika kujihesabia haki mwenyewe.

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9).

Anatambua kwamba hawezi kufanya lolote (matendo) litakalomfanya astahili kuokoka, hata kwa sehemu kidogo tu.

(2) Anaamini kwamba dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake.

" Naye ndiye kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote" (1 Yohane 2:2).

Kipatanisho inamaanisha ni dhabihu inayofanya msamaha wetu uwezekane.

(3) Anaamini kwamba Mungu atamsamehe yeye kwa sharti la imani peke yake.

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohane 1:9).

Kama anafikiria kwamba kuna masharti mengine, anategemea kuokoka kwa matendo badala ya kuokoka kabisa kwa neema.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 3

Sehemu ya 3 ina vifungu vitatu. Kifungu cha kwanza (3:21-31) kinaonesha kwamba mwanadamu ni lazima athibitishwe kuwa mwenye haki kwa njia ambayo Mungu hupanga mwenyewe, kwa kuwa mwanadamu hawezi kujihesabia haki mwenyewe katika lolote alilolitenda. Kifungu cha pili (Warumi 4) inamtumia Ibrahimu na Daudi kama vielelezo vya kuthibitisha imani, ikionyesha kwamba fundisho la imani siyo kitu kigeni. Kifungu cha tatu (Warumi 5) kinaelezea jinsi dhabihu ya Kristo inavyoweza kufanya aina hii ya kufanywa mwenye haki iwe kitu kinachowezekana. Katika somo ili tutajifunza aina zote tatu za vifungu hivi.

Jambo Kuu katika sura ya 3:21 - 5:21

Alichokitoa Mungu kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu ni dhabihu ya Kristo, ambayo inaleta kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 3, kifungu cha 1

Jambo Kuu katika sura ya 3:21-31

Njia ambayo Mungu ya kumhesabia mtu haki ni kwa neema kwa njia ya imani, na kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo haiwezekani.

Muhtasari wa kifungu cha sura ya 3:21-31

Kwa kuwa hakuna mtu yeyote mwenye haki kwa msingi wa kuhifadhi sheria zote kwa wakati wote, njia nyingine ya kuhesabiwa mwenye haki ni lazima itafutwe. **Tatizo (lililotolewa katika 3:26) ni kwa ajili ya Mungu kumhesabia haki mwenye dhambi na bado akaendelea kuwa jaji mwenye haki**. Tatizo hili linatatuliwa kwa upatanisho; Mungu alitoa dhabihu kama msingi wa msamaha. Anaweza kumsamehe mtu aaminiye, lakini dhabihu huonesha kuwa Mungu huzichukulia dhambi kwa uzito wa hali ya juu sana.

► Mwanafunzi anapaswa asome Warumi 3:21-31 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(3:21) Haki inayokubalika kwa Mungu inakamilika mbali na sheria. Mtume anasema kwamba wazo hili siyo jambo geni, lakini lilifundishwa katika sheria hata na mitume. "Lakini sasa" linarejelea kwenye wakati wa ufunuo kamili wa injili katika Kristo, kama aya inayofuata inavyosema. (Ona pia 3:25).

(3:22-23) Hakuna njia tofauti ya kuokolewa kati ya Wayahudi na Wamataifa kwa sababu wote wanahukumiwa sawa. Hata katika Israeli ya kale, wakati walipofuata mila ambayo Mungu aliwapa, hakuna hata wakati mmoja ambao mtu aliokolewa kwa njia ya dhabihu au mila. Mtu yeyote aliyeokolewa, aliokoka kwa kupokea neema kwa njia ya imani. (Ona aya ya 30.)

Wokovu kwa kila mtu ni kwa njia ya imani. Neno *wote* linatumika mara nyingi hapa. Kama ambavyo wote wametenda dhambi, wote walioamini wanaweza wakaokolewa. Kifungu kinachosema "kwa wote waaminio" msisitizo jinsi unavyopatikana kwa kila mtu. Na "toka imani hadi imani" kinaweka msisitizo wa hali ya imani (1:17).

(3:24) Neema ni ya bure kwa ajili yetu kwa sababu Yesu alilipa gharama ya ukombozi.

(3:25) dhambi zote zilizotangulia kufanywa ni dhambi ambazo zilishawahi kufanywa kabla ya ujio wa Kristo. Hawakulipia makosa kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe, bali kwa kifo cha Kristo, ingawaje wakati dhambi zilipokuwa zinatendwa, kifo chake kilikuwa ni cha wakati ujao wa baadaye. Mungu aliwasamehe kwa msingi wa upatanisho wa Kristo kabla haijatokea, kwa sababu ilikuwa imepangwa hivyo tangu mwanzo (ona 3:21).

Upatanisho unaonesha kwamba Mungu alikuwa mwenye haki ingawaje haki yake ilikuwa siyo ya mara moja. Ilionyesha kwamba Mungu huichukulia dhambi kwa uzito wa hali ya juu sana.

(3:26) Aya inaonyesha ufumbuzi wa tatizo kubwa: Ni kwa jinsi gani Mungu anaweza kuwa mwenye haki halafu bado anamhesabia haki mwenye dhambi? Upatanisho ulionesha njia. Mungu alitoa dhabihu kama msingi wa msamaha. Anaweza kumsamehe mtu anayeamini na dhabihu inaonesha kwamba Mungu huzichukulia dhambi kwa uzito wa hali ya juu sana.

► Je, kutakuwepo na tatizo gani endapo Mungu atawasamehe watu bila ya upatanisho?

Mungu ni hakimu wa haki wa ulimwengu huu. Alishatangaza kwamba dhambi ina uzito mkubwa sana kiasi ambacho imewekewa adhabu ya milele. Watu wanatenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Mungu anawajibika na haki ya mwisho ya ulimwengu, thawabu kwa ajili ya wanaotenda mema na adhabu kwa ajili ya wale wote watendao maovu.

Msamaha bila ya kuwepo na msingi wa msamaha huo utaleta mgogoro wa utambulisho halisi wa Mungu. Itaweza kumshushia heshima yake kwa kumfanya aonekane hana msimamo katika kushughulikia dhambi. Ataonekana hana haki kama atawaadhibu baadhi ya watu na watu wengine akawasamehe. Hili siyo tatizo dogo, kwa sababu ulimwengu wote upo kwa ajili ya kumtukuza Mungu. Je, ni kwa jinsi gani watu wanaweza wakamtukuza Mungu kama hawatafikiria kwamba yeye ni mwenye haki?

Suluhu ya hili inabidi kuwepo na kitu ambacho kitaonyesha kwamba dhambi ni hali yenye kuchukuliwa uzito mkubwa sana, kuna sababu ya msamaha, na asili ya Mungu idhihirishwe; ili watu wapate kuendelea kumheshimu Mungu kama mtakatifu na mwenye haki.

Upatanisho ndio unaofaa katika hitaji hilo. Dhabihu iliyotolewa juu ya dhambi ya msalaba inaonesha kwamba dhambi ni hali yenye kuchukuliwa uzito mkubwa sana. Umuhimu wa kutubu unamfanya mwenye dhambi aweze kukiri dhambi zake. Kutolewa bure kwa wokovu kwa ajili ya watu wote kunafanya uchaguzi uwe wa mtu binafsi, ili iwe kwamba ni haki kwa Mungu kuweza kumsamehe mtu anayekubaliana na wokovu na asimsamehe yule anayeukataa wokovu.

Je, ni kwanini Mungu hawezi kuwasamehe wale watu wanaokataa kutubu? Kumsamehe mtu ambaye anaendelea kuwa kwenye dhambi bila kutubu ni kulikosea kusudi la upatanisho: ni kutoa msamaha wakati kuna haki ya Mungu inadai kutimizwa.

(3:27) Mtu hana sababu ya kujisifu kwa ajili ya kupata wokovu. Kumekuweko na baadhi ya watu wanaoamini kwamba mtu anaweza kujivunia kama akijijua kwamba ameokoka. Lakini mtu anayejijua kwamba amesamehewa kwa sababu ya neema anayo sababu ya kuwa na unyenyekevu na siyo kiburi.

(3:28) Kuhesabiwa haki hakutegemei haki iliyokwisha kuwepo nyakati zilizopita. **Kuhesabiwa haki inamaanisha kwamba mwenye dhambi anayetubu na kuamini anahesabiwa kuwa mwenye haki kama ambaye hajawahi kufanya dhambi tena.**

Maisha ya utii kwa Mungu yanaanzia kwenye kuhesabiwa haki, na siyo kabla ya hapo. Mtu hawezi kuyabadillisha maisha yake mwenyewe kwa kusudi la kumfanya yeye binafsi akubalike kwa Mungu. Anakuwa tayari ameshakubalika kwa Mungu kupitia upatanisho wa Kristo, na siyo kwa njia nyingine yeyote.

(3:29-30) Aya hizi zinaunganisha kifungu kwenye mada ya kitabu. Ujumbe ni kwa ajili ya ulimwengu mzima. Matumizi haya ya injili ulimwenguni kote yana msingi wake kwenye imani kwamba kuna Mungu mmoja tu Kwa kuwa kuna Mungu mmoja tu, makusudi yake hufanya kazi kwa wanadamu wote, tofauti na mungu wa kienyeji ambaye huenda akapendezwa na taifa moja tu au ukoo mmoja tu Siku zote Mungu alikusudia kwamba Israeli ishirikishane ufahamu wa Mungu pamoja na Wamataifa (Isaya 42:6, Isaya 43:21, Isaya 49:6).

► Mtume alisema kwamba kuhesabiwa haki kwa njia ya imani hakuharibu sheria, bali kuidumisha. Je, jambo hili likoje?

(3:31) Wakati mtu anapotubu dhambi zake na kuanza kuishi maisha ya utii, anakuwa anaidumisha sheria ya kuwa ni kipimo cha haki. dhana yeyote ya upatanisho na kuhesabiwa haki ambayo itaifanya sheria ionekane kwamba haina maana kwa Mkristo haiendani na aya hii.[33] Kama mtu akiomba msamaha lakini hatarajii kuanza kumtii Mungu, inaonesha kwamba haelewi uovu wa dhambi na sababu halisi ya yeye kuhitaji msamaha. Anajitahidi kupata faida za wokovu kwa kujifanya tu kwamba anaheshimu sheria.

> "Hakuna mtu anayeweka sheria kwa ukamilifu kama wale ambao wametubu na kugeuka kabisa kutoka katika matendo yao ya dhambi na kumtegemea Yesu ka ajili ya wokovu."
>
> - George McLaughlin,
> *Maelezo ya Warumii*

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 3, kifungu cha 2

Jambo Kuu katika sura ya 4

Ibrahimu, aliyekuwa amechaguliwa na Mungu kuwa baba wa watu wa Mungu, alihesabiwa haki kwa njia ya imani.

Muhtasari wa sura ya 4

Fundisho la imani kuhusu kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani linapatikana katika kitabu cha Agano la Kale. Ibrahimu, aliyekuwa amechaguliwa na Mungu kuwa baba wa watu wa Mungu, alihesabiwa haki kwa njia ya imani. Mfalme Daudi pia alielewa kuhusu kuhesabiwa haki kwa neema. Kutahiriwa hakukuwa njia ya kupata wokovu lakini baadaye ilifanyika kama ishara ya imani ambayo Ibrahimu tayari alikuwa nayo. Ibrahimu alikuja kuwa baba na mfano wa wale wote ambao baadaye waliokoka kwa njia ya imani.

[33] Mahubiri ya John Wesley yanayohusiana na jinsi sheria inavyoanzishwa kwa imani yanaelezea dhana hizi vizuri zaidi. (Angalia sehemu ya nyumba ya somo hili kuhusu vitabu vingine vinavyopendekezwa kusoma.)

► Mwanafunzi anapaswa asome Warumi 4 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(4:1) Ibrahimu alikuwa baba wa kimwili wa Wayahudi. Swali ni kwamba, je, "Alipokea nini hasa?" Swali hili litajibiwa ili kujibu maswali "Nani anaweza kuwa mrithi?" na "Ni kwa jinsi gani tunaweza kuwa warithi?"

(4:2) Dhana ya wokovu kwa njia ya matendo kwa kawaida husababisha kuwa na kiburi.

► Je, Ibrahimu alikuwa na imani ya aina gani ambayo ilihesabika kama imani inayookoa?

(4:3) Ibrahimu hakuwa anajua mpango mzima wa wokovu, kwa hiyo, hangeweza kuweka imani yake kwenye upatanisho wa Kristo. Hata hivyo, aliamini ahadi ya Mungu kama ambavyo ilikuwa imefunuliwa kwake. Sehemu ya ahadi ambayo imetajwa katika sura hii ni kwamba Ibrahimu atakuwa baba wa mataifa mengi (4:17-18), lakini sehemu nyingine ya ahadi iliyobakia ni kwamba watu wote wa ulimwengu huu watabarikiwa kupitia uzao wake (Mwanzo 12:2-3, Mwanzo 22:17-18). Ahadi hii ilirudiwa tena kwa Yakobo (Mwanzo 28:14). Kupitia uzao wake neema ya Mungu itatolewa kwa watu wote wa ulimwengu huu. Hii ilikuwa ni ahadi ya neema ya Mungu kwa Ibrahim. Iliyotolewa kwa watu wote.

Ibrahimu alihesabiwa haki kwa neema kwa kuwa aliiamini ahadi ya neema Mungu. Kuhesabiwa kwake haki kulikuwa ni sawasawa na inavyokuwa kwetu, ingawaje imani yetu ina maudhui ya zaidi.

(4:4) Kama mtu anafanya kazi ili apate wokovu wake, wokovu siyo zawadi. Badala yake yeye anadaiwa kwamba anajaribu kujifanyia malipo (ona Warumi 11:6).

(4:5) Mtu ambaye hafanyi kazi siyo mtu ambaye hajali kuhusu kumtii Mungu, lakini ni mtu ambaye hafanyi kazi ili kuokoka. Badala ya kutegemea matendo yake ili yampatie nafasi ya kuingia mbinguni, anaamini ahadi ya Mungu ya kumwokoa.

(4:6-8) Daudi pia alirejelea kwenye kuhesabiwa haki kwa imani wakati alipoelezea kukubaliwa na Mungu ambako kunategemea msamaha wa dhambi. Mungu hawezi kumhesabia mtu aliyeamini kuwa mwenye hatia kwa dhambi ya zamani iliyokwishapita. Mtume anaonyesha hapa kwamba fundisho la imani kuhusu kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani sio wazo Jipya – hata mfalme Daudi alilielewa hilo.

Je, ni kwa jinsi gani tutajua kwamba jambo hili linahusika na dhambi ya zamani iliyopita na siyo dhambi inayoendelea? Kwenye Warumi 6:2 panasema kwamba sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi. Ujumbe wote wa Warumi 6 unakataa wazo la kwamba tunaweza tukaishi kwenye dhambi na wakati huo tukiendelea kuhesabiwa haki kwa njia ya imani. (Ona pia Warumi 5:6-8: "tulipokuwa hatuna nguvu" na "tulipokuwa tungali wenye dhambi," ina maana kwamba sasa tuna nguvu na si wenye dhambi kama hapo awali, lakini tumehesabiwa wenye haki na kubadilishwa.)

(4:9) Swali hili linatambulisha mada kwamba ni kwa jinsi gani mtu anaweza kuingia kwenye nafasi hii ya kuhesabiwa mwenye haki kwa njia ya imani. Je, baraka hizi huja tu kwa watu ambao wametahiriwa?

► Je, ni kitu gani kilitangulia kwanza: sheria au neema?

(4:10-12) Ibrahimu hakuwa ametahiriwa wakati alipopokea neema. Kutahiriwa kulikuja baadaye. Kwa hiyo, inawezekana mtu ambaye hajawahi Kutahiriwa akapokea neema kwa njia ya imani. Ibrahimu ni baba wa imani kwa wale wote wanaofuata mfano wake. (wanaotembea katika hatua zake) za imani, hata kama hawajawahi kutahiriwa. Watu ambao wana imani inayookoa ni Watoto wa kiroho wa Ibrahimu. Waisraeli siyo watoto wake wa kiroho hadi wawe wameamini, ingawaje kibiolojia ni uzao uliotoka kwake.

(4:13-14) Je, ni nani mrithi wa baraka za Ibrahimu? Kama ni wale wanaoshika sheria, basi siyo imani iliyoko kwenye ahadi.

(4:15) Sheria ndiyo inayohalalisha hukumu kwa kuwa inaonyesha dhambi. Siyo sababu ya kupokea neema. Kama hakungekuwepo na sheria, pia hakungekuwepo na uvunjaji wa sheria. Paulo hazungumzii hasa kuhusu sheria ya Musa, bali mahitaji ya Mungu kuhusiana na mwanadamu kwa ujumla. Hakuna mahali ambapo mahitaji ya Mungu hayafahamiki kabisa. (1:20)

(4:16-17) Ibrahimu alikuwa na uzao mwingi wa kibiolojia waliofanyika kuwa mataifa mengi. Hata hivyo, mtume hapa anasema kwamba Ibrahimu alikuwa ni baba wa wengi kwa sababu ni baba wa wale wote walio na imani.

Wokovu unapokelewa kwa imani ili utolewe kwa neema. Kama matendo yeyote yalikuwa yanahitajika ili mtu aweze kuwa na sifa ya kupokea wokovu, haitakuwa tena ni kwa neema. Kwa kuwa ni kwa neema, ni lazima ipokelewe kwa imani peke yake. Mtu anayejaribu kuufanyia kazi wokovu kwa matendo yake haelewi maana ya wokovu.

► Je, ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu ilikuwa nini? Ilikuwaje sawa na ahadi ya wokovu tunayopokea?

(4:18-19) Ibrahimu alimwamini Mungu hata wakati ambapo hapakuwepo na mazingira ya kumpa matumaini. Mwili wake ulikuwa sawa na umekufa ukizingatia uwezo wake wa kupata mtoto. Sara alikuwa pia ameshapitiliza muda ule wa mwili kuwa na uwezo wa kubeba mtoto. Lakini imani ya kweli haina utegemezi na aina za mazingira yaliyopo.

Imani hii ni kinyume na kutegemea matendo. Hii inaelezea ni kwa nini Ismaili, mwana wa Hagai, ni mfano wa wokovu kwa njia ya matendo (Wagalatia 4:22-31). Kuzaliwa kwa Ismaili kulifikiwa kwa njia ya kimwili, badala ya imani. **Wokovu ni kwa ahadi, kisha imani, halafu miujiza.**

(4:20-21) Mungu hutukuzwa zaidi na imani ya mwanadamu kuliko uwezo wa kibinadamu.

(4:22) Ona maelezo katika aya ya 3.

► Je, tunapokea wokovu ule ule ambao Ibrahimu alipokea?

(4:23-25) Imani ya Ibrahimu ni mfano wa kuigwa kwetu sisi. Hakuwa anajua mpango mzima wa wokovu lakini aliamini sehemu ya kile ambacho kilikuwa kimefunuliwa kwake. Ni lazima tuamini kwa undani yale yote yaliyofunuliwa katika mpango wa wokovu ambao Ibrahimu hakuwahi kujua: kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. Aya hizi zinaonyesha kwamba tunapokea kuhesabiwa haki kama vile Ibrahimu alivyopokea, kwa sababu inasema kwamba haki ilihusishwa na yeye na itahusishwa na sisi pia katika msingi huo huo unaofanana.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 3, kifungu cha 3

Jambo Kuu katika sura ya 5

Kristo katika kifo chake na kufufuka kwake alibatilisha matokeo ya dhambi akaleta upatanisho, haki, na uzima.

Muhtasari wa sura ya 5

Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo (5:1). Kifungu kinachosema "kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo" kinatoa utambulisho wa sura hii: ufanisi wa kazi ya upatanisho ya Kristo. Dhambi ya Adamu iliufanya ulimwengu ukawa chini ya dhambi na kifo, na kila mwanadamu baada yake ametenda dhambi. Upatanisho wa Kristo ulipindua madhara ya dhambi.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 5 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(5:1-2a) Aya hii inaunganisha sehemu iliyopita pamoja na sehemu hii ya sasa. Somo la sura hii ni ufanisi wa kazi ya upatanisho ya Kristo. Amani inayorejewa inahusika na upatanisho pamoja na Mungu - uadui ukiondolewa na ghadhabu au hasira ikiwa imetupiliwa mbali.

> Upendo wa Mungu hauna sababu, hauna kipimo, na haukomi.

Yesu alisema kwamba yeye ni mlango (Yohane 10:9). Aya hii inasema kitu kinachofanana, kwa sababu kwa kupitia yeye tunayo njia ya kuingia kwenye neema kwa njia ya imani. Yeye ni njia, kweli na uzima (Yohane 14:6).

(5:2b-5) Aya hizi zinaelezea uzoefu wa mtu aliyeamini anapokuwa anaishi kwenye neema.

Paulo alisema kwamba furaha yetu iko kwa sababu ya matumaini kwamba tutauona utukufu wa Bwana. Alisema kwamba tunaweza tukafurahia hata katika nyakati za mateso.

Mkristo anaweza akafurahia na kuvumilia mambo madogo (hali a maisha) kwa sababu mambo makubwa yana usalama. Mtu asiyeamini hujaribu kujipatia furaha yake kutoka katika vitu vya kimaisha. Lakini vitu vya kimaisha kamwe siyo vizuri kwa ajili ya kuleta utoshelevu wa kutosha; vinapita kwa haraka. Hali za maisha siyo mbaya sana kama maisha

ni ya safari, lakini hali za maisha huonekana kuwa za kusikitisha sana kama hakuna kitu kingine chochote.

Kuvumilia mateso kwa uaminifu kunakamilisha mchakato kwa ajili ya mtu aliyeamini. (Ona pia Yakobo 1:2-4.) Tunapokuwa tunavumilia mateso kwa imani, tunajenga uvumilivu. Uvumilivu siyo tu uhiari wa kusubiri; ni uwezo wa kuvumilia kwa imani. Tunavyoendelea kufanyia mazoezi imani hii ya uvumilivu, tunaendelea kuwa na mazoea na kuiangalia kazi ya Mungu ambayo inatupa sisi matumaini. Tunajua kwamba makusudi ya Mungu yanakamilishwa hata katika wakati ambapo hali ya mambo yanaonekana kuwa mabaya.

► Je, unajifariji vipi wewe mwenyewe unapokuwa katika hali mbaya?

Tunajua kwamba matumaini yetu hayatakuwa ni ya kukatishwa tamaa, kwa sababu tayari tuna uzoefu wa upendo wa Mungu ndani ya mioyo yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Kwenye Waefeso 1:13-14, Paulo alisema kwamba Roho Mtakatifu ni dhamana ambayo Mungu atatumia katika kukamilisha kitu kingine chochote alichoahidi. Roho Mtakatifu ni kama amana ya mkataba.

5:6-10 inaweka msisitizo kwamba wakati wa kuhesabiwa kwetu haki hatukuwa tunastahili na hatungeweza kufanya lolote kukamilisha hilo. Tulikuwa hatuna nguvu, tulikuwa tungali wenye dhambi, na tulikuwa maadui.

(5:6) Kuwa bila nguvu inamaanisha kwamba ni kukosa uwezo wa kujiokoa wenyewe, hasa kwa kutimiza matakwa ya sheria. Tulikuwa hatuna nguvu ya kutimiza matakwa ya Mungu au kujikomboa wenyewe kutoka katika dhambi.

(5:7-8) Ni mara chache sana kwamba mtu anaweza kufa kwa ajili ya mtu mwingine mwema, lakini Kristo alikufa kwa ajili yetu wakati tukiwa wenye dhambi.

(5:9-10) Kristo anaishi kama mpatanishi na wakili wetu. Paulo anatoa sababu kwamba kama Mungu alikuwa tayari kusamehe wakati tulipokuwa wenye dhambi, basi tunaweza kuwa na uhakika hata na zaidi sana kuhusiana na upendeleo wake ambao sasa tunahesabiwa haki kwa njia ya Kristo. Tulipatanishwa kwa kifo chake kwa ajili yetu na kuendelea kukubaliwa na Mungu kwa njia ya kuunganishwa na Kristo aliye hai.

(Sehemu ifuatayo ni muhimu kwa ajili ya 5:12-19.)

Je, sisi ni wenye hatia kwa dhambi ya Adamu?

► Je, sisi ni wenye hatia kwa dhambi ya Adamu? Elezea jibu lako.

Katika Warumi 5:12-19 panasema kwamba watu wote waliingizwa katika hali ya dhambi na kifo kwa sababu ya dhambi ya Adamu. Je, sisi binafsi tunayo hatia kwa dhambi ya Adamu? Je, wenye dhambi wataadhibiwa kwa dhambi ya Adamu?

Paulo hajasema kwamba wenye dhambi wataadhibiwa kwa dhambi ya Adamu. Katika 5:12 alisema kwamba mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi. Kila mtu kwa nafsi yake ni mwenye hatia kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe. Warumi 1-2

tayari ilishatoa msisitizo kwamba watu wanahitaji kuhesabiwa haki kwa sababu ni wenye dhambi ambao wamevunja sheria ya Mungu. Watu hawahukumiwi kwa ajili ya hali waliyozaliwa nayo, bali kwa ajili ya chaguo lao la kutenda dhambi. Hukumu inatokana na matendo (Ufunuo 20:12, Warumi 2:6-16, 2 Wakorintho 5:10).

Hata hivyo, kwa Adamu dhambi iliingia ulimwenguni. Kama baba wa wanadamu wote ambao walikuwa bado hawajazaliwa, alitenganisha wanadamu na Mungu. Watu wote baadaye wakawa wanazaliwa wakiwa tayari wametengwa na Mungu na, kwahiyo, kukasababisha uasi. Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, watu wote huwa wanazaliwa wakiwa na tabia ya kutenda dhambi na wote kwa pamoja wameifuata kwa kutenda matendo ya dhambi.

Taarifa zifuatazo zinaweza zikatafsiriwa katika ufahamu huo:

- Kwa kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa (5:15)
- Hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhabu (5:16)
- Kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala (5:17)
- Kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu (5:18)
- Kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi (5:19)

Paulo hakusema kwamba tuna hatia kwa dhambi ya Adamu; lakini Adamu aliileta dhambi, na kila mtu akafuata. Wenye dhambi wanahitaji kusamehewa kwa ajili ya makosa yao mengi (5:16) na siyo kwa ajili ya dhambi ya Adamu.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 3, kifungu cha 3

Mwendelezo wa maelezo ya Aya–kwa-Aya

(5:12) Sababu ya kifo kuenea kwa watu wote siyo kwamba kosa la Adamu liliingizwa kwao, bali ni kwa sababu wote wamefanya dhambi. Adamu ndiye aliyeleta dhambi duniani na alileta uvutano wa dhambi juu ya wazao wake.

(5:13-14) Dhambi haijafunuliwa na kuhukumiwa kwa uwazi bila sheria. Hata hivyo, hata hadi wakati Musa alipopokea sheria, kifo kilikuwa bado kinatawala. Watu walikuwa wanajua kwamba ni wenye hatia kwa ajili ya dhambi, hata bila ya ufafanuzi uliokuwa unatolewa na sheria (Ona 1:20). Uhalisia kamili wa kiwango cha dhambi unaoneshwa na sheria. Kosa kama la Adamu linarejelea kwenye kukosa utii kwa kudhamiria dhidi ya sheria iliyotolewa. Wale waliokuwa hawana ufahamu wowote hawakuwa na chaguo lililo wazi, lakini bado hawakufuata kikamilifu dhamira zao (1:21).

(5:15) Kitendo cha Adamu kilisababisha kifo kwa watu wengi na kazi ya Kristo ikaleta uzima kwa watu wengi. Neno "wengi" linarejelea kila mtu kwa ujumla. Msisitizo ni kwamba matokeo ya upatanisho wa Kristo ulikuwa unafika mbali kuliko dhambi ya Adamu. Aya hii inasema kwamba **kama vile dhambi ya Adamu ilivyosababisha kila mtu akawa mwenye dhambi, upatanisho wa Kristo unatoa neema kwa kila mtu**. Mungu hutoa neema kwa kila mtu aliyefanywa kuwa mwenye dhambi kutokana na anguko la Adamu.

► Kutoka katika aya ya 15, utawezaje kumjibu mtu anayefikiri kwamba Mungu alitoa wokovu tu kwa asilimia ndogo ya wanadamu?

(5:16) Dhambi ya asili ilikuwa ni kitendo kimoja tu, lakini neema inahitajika sasa kwa ajili ya dhambi nyingi. Neema ni lazima iwe juu zaidi kuliko dhambi ya asili.

(5:17-19) Watu wengi walifanywa watenda dhambi kutokana na madhara ya dhambi ya Adamu. Watafanywa tena wenye haki halisi na Kristo. Maana yake ni kwamba wamebadilishwa.

(5:20) Sheria inazidisha dhambi kwa mantiki kwamba inasababisha msururu mrefu wa makosa wakati ambapo hapo awali dhambi chache tu ndizo zilizokuwa zinatambuliwa. Sheria pia iliongeza dhambi kwa mantiki kwamba kama mtu atakuwa anaijua sheria na akaamua kuikataa, anakuwa ni mtenda dhambi mbaya zaidi kuliko alivyokuwa mwanzo. Hii ni hali inayoelezewa katika 7:5-24. Lakini neema imezidishwa juu sana kupita upeo wa dhambi zote.

Neema ya Kushangaza

John Newton alikuwa na mama wa Kikristo, lakini akaamua kuwa baharia na kapteni wa meli. Akawa mwenye dhambi sana. Aliitabika kwa hali ngumu zikizomkabili katika maisha yake. Alisalitiwa na marafiki zake, kwa muda wa kipindi fulani, akafanywa mtumwa. Wakati hali yake ilipoanza kuonesha ahueni, aliendelea katika dhambi na akasaidia kuharibu maisha ya wengi kwa biashara ya utumwa. Alikuwa ni kapteni wa meli ya watumwa kwa miaka mingi. Wakati fulani alivunjikiwa na meli yake katika kisiwa lakini aliokolewa na kapteni wa meli nyingine ambaye alikuwa rafiki wa baba yake. Alihisi kwamba Mungu alikuwa amemrehemu ingawa alikuwa mwovu. Baadaye ile meli ilikuwa katikati ya dhoruba kali ya mawimbi baharini; akamwita Mungu akiomba rehema. Ile meli ilinusurika na ile dhoruba, na Newton aliendelea kumtumainia Mungu kwa ajili ya rehema. Hatimaye aliachana na mambo ya bahari na kuwa Mchungaji. Mojawapo ya nyimbo alizoandika ni huu ulioimbwa sana na ambao umerekodiwa zaidi kuliko wimbo wowote wa Kikristo uliowahi kuandikwa, "Katika Neema ya Yesu."

Katika ushuhuda wake, Newton alisema, "Mungu kwa rehema zake amenitoa mimi kutoka katika dimbwi la matope na akaiweka miguu yangu juu ya mwamba, Yesu Kristo. Ameiokoa roho yangu. Na sasa, ni hamu ya moyo wangu kusifia sana, uhuru, ukuu wake na kuheshimu neema yake isiyolinganishwa na kitu chochote kwa sababu 'Kwa neema ya Mungu niko kama nilivyo' (1 Wakorintho 15:10). Ni furaha kuu ya moyo wangu ya kuuweka wokovu wangu kwenye neema ya Mungu." [34]

[34] "John Newton's Conversion," kutoka https://banneroftruth.org/us/resources/articles/2001/john-newtons-conversion/ (Ilifikiwa Desemba 29, 2022).

Maswali ya Mapitio Somo la 5

(1) Je, Mtu aliye na imani iokoayo anaamini nini?

(2) Je, ni tatizo gani lilitatuliwa na upatanisho?

(3) Ni jinsi gani upatanisho ulitatua tatizo?

(4) Je, kuhesabiwa haki ina maana gani?

(5) Je, ni kwa njia gani mtu anaiheshimu sheria kama kipimo cha kuhesabiwa haki?

(6) Je, ahadi ya Mungu ya neema kwa Abraham ilikuwa ni nini?

(7) Je, Daudi alisemaje kuhusu kuhesabiwa kwa imani?

(8) Je, nani ni watoto wa kiroho wa Ibraham?

(9) Tunajua nini kutoka katika Warumi 5:15 kwamba wokovu hutolewa kwa kila mmoja?

Kazi ya kufanya Somo la 5

Andika ukurasa mmoja kuhusu kuhesabiwa haki kwa njia ya imani pamoja na kutoa majibu kwa maswali yafuatayo: Je, ni tatizo gani linalotatuliwa na upatanisho? Je, ni kwa nini mwenye dhambi hawezi akaokolewa kwa kutii? Je, ni kwa jinsi gani Ibrahimu amedhihirisha kuhesabiwa haki kwa imani? Je, tunajuaje kwamba wokovu unapatikana kwa kila mtu?

Somo la 6
Ushindi dhidi ya Dhambi

Dhambi

Warumi 6 inahusu ukombozi kutokana na nguvu ya dhambi. Ili tuweze kuelewa toba na ushindi, ni lazima tuelewe dhambi ni nini.

► Dhambi ni nini?

Kwa kawaida Biblia huzungumzia kuhusu matendo ya dhambi kama yanayofanywa kwa hiari (1 Yohane 3:4-9, Yakobo 4:17). Wakati mtu anapofanya kwa kukusudia na kwa kujua akachagua kutokumtii Mungu, hiyo ni dhambi ya kujitakia au hiari.

Kuna utendaji wa bila kufahamu au ukiukaji wa bahati mbaya wa sheria ya Mungu hauvunji sheria au uhusiano na Mungu kama dhambi ya kukusudia inavyofanya. Tunapokuwa tunatembea kwenye nuru (tukiishi kulingana na ukweli tunaoujua), tunatakaswa na aina zote za dhambi (1 Yohane 1:7) na haihitajiki kuwa kwenye mashaka kwamba ukiukaji unaofanyika kwa bahati mbaya utatutenganisha na Mungu.

Kimsingi kifungu hiki kinazungumzia kuhusu dhambi za kujitakia au za hiari, ambazo huharibu Imani na kuleta madhara katika uhusiano wa mtu na.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 4, kifungu cha 1

Sehemu ya 4 ya Warumi (Warumi 6-8) inahusu utakaso wa wale waliohesabiwa haki.

Hadi kufikia hatua hii, Paulo alikuwa anazungumzia kuhusu haki iliyoingizwa ndani. Haki hii inaingizwa kwa neema wakati wa kuhesabiwa haki na ina maana kuwa mwamini anakuwa mwenye haki kweli kwa kuwa huru kutoka nguvu za dhambi na anasaidiwa na Roho Makatifu kuishi maisha matakatifu. Kwa hiyo, Mwamini sio tu anahesabiwa kuwa mtakatifu, lakini anafanywa kuwa mtakatifu haswa. Hii huitwa utakaso.

Kwenye somo hili tutajifunza Warumi 6, ambayo ni ushindi dhidi ya dhambi.

Jambo Kuu katika sura ya 6

Mtu aliyeamini yuko huru kutokana na utumwa wa dhambi na ni lazima achague kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi na kwa utii kwa Mungu, asije akarudia tena kuwa chini ya udhibiti wa dhambi.

Muhtasari wa sura ya 6

Warumi 6 ni majibu ya Paulo kwa dhana potofu waliyonayo watu: dhana potofu ni kwamba kwasababu ya neema, waamini hawahitaji kuishi katika utii wa sheria za Mungu. Kosa hili

linatokana na uelewa mbaya wa neema. Paulo anasahihisha kosa hili kwa kuuliza na kujibu maswali mawili yanayodhaniwa (6:1,15).

Baadhi ya watu wanaposoma 5:20, wanafikiri kuwa wanapaswa kuendelea katika dhambi, ili kwamba tuwe na neema zaidi (6:1). Inaonekana wanafikiri kuwa, kwa kuwa kumbukumbu za dhambi zetu zimebadilishana na haki ya kupewa, basi haina shida kama tukiendelea kufanya dhambi.

Kuna sababu nyingine ambayo baadhi ya watu hufikiri kwamba waamini hawahitaji kuishi katika utii wa sheria za Mungu. Wanasema kuwa tumekubaliwa kwa neema na sio kwa matendo. Hii ni sababu inayowafanya kukosea kufikiri kuwa chochote tunachofanya hakuna shida (6:15).

Paulo anakataa kwa nguvu zote maswali ya dhana hizo. Anajibu kwa kutao ufanfanuzi kuonyesha kuwa ushindi dhidi ya dhambi ni muhimu.

► Mwanafunzi atapaswa asome Warumi 6 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(6:1) Hapa mtume aliuliza swali ambalo mtu anaweza akauliza baada ya kuwa ameshasikia kwamba neema ilikuwa nyingi zaidi kuliko dhambi. Mtu anaweza kufikiri kwamba dhambi kwa uhakika inaleta matokeo mazuri kwa sababu inaleta neema zaidi. Kwa wazo hili ni kuwa tuko huru kuishi kiholela katika dhambi.

(6:2) Mtume anatoa majibu ya swali hilo kwa namna ya kukasirika. Kisha analitolea ufafanuzi kwamba haiwezekani tena sisi tuendelee kuishi kwenye dhambi, kwa sababu tayari tulishaifia dhambi.

(6:3-5) Hatuendelei kuwa kwenye dhambi kwa sababu tumeunganishwa pamoja na Kristo katika mfano wa mauti yake na kufufuka kwake. Kama Warumi 5:15-19 inavyoeleza, Yesu alikamilisha kazi ya ukombozi kwa ajili yetu sisi sote. Kwa imani tunaunganishwa pamoja naye, ili kwamba upendeleo wa Mungu uweze kuendelezwa kwetu kama ilivyo kwa Kristo.

Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi mara moja tu, na kisha anaishi kwa ajili ya Mungu. Kifo cha Yesu kilikuwa ni kwa ajili ya dhambi zetu na siyo kwa ajili yake mwenyewe, lakini jambo muhimu hapa ni kwamba suala la dhambi lilifikishwa mwisho. Kwa imani, tumekufa na kufufuka pamoja na Kristo; ili kwamba na sisi pia tuwe tumefikia mwisho wa kuishi dhambi.

Ubatizo ni tendo la kuonyesha kifo cha Yesu na kufufuka kwake, ikiashiria ushiriki wetu katika hayo.

(6:6) Utu wa kale unawakilisha hali na maisha ya dhambi kabla ya kuokoka. (Sehemu nyingine ya baadaye katika somo hili inaelezea dhana ya "Utu wa Kale") Maisha ya dhambi yamemalizwa kabisa, kwahiyo sisi siyo watumwa wa kutumikia dhambi tena.

Tambua maneno yaliyotumika katika kifungu hiki kuhusiana na kile kilichofanyika dhidi ya dhambi: imekufa, ilisulubiwa, na iliharibiwa. Maneno yanaunganisha ushindi kamili dhidi au juu ya dhambi.

(6:7-11) Msisitizo katika aya hizi ni kwamba udhibiti wa dhambi umekwisha kwa mtu aliyeamini. Kielelezo hapa ni kifo. Mtu aliye mfu yuko ameshida dhambi, na tunapaswa tuwe na uzoefu wa kiroho ambao unafanana na kifo.

Baada ya kufufuka, Yesu hakufa tena na hataendelea kufa tena. Alimalizana na kifo. Tunapaswa tufe kabisa juu ya dhambi na kumalizana nazo na kisha tuwe huru dhidi ya hiyo dhambi. Kifo katika dhambi ni suala la kumalizika kwa haraka, kisha tunaendelea kuishi kwa ajili ya Mungu.

Muunganiko wa Mkristo na kifo cha Kristo kwa dhambi, kuzikwa kwake, na baadaye kufufuka ambako Paulo alielezea katika Warumi 6:1-23 kunamweka Mkristo huru kutokana na nguvu na utumwa wa dhambi. Anakuwa ametangazwa kuwa mfu katika dhambi (Warumi 6:2) na kuwekwa huru kutokana nayo (Warumi 6:7). Kuwa mfu katika dhambi ni kutokuwa tena chini ya nguvu za dhambi au kuthibitiwa nayo. Kwa Imani mwamini lazima kujifikiria kuwa mfu katika dhambi, lakini aliye hai kwa Mungu katika Yesu Kristo. (Warumi 6:11). Hii inamaanisha kwamba Mkristo anapaswa awe na uzoefu wake binafsi katika kile ambacho Mungu anatangaza kwamba ni cha ukweli kuhusiana na yeye. Hapaswi kutoa mwanya kwa dhambi kuendelea kutawala tena ndani ya mwili wake (Warumi 6:12), au kuvitoa viungo vya mwili wake kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi (Warumi 6:13a). Badala yake, anapaswa ajitoe mwenyewe kama dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu (Warumi 12:1), na kuvitumia viungo vya mwili wake kuwa silaha za haki. (Warumi 6:13, 19).[35]

Katika Warumi 6:11 neno "Hesabu" ni neno la uhasibu. Ni kuthibitisha kitu ambacho ni cha ukweli. Siyo tamko la kujifanya. Mtume hawaelezi waamini waseme kitu ambacho siyo cha ukweli. Mtu aliyeamini anapaswa atambue kwamba amekombolewa kabisa kutokana na dhambi kama kwamba amekufa, na anapaswa achague kuishi kwenye uhuru kamili dhidi ya nguvu ya dhambi.

► Je, inamaanisha nini kujihesabu umekufa katika dhambi?

Sehemu iliyobakia ya sura hii inaelezea sababu nyingine kwamba ushindi dhidi ya dhambi ni jambo muhimu. Sisi siyo watumwa wa kufanya dhambi, bali watumishi wa Mungu. Huwezi kutumikia dhambi na Mungu kwa wakati mmoja. Ulipokuwa mtumishi wa dhambi, hukufanya uadilifu (6:20). Kwa sasa uko huru na dhambi na ni mtumishi wa Mungu; kwa hiyo, unaishi katika utakatifu (6:22).

(6:12-13) Hapa tunaona ulinganifu. Kama hatuwezi kuwa na ushindi dhidi ya dhambi, dhambi itatutawala. Waamini hawatawaliwi na tamaa za dhambi. Kutumia mwili wako kwa

[35] Kifungu hiki kimeandikwa na Dr. Allan Brown.

ajili ya matendo ya uovu ni sawa na kuutoa uwe kwenye mamlaka ya dhambi. Badala yake, mwili wako ni mali ya Mungu na unapaswa utumike kwa ajili yake.

(6:14) **Kuwa chini ya sheria ina maana kuwa unategemea kuitii sheria ili ukubaliwe na Mungu.** Mtu huyo hana neema inayookoa, kwa hiyo, anahukumiwa katika misingi ya matendo. Kwa kuwa hakuna mtu yeyote asiye na neema anaweza kuishi kwa kuishinda dhambi, kuwa chini ya sheria ina maana umehukumiwa na uko chini ya nguvu ya dhambi. **Kuwa chini ya neema ina maana kuwa unategemea neema ili kukubaliwa na Mungu**. Mtu aliye chini ya neema hayuko chini ya nguvu ya dhambi. Aidha Kuwa chini ya sheria au chini ya neema haisemi ni Agano la Kale au Agano Jipya.

► Watake wanafunzi waelezee tena inamaanisha nini kuwa chini ya sheria.

(6:15) Hapa mtume aliuliza swali ambalo mtu anaweza kuuliza baada ya kusikia kwamba hatuko chini ya sheria: "Je, tunaweza kutenda dhambi, kwa sababu hatuko chini ya sheria?" Mtu anafikiri kwamba kama kukubaliwa kwetu mbele za Mungu sio kwa utii wetu basi utiifu si wa muhimu. Paulo anajibu swali hili kwa uzito mkubwa.

Jeshi la Kirumi lilikuwa ni bora uliko wengine katika mafunzo yake, lilikuwa na nidhamu, navifaa. Katika Waefeso 6:13-17, Paulo alitumia silaha ya Kirumi kama mfano wa vita vya kiroho.

Paulo hakuelezea moja kwa moja ni kwa nini neema haifuniki dhambi zinazoendelea kufanywa. Badala yake anaelezea kwamba mtu hawezi kuwa mtumishi wa Mungu kama yuko chini ya nguvu ya dhambi.

(6:16) Haiwezekani kutumikia kwa pamoja Mungu na dhambi kwa sababu wewe ni mtumishi kwa yule unayemtii. Kama utaitii dhambi, dhambi ndiyo bwana wako; ikiwa na maana kwamba Mungu siyo Bwana wako. Kama mtume Petro alivyosema, kwamba mtu akishindwa na mtu basi aliyeshindwa huwa mtumwa wa mtu yule" (2 Peter 2:19). Huwezi ukajiachilia kwa dhambi bila ya kuwa mtumwa wa dhambi.[36]

(6:17-18) Waamini wamekombolewa kutoka katika nguvu ya dhambi na sasa wanaitumikia haki. Walipata ukombozi huu kwa kuitii injili. Pia, imeelezwa kwamba kuitumikia haki ilikuwa ni muhimu kwao kukombolewa kutokana na dhambi.

Sura yote inaelezea ulinganifu kati ya kifungo cha dhambi na kuishi ya maisha ushindi. Kamwe hakuna wazo kwamba inawezekana kwa mtu aliyeamini kuwa chini ya nguvu ya dhambi au kwa mwenye dhambi kuwa mwenye haki wakati anaendelea kutenda dhambi. Itakuwa ni vigumu kupata njia ambayo Paulo angeweza kusemea jambo hili kwa njia iliyo hakika zaidi.

[36] Picha kutoka Piqsels, imepatikana kutoka https://www.piqsels.com/en/public-domain-photo-sriuc.

(6:19) Alisema kwamba analisemea hili kwa jinsi ya kibinadamu ili kwamba waweze kulielewa. Hapo mwanzo walijiachilia kwa ajili ya kutumikia dhambi, ambako kuliwaingiza ndani zaidi katika kutenda dhambi. Sasa, wanapaswa wawe wenye haki katika matendo yao, jambo ambalo ni muhimu kwa ajili ya utakatifu. Mtu hawi mtakatifu kwa kutenda mambo ya haki, lakini pia siyo mtakatifu kama hatendi mambo ya haki.

► Je ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea isivyowezekana kumtumikia Mungu na kuishi katika dhambi kwa wakati mmoja?

(6:21-23) Dhambi haileti faida yeyote lakini yenyewe mwisho wake ni kifo. Mwenye dhambi huchuma mauti; kifo ni mshahara wa dhambi. Mwamini hapati uzima wa milele kwa kuufanyia kazi, lakini huupokea kama kipawa cha neema.

Msingi wa Uhakika Binafsi wa Wokovu

Wengine wanafikiri kuwa wakati mtu binafsi amemkubali Kristo wokovu wake uko salama bila matatizo hata wakati ambapo aina ya maisha yake yanajichanganya kabisa na anavyosema.[37] Hata wakati ambapo madai ya wokovu bado hayajaanza kutenda kazi katika kuleta mabadiliko ya maisha; hata wakati ambapo hakuna tunda la toba na kuokoka kunakoonekana; na hata wakati ambapo mtu anakataa kuwa mwanafunzi wa kweli wa Yesu, anaweza kuwa amekiri wokovu kwa kudanganya. Huu ni udanganyifu wa kiwango cha juu sana na unapingwa na maandiko mengi.

> Na tukaribie wenye **moyo wa kweli**, kwa **utimilifu wa imani**, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi (Waebrania 10:22).
>
> Nanyi **mnalindwa** na nguvu za Mungu **kwa njia ya imani** hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho (1 Petro 1:5).

Kutokana na vifungu hivi tunajifunza kwamba uhakika wa kibiblia wa wokovu unategemea **imani:**

- **Uhakika wa wokovu unategemea imani ambayo huelewa "uhakika kamili."** Uhakika huanza na ufahamu ulio wazi wa injili (1 Wakorintho 15:3-4). Haya ndiyo "maarifa kuhusiana na uhakika" ambayo yamezungumziwa pia katika Wakolosai 2:2. Wokovu ni kwa neema peke yake, kupitia imani iliyo katika kifo kilichochukua nafasi mbadala cha Yesu Kristo kwa niaba yetu (Waefeso 2:8-9). Hitaji la wokovu siyo ukamilifu usio na dhambi (hakuna mtu atakayestahili) au kujisikia umeokoka wakati wote, lakini afadhali kuaminika mara kwa mara katika sifa ya Kristo na kazi ya ukombozi iliyokamilishwa hata wakati tunapojikuta tumeanguka. Hamu ya kuwa mwaminifu itafuata imani inayookoa iliyo halisi.

[37] Sehemu hii iliandikwa na Tim Keep

- **Uhakika wa wokovu unategemea imani ya dhati – "moyo wa kweli."** Mtu aliyeokoka kwa dhati ni yule ambaye "ameoshwa kutokana na dhamiri ya uovu" (Waebrania 10:22). Hatia na aibu vimeondolewa na kubadilishwa kwa amani na upendo. Mtu aliyeokoka kwa dhati ni yule pia ambaye mwili wake "umetakaswa kwa maji yaliyo safi" kwa kuwa ya kale yamepita tazama, yamekuwa mapya (2 Wakorintho 5:17). Mtu aliyeokoka kwa dhati ni yule pia ambaye hukubali na huyakiri makosa yake na dhambi ili apate kusamehewa na kuwekwa huru (Mathayo 6:12, Yakobo 5:16).
- **Uhakika una masharti yake kwenye imani iliyo hai – "kwa nguvu za Mungu wanaongozwa kupitia imani"** maana yake ni kama vile ulinzi ulipo katika kasiri au ngome. Nguvu ya kiungu inalinda, inahifadhi, na mwisho wake itatuongoza kwenye ushindi. Ni nguvu ya utakaso inayotokana na damu ya Kristo na nguvu ya kufufuka kwake ambayo tunaipata kwa njia ya imani na kwamba inahifadhi roho zetu katika uzima wa milele. Imani peke ya kweli inayookoa; imani ambayo inaendelea katika Kristo na katika kazi yake aliyoikamilisha msalabani. Imani siyo kazi, ni sharti kwa ajili ya wokovu. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anasema hivi: "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza" (Waebrania 11:6).

Watu wengi wanaamini kwamba kufungamanisha masharti yeyote kwenye wokovu ni kushika sheria, lakini Yesu na kila mwandishi kwenye Agano Jipya kwa uwazi kabisa walifundisha kuhusu umuhimu wa imani endelevu.

> **Ninyi mkikaa** katika neno langu, mmekuwa **wanafunzi wangu kweli kweli** (Yohane 8:31).
>
> **Mkidumu tu katika ile imani**, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; **msipogeuzwa** na kuliacha tumaini la Injili… (Wakolosai 1:23).
>
> Lakini **mwenye haki wangu ataishi kwa imani**; Naye **akisita-sita**, roho yangu haina furaha naye (Waebrania 10:38).
>
> Uwe mwenye **imani** na dhamiri njema, ambayo wengine **wameisukumia mbali, wakaangamia** (1 Timotheo 1:19).

Akielezea uhakika wa wokovu, John Wesley alisema,

> Faraja yangu haitegemei maoni yoyote, iwe muumini anaweza au hawezi kuanguka, wala haitegemei kumbukumbu ya chochote kilichofanyika ndani yangu jana; bali inategemea kile kilichopo leo, katika kumjua kwangu Mungu leo ndani ya Kristo, akinipatanisha na yeye mwenyewe; kwa sasa ninapoona nuru ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo; nikitembea katika nuru kama yeye alivyo katika nuru, na kuwa na ushirika na Baba na Mwana. Faraja yangu ni kwamba kwa neema ninaweza

kumwamini Bwana Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu anashuhudia pamoja na roho yangu kwamba mimi ni mtoto wa Mungu.[38]

► Kutokana na dhana zilizoko katika sehemu iliyotangulia, nawezaje kuelezea kwamba Mkristo anaweza kuwa na uhakika wa wokovu ulio katika msingi wa imani iliyo hai?

Utu wa Kale

Neno *utu wa kale* limejitokeza mara tatu katika nyaraka. Kwa mara zote tatu linatumiwa na Paulo. Kwa kulinganisha haya matukio matatu katika muktadha wake tunaweza tukaona neno hili linamaanisha nini.

Wakolosai 3:9

Wakolosai 3:9-10a panasema," "Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, …" Paulo alisema kwamba waamini hawa walikuwa tayari wameshauvua utu wa kale. Hakuwa amemaanisha kwamba walikuwa tayari wameshatakaswa kabisa, kwa sababu mengi yaliyoko katika Wakolosai 3 ni wito kwao kwa ajili ya utakatifu.

Mwanzoni alikuwa amewaambia waamini wa Kolosai kwamba, "Yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko... Yafikirini yaliyo juu... Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu" (Wakolosai 3:1-3) Aliendelea kusema, "Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya..." (3:5). 3:6 inasema dhambi kama hizo zitaleta hukumu ya Mungu, na 3:7 inasema kwamba waamini hawa hapo nyuma walifanya mambo haya. Paulo anadai kuwa hawavumilii mambo kama hayo katika maisha yao kabisa. Hii inaoneshwa katika maelezo kuwa wanapaswa kufisha vitu vyote hivi.

Kisha, aliwataka wayaweke mbali yote yale: hasira, na ghadhabu, na uovu, na matusi vinywani mwao (3:8). Haya yote hayaendani na maisha katika Kristo.

Kisha tunakuja kwenye taarifa kwamba wanapaswa wayafanye haya yote kwa sababu tayari walishauweka nje utu wa kale pamoja na matendo yake yote.

Anawataka kuendelea katika imani ya kikikristo kwa kuelezea tabia ya utakatifu (3:12), kisha kwa kuhimiza kufanana na Kristo katika mahusiano (3:13), kisha akawaeleza wawe na upendo, ambao hufunga kila kitu pamoja katika ukamilifu (3:14).

Inaonekana wazi kwamba katika muktadha huu utu wa kale ulikuwa ni maisha ya kale yaliyoachwa wakati wa kuokoka. Kwa kuwa walishafanya hivyo, Paulo aliamini kwamba wanaweza wakaendelea kukamilika kabisa kwenye utakatifu.

---

[38] John Wesley, "Serious Thoughts Upon the Perseverance of the Saints", in *The Works of John Wesley: Letters, Essays, Dialogs and Addresses Vol. X*, (Grand Rapids, MI: Zondervan) 295. Pia inapatikana mtandaoni kupitia: https://archive.org/details/worksofjohnwesle0010wesl/

Waefeso 4:22

Mstari huu uko kwenye kifungu ambacho kinaenda sambamba na kifungu kingine kilichoko katika Wakolosai. Katika 4:17-19, anaelezea mfumo wa maisha ya Wamataifa; kisha kwenye 4:20 akalinganisha na maisha ya mtu aliyeamini. 4:21-24 zinaelezea inamaanisha nini kuwa "umejifunza Kristo" (4:20) na kuwa umemsikia na kufundishwa katika yeye (4:21). Mambo haya yote yanahusisha kuachana na utu wa kale na kuvaa utu mpya. Hii ni sehemu ya kile kilichokuwa kimetokea wakati walipookoka.

Kifungu hiki katika Waefeso kinafuata mpangilio sawa na ulioko katika Wakolosai 3. Baada ya taarifa kwamba kuachana na utu wa kale ni sehemu ya injili waliyokuwa tayari wameshajifunza, agizo la kwanza la Paulo kwao ni kwamba waachane na uongo. Akaendelea kutaja uchungu wote na ghadhabu, hasira, kelele, matukano pamoja na kila namna ya ubaya. Aliwaagiza wawe wema na wenye kusamehe. Mambo haya yote pia yametajwa katika Wakolosai baada ya maelezo kwamba walishaachana na utu wa kale.

Utu wa kale siyo kitu ambacho mtu aliyeamini anahitaji kuachana nacho, bali ni kitu ambacho kiliondoka wakati ule wa kuamini na kuokoka. Walikuwa bado hawajawa watakatifu kabisa, na Paulo aliwataka wakamilishe utakatifu wao katika maisha yao ambao utakuwa sawa na mwanzo waliokuwa wameuanzisha wakati walipoachana na utu wa kale.

Warumi 6:6

Katika kifungu hiki Paulo anaonyesha tofauti kubwa iliyopo kati ya mwenye dhambi na mtu aliyeamini. Jambo kuu katika sura hii ni kuwathibitishia mfuasi wa Yesu kuwa anayo ushindi dhidi ya dhambi. Moja ya sababu alizitoa kuthibitisha kwamba mtu aliyeamini anaweza kuishi maisha yenye ushindi dhidi ya dhambi ni kwamba utu wa kale umesulibiwa. "mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena." Hapa ni wazi anasema kwamba mtu aliyeamini yuko huru mbali na dhambi kwa sababu ya kile kitu ambacho tayari kilishatendeka wakati wa kuamini na kuokoka.

Hitimisho

Kwa hiyo neno *utu wa kale* linamaanisha nini? Utu wa kale ni maisha ya kibinafsi ya dhambi ambayo mwenye dhambi anaachana nayo wakati anapokuwa ameamini na kuokoka.

Mtu mpya anapookoka anakuwa bado ana tabia na mwenendo ambavyo ni sawa zaidi na utu wa kale kuliko utu mpya. Hii ndio maana Paulo aliwaambia waamini kuendelea kufanya matengenezo katika maisha yao ambayo yatakwenda sawa na kule kuukataa utu wa kale. Alikuwa anasema, "Kwa kuwa umeachana na maisha ya zamani ya dhambi, unahitajika uachane na tabia yeyote ambayo haiendani na maisha mapya ya haki."

Kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya Utakaso wetu.

Katika Warumi 6:1-10 tunaelezwa kuhusu kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya Utakaso wetu binafsi.[39] Tulipokuwa tumezaliwa mara ya pili, tuliwekwa ndani ya Kristo. Kile chote alichokifia na kufufuka tena ili kukikamilisha kilifanyika chetu katika yake. Hii inamaanisha kwamba katika Kristo tunavyo rasilimali ya ushindi kamili dhidi au juu ya dhambi.

Kwa sababu ya muunganiko wetu na Kristo, lolote lililotokea kwake lilikuwa limetokea pia kwangu. Alipokufa, na mimi nilikufa. Alipofufuka, na mimi nilifufuka ndani yake. Kwa sababu ya muunganiko huu ulio hai pamoja na Kristo, mtu aliyeamini ana uhusiano mpya kabisa katika dhambi. Kwa sasa tumekufa kwa dhambi. Tumekufa kwa pamoja kwenye matendo ya dhambi pamoja na kanuni ya dhambi. Huu ndio msimamo wa uhusiano wetu katika dhambi.

Kutokana na muungano wetu na Kristo, kwa sasa tunatembea katika upya wa maisha kwa sababu tunashiriki maisha yake ya ufufuo.

Kutokana na muungano wetu na Kristo, kusulubishwa kwake kunakuwa ni kusulubishwa kwangu. Kwa kuwa kifo chake kulishinda nguvu ya dhambi, hatushikiliwa tena na nguvu zake katika maisha yetu.

Je, ni nini maana ya *kujihesabu*? (Warumi 6:11). Ni neno linalohusika na utunzaji wa mahesabu. Inamaanisha ni kujihesabu kwa kile ambacho ndicho. Neno la Kiyunani linatumika mara 11 kwenye Agano Jipya, ingawa katika vifungu tofauti imetafsiriwa katika maneno tofauti. "Kwa hapa inamaanisha kwamba ni "kutengwa kwa imani ya uhuru wa kutoka kwenye dhambi na muungano na Mungu uliotolewa katika upatanisho na kufufuka kwa Kristo."[40]. Kitenzi kinaonesha kuwa tunapaswa kuamini kile ambacho tayari kimeshakuwa kweli:tumekufa katika kufanya dhambi.

Je, inanipasa kufanya nini ili kuonesha kweli kwamba nimekufa kufanya dhambi na kuwa ninaishi katika Kristo Yesu? Kwa imani ninapokea Neno la Mungu kama Ukweli kwa ajili ya moyo wangu. Natangaza juu ya mamlaka ya neno la Mungu lililovuviwa na lisilo na makosa kwamba nimewekwa huru kutokana na dhambi zote na kufanywa kuwa hai kabisa kwa Mungu katika Kristo Yesu aliye Bwana wangu.

Kama mtumwa wa upendo na hiari wa Yesu Kristo, kwa hiari yangu mwenyewe ninaachana na tabia hizo na matendo yote ambayo yalikuwa ni sifa bainifu za matendo ya zamani. Kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu ni furaha! Na kwa matokeo ya uhusiano wangu na Kristo, ninayo maisha ya milele.

---

[39] Sehemu hii imetoka kwa Dr. Allan Brown.
[40] W.T. Purkiser, *Exploring Christian Holiness, (Volume 1)*, 138

Hitimisho

Tumeshaona kwamba ni heshima yetu iliyonunuliwa kwa damu kuwa na uhuru kutokana na nguvu ya kutawaliwa na dhambi. Lakini zaidi y hapo, ni agizo la Mungu kwamba tuwe washindi.

Pengine huko nyuma hujaweza kutambua huu ukweli. Mungu amekuokoa wewe na unatembea katika upya wa maisha; lakini unakuta kwamba dhambi bado inazidi kujitokeza katika maisha yako. Hupendi iwe hivyo! Lakini ndani yako kuna kitu ambacho kinataka kufanya vitu kivyake. Kama hivi ndivyo, fuata agizo la Paulo la *kujihesabu* mwenyewe kuwa umekufa kabisa kwa dhambi (6:11) na kujitoa mwenyewe kwa Mungu (6:13).

> "Tunaposoma Warumi 6-8 tutagundua kwmaba hali ya kuishji kawaida maisha ya kikristo yana sehemu nne. Nayo ni (1) kujua, (2) kujihesabu, (3) kujiweka nafsi zetu kwa Mungu, na (4) kutembea katika roho , na yamepangwa katika utaratibu huo."
>
> - Watchman Nee, *The Normal Christian Life*

Mkabidhi yeye udhibiti wote! Kama utafanya hivyo, anaahidi kukuwezeshakuishi maisha huru kutoka nguvu ya udhibiti wa dhambi. Amini kile Mungu anachosema na udai kwa imani uhuru wako wa kutoka katika dhambi.

► Je, inamaanisha nini kuungana na Kristo? Je, ni nini utegemee kwenye maisha yako kwa sababu umeunganika na Kristo?

Jinsi ya Kuishi Maisha ya Ushindi

Je, ulishawahi kujiuliza kama kweli inawezekana kuishi kwa ushindi kabisa dhidi ya dhambi? Mungu ameahidi kutuwezesha neema ambayo ni zaidi ya fidia kwa madhaifu yetu katika majaribu:

> Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili (1 Wakorintho 10:13).

Aya hii inatuelezea mambo mengi muhimu:

1. **Kila jaribu ni jambo la kawaida kwa mwanadamu.** Linatokea kwa sababu ya ubinadamu wetu na linalenga kwenye madhaifu kadhaa ya kibinadamu. Hii ina maana kwamba mapambano yako siyo ya kipekee kwako.

2. **Mungu anajua mipaka yetu.** Anajua ni kwa jinsi tunaweza kuwa na uvumilivu. Hatujui kwa uhakika ni kwa jinsi tunaweza tukavumilia, lakini yeye anajua.

3. **Mungu huweka mipaka ya majaribu yanayokuja kwetu kwa sababu anataka tuishi kwa ushindi.** Watu wengine wanadhania kwamba majaribu mara nyingi yatakuwa juu ya uwezo wetu kwa sababu sisi ni wanadamu. Wanadhani kwamba haiwezekani kuwa na ushindi wa kudumu, lakini kwa mujibu wa aya hii sivyo ilivyo.

4. **Mungu hutoa kile ambacho tunahitaji kwa ajili ya kuishi kwa ushindi.** Hufanya njia ya kutokea.

Kwa hiyo hitimisho ambalo tunaweza kulipata kutoka katika aya hii ni kwamba Mungu anatukusudia tuishi maisha ya uhuru. Neema kwa ajili ya maisha ya ushindi hutolewa kwa kuitikia imani.

> Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu (1 Yohane 5:4).
>
> Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao (Yakobo 1:12).

Kama tutaelewa imetokeaje kwamba waamini wameshindwa na majaribu, inawezekana tukaelewa pia na jinsi ya kuzuia. Mtu anayeangukia kwenye majaribu kwa kawaida amejiruhusu yeye mwenyewe kupitia katika mchakato fulani.

Mchakato huo umeelezwa katika Yakobo 1:14-15: "Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti…"

John Wesley aliona kwamba hatua za kutenda dhambi kwa hiari kwa kawaida hufanyika kama ifuatavyo:

1. Jaribu hujitokeza (kutoka katika dunia, mwili, au Shetani).
2. Roho Mtakatifu humonya mtu aliyeamini awe mwangalifu.
3. Mtu huweka usikivu wake kwenye jaribu na mvuto wake huongezeka. (Kwenye mchakato huu, hapa ndipo mtu anapofanya kosa lake la kwanza.)
4. Roho Mtakatifu huhuzunishwa, imani ya mtu hufifishwa, na upendo wake kwa Mungu unakuwa baridi.
5. Roho Mtakatifu hukemea na kusahihisha kwa uchungu.
6. Mtu hugeuka katika kusikiliza sauti yenye maumivu ya Roho Mtakatifu na kuanza kusikiliza sauti ya kuvutia kutoka kwa mjaribu.
7. Matamanio ya uovu huanza na kuujaza moyo wake; imani na upendo hutoweka; na yuko tayari kufanya dhambi ya wazi.

Hatupaswi tudhanie kwamba uzoefu wa kila mtu kwenye kutenda dhambi siku zote utakuwa unafanana na mpangilio huu. Mara nyingine watu hujitoa kwa ghafla kutenda dhambi hata bila kufuata mchakato wowote.

Kwa kuwa jaribu huongezeka nguvu yake wakati tukiwa tunashikilia usikivu wetu, mtu aliyeamini ambaye yuko makini katika kuimarisha ushindi wake dhidi ya dhambi ni lazima auimarishe moyo wake ili aweze kulikataa jaribu mara moja. Mtu anayetambua kwamba

jaribu linampeleka kwenye kufanya dhambi lakini akasita kulizuia linamweka kwenye hatari kubwa zaidi. Kwa kusitasita, anajidhihirisha kwamba moyo wake haujaamua kwa ukamilifu kumpendeza Mungu.

Jaribu ni changamoto kwa imani yetu, kwa kuwa linatupa sisi nafasi ya kuwa na shaka kwamba utii kwa Mungu ndiyo njia nzuri zaidi kwa wakati huo.

► Kama inaonekana kwamba mtu aliyeamini anashindwa kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi, je, kuna sababu gani katika hilo?

Inawezekana ikawa ni kwa sababu mojawapo ya matatizo yafuatayo:

1. Haoni kwamba Mungu anahitaji utii.
2. Haoni au haamini ahadi ya Mungu ya neema inayowezesha.
3. Hategemei neema ya Mungu inayowezesha badala yake anategemea nguvu zake mwenyewe.
4. Anamtumikia Mungu huku akiwa na chaguo la aina ya utii atakaouonesha badala ya utii kamili, na ambao hauna masharti.
5. Hajatafuta kwa neema kuwa na lengo moja la kufanya mapenzi ya Mungu (Wafilipi 3:13-15).
6. Hajadumisha nidhamu ya kiroho ambayo itampa nguvu ya imani ya kujenga uhusiano na Mungu.
7. Hatimizi uwajibikaji wake wa kiroho kwenye kanisa lake la mahali pamoja.
8. Mara kwa mara hatafakari neno la Mungu.
9. Haja zoeza hisia zake katika kusikia sauti ya Roho Mtakatifu katika maisha yake.

Watu watatu waliomba kazi ya udereva wa kumwendesha mwajiri wao. Yule wa kwanza, akitaka kumvutia mwajiri wake mtarajiwa, akasema, "Mimi ni dereva mwenye uwezo wa hali ya juu sana kiasi kwamba hata nikaendesha gari kwa mwendo wa kasi futi chache tu kutoka kwenye mteremko mkali wa mlima uliochongoka hutahitaji kuwa na wasiwasi." Yule wa pili naye hakutaka kupitwa na mwenzake, akasema, "Mimi ninaweza nikaendesha kwa mwendo wa kasi inchi chache tu kutoka kwenye mteremko mkali wa mlima uliochongoka bila kupita juu yake na hutahitaji kuwa na wasiwasi." Yule mwombaji wa tatu akasita, kisha akamwambia yule mwajiri, "mimi sitadiriki kuhatarisha maisha yako kwa kupita karibu na huo mteremko mkali wa mlima uliochongoka." Unadhani ni yupi katika hawa waombaji watatu aliyepata ajira?

Hatupaswi tuangalie ni kwa karibu kiasi gani tunaweza kufika kwenye jaribu. Mungu anataka atupe sisi miongozo ambayo itatuongoza kwenye maeneo ya madhaifu yetu.Tunapaswa

tujifunze ni mambo gani yenye madhara, kama vile baadhi ya burudani mbalimbali, na kukaa mbali na mambo hayo.

Kama mtu aliyeamini hajadumisha uhusiano wake na Mungu, anapaswa kwa haraka atubu na kurejeshwa tena kwa Mungu kupitia kwa wakili wetu Yesu Kristo (1 Yohane 2:1-2). Hapaswi angojee muda wowote ujao ambao anauona kwamba utakuwa ni mzuri kwake. Kama anataka kurejeshwa, Roho Mtakatifu atampa hiyo nia na kumrudisha alikotoka kwenye uhusiano wake na Mungu. Kama toba yake ni ya kweli, anaweza akarejeshwa mara moja.

Mungu tayari alishafanya uwekezaji mkubwa kwa ajili ya wokovu wetu, katika dhabihu ya Yesu. Hayuko tayari kuachilia huo uwekezaji alioufanya upotee bure kwa kushindwa kutupa sisi neema tunayoihitaji ili tuendelee mbele.

Kweli Tano za Kujua na Kuzidai

Ushindi dhidi ya matendo ya dhambi ni zoezi la kawaida la Mkristo kwa sababu amewekwa huru kutoka katika utumwa wa dhambi kwa kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu.[41] Kuendelea kukaa kwenye dhambi kunatokana na kupuuzia neema ya Mungu inayookoa, kushindwa kukaa kwenye muunganiko na Yesu, kushindwa kuendelea kujihesabia binafsi kwamba umekufa kwa dhambi na unaishi kwa Mungu na kushindwa kuwakilisha kikamilifu na kwa uamuzi wa dhati mwili wa mtu kwa Mungu kama chombo cha haki.

Kila mwamini wa kweli anatamani kuwa na uzoefu wa ushindi dhidi ya dhambi. Hii ni kwa sababu ya gharama kubwa Yesu aliyolipa ili kutukomboa kutokana na dhambi. Hii ni kwa sababu ya asili ya uharibifu ya dhambi. Jibu la Paulo kwa wale ambao wangehoji kwamba "Je, kwa kuwa neema inakua kwa ajili ya dhambi, kwa nini tusiendelee kutenda dhambi?" kunakoonekana kuwa na nguvu sana. "Hasha!" anasema (Warumi 6:1-2). Kwa mtu kuwa na tabia ya kizembe kuelekea ugonjwa wa dhambi kisa tu kwa sababu Mungu ameleta tiba kwa ajili ya hilo itakuwa ni sawasawa tu na kuwa mzembe kwenye ugonjwa wa UKIMWI na Kansa kisa tu kwa sababu tiba imegundulika. Tiba haiwezi kumsaidia mtu wakati wa maumivu au ugonjwa. Wala haiwezi kumwepusha mtu na makovu. Hakuna mtu mwenye akili timamu atakayeweza kusema, "Acha tuugue ili kwamba tuweze kupata tiba." Hakuna mtu aliyeona ubaya wa dhambi, makosa ya dhambi kwa Mungu mtakatifu, na gharama ya kutisha iliyolipwa kwa ajili ya kuondoa dhambi atakayesema, "Tutende dhambi kwa kuwa maana neema itazifunika zote!"

Uzoefu wa Mkristo wa uhuru kutokana na dhambi unategemea juu ya ufahamu wake (Warumi 6:3, 6, 9) na matumizi ya hizi kweli:

(1) Kama mwenye dhambi mimi nilikufa

"Utu wa kale" ambao mtu mtenda dhambi wa zamani kama tulivyokuwa, kiroho ulikufa pamoja na Kristo pale juu ya msalaba na alizikwa pamoja naye kwenye kaburi lake. Kwa

[41] Sehemu hii iliandikwa na Bwana Tim Keep.

kuwa mtu aliyekufa hawezi tena kutumika kama mtumwa, ubwana wa dhambi juu yetu umevunjika. Kifo hiki *tayari* kilishatokea. Kifo cha maisha yetu ya dhambi ya zamani kilifanyika mara tu tulipoamini katika kifo cha Kristo kwa ajili yetu, tulipotubu kwa ajili ya dhambi zetu, na tukapokea zawadi yake ya uzima wa milele.

Angalia maneno haya kutoka kitabu cha Warumi 6:

- "…**Sisi tulioifia** dhambi tutaishije tena katika dhambi?" (6:2).
- "…Sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu **tulibatizwa katika mauti yake**" (6:3).
- "**Basi tulizikwa pamoja naye** kwa njia ya ubatizo katika mauti yake…" (6:4).
- "Kwa maana kama mlivyounganika naye katika **mfano wa mauti yake**..." (6:5).
- "Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale **ulisulibishwa** pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena" (6:6).
- "Kwa kuwa yeye **aliyekufa** amehesabiwa haki mbali na dhambi" (6:7).

Tatizo lililoko kwa waamini wengi wakati wa sasa ni kwamba wanaishi chini ya uwezo wao. Waamini wengi wamejiweka kwenye hali ya kukubali kushindwa kama *jambo la kawaida*. Wanafikiri kwamba maisha ya ushindi kwa Mkristo ni jambo lisilowezekana na kwamba ni na kwamba wanategemea kuendelea kuishi katika dhambi. Waamini wengine wanafikiri kuwa hakuna kuvumilia kumvumilia anayeshindwa mtu lazima awe mkamilifu. Mafundisho haya pia ni uharibifu kwa imani na yameelekeza wengi aidha kwenye kukata tamaa au kuwa wanafiki. Paulo anaweka bayana kwamba ushindi ni wetu kupitia ushirikishwaji wa ushindi wa Kristo pale msalabani.

(2) Mungu amenifufua pamoja na Yesui li kuwa mtu mpya

Yesu alizishinda dhambi zote kupitia kufufuka kwake. Ni maisha ya ufufuko ambayo tumekuja kushirikishana kwa imani. Kwa imani, dhambi haina uwezo tena wa kutuweka chini, kutudhalilisha, kutujeruhi au kutuua sisi. Kiroho tulifufuliwa pamoja na Kristo kwenye maisha mapya ya ushindi.

- "…Kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi **tuenende katika upya wa uzima**" (6:4).
- "…Kadhalika mtaunganika kwa **mfano wa kufufuka kwake**" (6:5).
- "Tukijua ya kuwa **Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena**, wala mauti haimtawali tena" (6:9).
- "Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; **lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu**" (6:10).
- "Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na **walio hai kwa Mungu** katika Kristo Yesu" (6:11).

- "Jitoeni wenyewe kwa Mungu **kama walio hai baada ya kufa**…" (6:13).

(3) Nimeunganishwa kiroho na Yesu.

Siyo tu kwamba maisha yangu ya zamani yamesulubiwa pamoja naye, na siyo tu kwamba nimepokea maisha mapya kama yake; bali ninakaa ndani yake, na yeye ndani yangu! (Ona pia Wagalatia 2:20 na Yohane 14-16.) Hii ni ahadi iliyoahidiwa na Yesu kwa kila Mwanafunzi: kwamba Mungu amechchagua kukaa ndani ya waamini kwa njia ya Roho Mtakatifu. Muungano huu pamoja na kukaa ndani yetu ndicho kinachosababisha ushindi dhidi ya dhambi na kufanya iwezekane kuishi maisha matakatifu. Hii ndiyo inayofanya iwezekane kwa waamini kupokea kuishi kwa usafi, upendo, wenye huruma, wapole, wenye kusamehe na maisha matakatifu kwa ajili ya Yesu.

- "Kwa maana kama **mlivyounganika naye** katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake" (6:5).
- "…Utu wetu wa kale **ulisulibishwa pamoja naye**…" (6:6).
- "Lakini tukiwa **tulikufa pamoja na Kristo**, twaamini ya kuwa **tutaishi pamoja naye***"* (6:8).

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuhusu muungano huu katika Yohane 15. Fundisho la imani kuhusiana na muungano wa kiroho pamoja na Kristo ni muhimu kwa ajili ya mafanikio yetu katika maisha ya Kikristo!

(4) Ni lazima nimiliki kwa imani uhuru na ushindi Mungu aliotupa sisi.

> Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu (6:11).

Kujihesabia ni *kuhesabu* kama jambo hili ni kweli ili kwamba uweze kupata uzoefu katika maisha yako mwenyewe.

Hapa kuna kielelezo kutoka katika Agano la Kale ambacho kinaweza kuwa cha msaada. Tunakumbuka kwamba Mungu hakuwa tu amewaahidi Waisraeli ardhi yaani nchi ya Ahadi, bali pia alikuwa *amewapa hiyo* nchi muda mrefu hata kabla *hawajaimiliki* kiukweli. Kwa miaka arobaini walizunguka jangwani, wakiishi chini ya kiwango cha uwezo wao, kwa sababu walijiingiza katika hofu na walishindwa kumwamini Mungu. Lakini Mungu aliwapenda na akawaongoza kwenda kwenye urithi wao.

Katika Yoshua 1:3 panasomeka, "Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu, **nimewapa** ninyi, kama nilivyomwapia Musa." Kwenye aya nyingine za baadaye Mungu anaagiza, "Piteni katikati ya matuo, mkawaamuru hao watu, mkisema, 'Fanyeni tayari vyakula; kwa maana baada ya siku tatu mtavuka mto huu wa Yordani, ili kuingia na **kuimiliki nchi** awapayo Bwana, Mungu wenu, **mpate kuimiliki'"** (Yoshua 1:11).

Watu wa Mungu wanatakiwa, kwa imani, wamiliki nchi ambayo Mungu amewapa. Wakati ushindi juu ya wakazi wa kimwili wa Kaanani ulipotolewa, na kwa kila hali ikawa

umekamilika, Waisraeli walikuwa wauzoee ushindi huu kupitia imani ya utii. Waamini wa Agano Jipya hushinda kwa njia hiyo hiyo; kwa kujihesabia, kwa imani, kwa ushindi wa Yesu Kristo alioufanya kwa ajili yetu na kumiliki ahadi mbalimbali.

(5) Ni lazima niutoe mwili wangu kwa Mungu.

> Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake. Wala msiendelee **kuvitoa** viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali **jitoeni** wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki (Warumi 6:12-13).

Mapitio

► Wanafunzi mbalimbali watapaswa watoe ufafanuzi kuhusu umuhimu wa kweli tano zilizoko katika kifungu kilichotangulia.

> Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? (Warumi 8:32).
>
> Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu; Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina (Yuda 24-25).

Maswali ya Mapitio Somo la 6

(1) Je, kwa nini ni muhimu kuelewa dhambi ni nini?

(2) Je, maana ya dhambi ya kukusudia ni nini?

(3) Ni dhana gani potofu ambayo Paulo anaijibu katika Warumi 6?

(4) Je, kuifia dhambi ina maana gani?

(5) Je, ina maana gani kuwa chini ya neema?

(6) Je, kuwa chini ya sheria ina maana gani?

(7) Je, kwa nini ni haiwezekani kumtumikia Mungu na dhambi?

(8) Je, msemo wa utu wa kale maana yake ni nini?

Kazi ya kufanya Somo la 6

(1) Andika ukurasa mmoja ukielezea ni ushindi gani unaowezekana dhidi ya dhambi kwa mtu aliyeamini. Husisha pamoja na ufafanuzi wa dhambi ya hiari au kujitakia, na elezea kwa nini ufafanuzi wa dhambi ni muhimu. Jibu upinzani wa watu wanaotoa kuhusu uwezekano wa ushindi dhidi ya dhambi.

(2) Unahitajika kumalizia uwakilishaji wa mahubiri au masomo yako matatu.

Somo la 7
Mtenda Dhambi Mwenye Hatia

Je, ni sheria gani tunaizungumzia?

Maagizo mengi ya Agano la Kale yanaonekana kama hayataweza kutumika kwa watu wa wakati huu. Hapa kuna mifano:

- Usimwache mwanamke mchawi kuishi (Kutoka 22:18)
- Kila miaka saba, mwisho wake, fanya maachilio (Kumbukumbu la Torati 15:1-2).
- Siku saba mfanyie sikukuu Bwana pasaka katika Yerusalemu (Kumbukumbu la Torati 16:1-6).

Baadhi ya wanazuoni huzigawa sheria za Agano la Kale katika makundi matatu: sheria za ibada, sheria za kiraia, na, sheria za maadili

Sheria za ibada zilihusika na utoaji wa dhabihu, eneo la kuabudia, na taratibu za kuabudu. Wakristo wa wakati huu hawafuati sheria za ibada za kiyahudi kwa sababu utaratibu huo umetimilika katika kazi iliyofanywa na Kristo (Wakolosai 2:17, Waebrania 10:1).

Sheria za kiraia zilikuwa ni kwa ajili ya taifa la Israeli. Walitoa sheria kwa ajili ya shughuli za biashara, kulinda haki za binadamu, kutoa kanuni za utekelezaji wa sheria, na kulinda utambulisho wa kidini wa Israeli. Haiwezekani kwa Mkristo wa leo kufuata sheria za kiraia za wayahudi kwa sababu sheria hizo siyo sheria za taifa lao. Kwa mfano, nyakati za agano la Kale, wakati mtu alipotakiwa kuuawa kwa ajili ya kuabudu miungu, hilo halikufanyika kwa uamuzi wa mtu mmoja. Hakimu alisikiliza shauri lililokuwepo, kisha hukumu iliungwa mkono na watu (Kumbukumbu la Torati 17:6-12).

► Je kwa nini haiwezekani kwa Mkristo kutimiza sheria za kiraia za waisraeli wa kale katika hali zilivyokuwa mwanzoni?

Sheria za maadili zilitambua matendo kadhaa kwamba yalikuwa ni sahihi au ni mabaya kwa nyakati zote. Kwa mfano, Amri Kuu za Mungu zilizuia ibada za sanamu, kumkufuru Mungu, uzinzi na wizi (Kutoka 20:5, 7, 14, 15).

Ingawa wakristo hawafanyi kama zilivyokuwa mwanzoni, yaani matendo maalumu yalioamriwa kwenye sheria za ibada na sheria za kiraia. Walakini, sheria hizo bado zina umuhimu kwa sababu zinadhihirisha asili ya Mungu, ambazo kamwe hazibadiliki. Ingawaje hatuwaui watu wenye kufuata ibada za sanamu au wazinzi, sheria hizo zinatuonyesha kwamba dhambi hizo ni machukizo kwa Mungu. Ingawaje hatuachi ngano shambani kwa ajili ya maskini, tunajua kwamba ni lazima tuwajali maskini kwa vitendo. Ingawaje hatuwapeleki tena wanyama kwenye maeneo ya ibada kabla hatujawaua, tunajua kwamba kila kitu ni mali ya Mungu, na tunatakiwa tutoe sadaka kwa vile vitu tulivyo navyo. Kwa

hiyo, ingawaje hatuyafanyi kwa vitendo matendo ya zamani, tunapaswa tutafute matendo mapya ambayo yataweza kukamilisha kanuni hizo.

Sababu nyingine ya umhiumu wa sheria za ibada na sheria za kiraia ni kuwa zinatoa kanuni za maadili za kutumiwa katika njia maalumu. Kukataa hizo kanuni ingekuwa ni sawa na kuzikataa sheria za maadili. Kwa mfano, hatuhitaji kuwa na chuma za kuzunguka dari ya nyumba kama nyumba yetu haijakusudiwa kuwa na watu juu ya dari (Kumbukumbu la Torati 22:8). Lakini sheria hii ya zamani inatuambia kwamba tunapaswa tuzifanye nyumba na maeneo ya ardhi zetu visiwe na vitu vya hatari kwa watu.

► Je, kuna utaratibu gani wa wakati huu wa sasa ambao tunapaswa tufanye ili kukamilisha kanuni iliyopo katika Kumbukumbu la Torati 22:8?

Kwa hiyo, ni sheria gani ambayo Paulo anazungumzia katika kitabu cha Warumi? Ni mapenzi ya Mungu kwa wanadamu, yaliyoelezwa kwenye amri zake (Agano la Kale na Agano Jipya). Ingawaje baadhi ya amri hazikamilishwi katika hali yake ya mwanzoni iliyotakiwa, mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu kimsingi yanafanana. Ukiukwaji wa sheria ya Mungu ni dhambi (1 Yohane 3:4).

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 4, kifungu cha 2

Katika somo hili tunaendelea na sehemu ya 4 ya kitabu cha Warumi. Katika somo la mwisho tumejifunza Warumi 6, "Ushindi dhidi ya dhambi."

Katika somo hili tunaenda kujifunza Warumi 7, "Mwenye dhambi aliye na hatia." Warumi 6 na 8 zinalezea kuhusu maisha ya ushindi kwa mtu aliyeamini. Warumi 7 ina tofauti kubwa zaidi, ikionyesha maisha ya mwenye dhambi ambaye anajijua kabisa kwamba ni mwenye dhambi lakini mwenyewe hawezi kubadilika.

Jambo Kuu katika Warumi 7

Mtu anayeijua sheria ya Mungu lakini hajabadilishwa kwa neema hana msaada wa kukwepa nguvu ya dhambi na hukumu ya sheria.

Muhtasari wa Sura ya 7

Sura hii inaelezea hali ya mtu ambaye yuko chini ya sheria. Kuwa chini ya sheria maana yake ni kuwa umesimama mbele za Mungu ukingojea kuhukumiwa kwa msingi wa kutii sheria. Kwa kuwa wote wamefanya dhambi, kuwa chini ya sheria maana yake ni kuwa chini ya hukumu. Mtu ambaye yuko chini ya sheria bado hajahesabika kuwa mwenye haki.

7:1-6 zinafafanua jinsi ambavyo mtu aliyeamini amekufa katika sheria. Sehemu nyingine yote iliyobakia katika hii sura inaonesha ni kwa nini hili jambo ni muhimu (ona maneno "kwa maana" kwenye 7:5 na "bali sasa" kwenye 7:6). 7:7-13 zinaonyesha jinsi ambavyo sheria ni nzuri lakini inaifanya dhambi kuwa mbaya zaidi. 7:14-25 zinaonesha mwenye dhambi aliye na hatia na ambaye hajaokoka asivyoweza kujisaidia.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 7 kwa ajili ya kikundi

Maelezo ay Aya-kwa-Aya

(7:1-3) Aya hizi tatu zinaelezea kwa mifano jambo kuu lililoko katika aya nyingine tatu zinazofuata. Ndoa inaonyesha kufungwa kwetu kwa asili kwa sheria. Mwanamke hakuruhusiwi kuachana na mumewe akaolewe na mume mwingine, lakini kama mume wake akifa, yuko huru kutoka katika mamlaka yake. Wajibu huu wa sheria siyo tu kwa ajili ya Wayahudi chini ya sheria ya Musa, lakini ni kwa kila mtu, kwa sababu sisi wote tutahukumiwa kwa sheria ya Mungu kama tungekuwa hatujaokolewa kwa neema.[42]

Jambo kuu katika kielezo cha mfano cha Paulo kuhusiana na ndoa ni kwamba kifo hubatilisha uhusiano. Tulikufa katika maisha yetu ya zamani wakati tulipoungana na Kristo. Sheria haijabadilishwa au kufutwa. Hata hivyo, madai ya sheria juu yetu kama wavunja-sheria sasa yanalipwa kwa upatanisho mbadala wa Yesu. Kwa sasa sisi "tumeolewa" kwa Kristo. Hii haitufanyi sisi tuwe hatuna sheria. Hatuna haki ya kutufanya tuwe wavunja sheria wakati huu ambao sasa sisi ni wa Kristo. Badala yake, tumewezeshwa nguvu kupitia kwa Roho Mtakatifu, tunaishi katika roho wa sheria. [43]

(7:4) Ukiukaji wa sheria una adhabu ya kifo. Yesu alikufa badala yetu sisi. Tunajitambulisha na yeye, hivyo inaweza kusemwa kwamba tumekufa kufanya kwenye sheria kupitia mwili wa Kristo. Kwa kuwa mahitaji ya sheria yamekamilishwa, tuko huru dhidi ya kifungo chake. Hatuhitajiki tuitimize sheria katika hali ya kuhofia adhabu. **Kuwa umekufa kwa sheria hatuhitajiki kuitimiza kama njia ya kuhesabiwa haki, kwa sababu tumehesabiwa haki kwa njia ya neema.**

Ujenzi wa uwanja wa mduara ulianza mwaka wa 72 B.K. miaka michache baada ya ziara ya Paulo ya Rumi. Jumba hilo lingeweza kuchukua zaidi ya watazamaji 50,000. Maonyesho yalihusisha mapigano baina ya watu wawili wenye ujuzi wa kupigana, mapigano kati ya watu na wanyama (wakiwemo simba, dubu, na wengine wengi), na kuwauwa watu wengine kwa kutumia wapiganaji au wanyama. Mara nyingine mamia ya watu walikufa katika eneo hilo. Wakristo wengi walipelekwa katika huo Uwanja wa mduara kwa ajili ya kuuwawa.



[42] Picha: "Colosseum - Rome - Italy" ilipigwa na Sam Valadi, imepakiwa mnamo Machi 31, 2015, imepatikana kutoka https://www.flickr.com/photos/132084522@N05/16800139540/, imepewa leseni chini ya CC BY 2.0, imeshushwa rangi kutoka kwenye asili. Picha: "The Christian Martyrs' Last Prayer", na Jean-Léon Gérôme, kutoka Walters Art Museum, imepatikana kutoka https://commons.wikimedia.org/w/index.php?curid=18824108, mali ya umma.

[43] Kifungu hiki kimetolewa kutoka kwa Dr. Allan Brown.

(7:5) Dhambi husababishwa na sheria kwa maana kwamba sheria huandika kumbukumbu ya dhambi kwa maana kwamba wakati mtu anapokuwa ameijua sheria na akaamua kwenda kinyume chake, anakuwa mwenye dhambi mbaya zaidi.

Kufafanua neno Mwili

► Angalia rejea nyingi zilizoko katika sehemu hii ili kwamba waweze kuelewa dhana nyingi zilizopo.

Maandiko yanarejea watu kadhaa kama walioko "katika hali ya mwili. Kuwa katika hali ya mwili kunaweza kuwa na angalau maana mbili tofauti, kutegemeana na muktadha uliokusudiwa.

Maana ya msingi ni kuwa tu katika hali ya kibinadamu, ya kufa. Katika muktadha huu, Yesu alikuwa katika hali ya mwili (1 Timotheo 3:16, 1 Petro 3:18). Hata mtu anayeishi kwenye maisha matakatifu anaweza kusemwa kwamba yuko katika hali ya mwili kwa muktadha huu. (2 Wakorintho 10:3; Wagalatia 2:20; Wafilipi 1:22, 24). Kuwa katika hali ya mwili huchukuliwa kama ni kutopendelea upande wowote kiuadilifu wakati neno hili linapotumika kwa njia hii, kama wakati Paulo alipowaambia Wagalatia kwamba hawawezi katika hali ya mwili (jitihada za kibinadamu) kukamilisha kile ambacho neema imekianzisha.

Maana ya pili ambayo mtu anaweza kuwa katika hali ya mwili ni kutawaliwa katika anguko la hali ya asili ya dhambi. Hali hii inafanana na mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili. (Waefeso 2:3). Kazi za asili za anguko la asili zimeorodheshwa katika Wagalatia 5:19-21. Kwenye Warumi 8:1-13, katika hali ya mwili ni kuwa tofauti na kuokoka. Kuwa katika hali ya mwili ni kifo (8:6) na ni uadui na Mungu (8:7). Mtu aliyeko katika hali ya mwili hawezi kumpendeza Mungu (8:8) na atakufa (8:13). Ufafanuzi wa hali ya mwili ulioko kwenye muktadha huu ni sawasawa na hali inayoelezwa kwenye Warumi 7 (ona 7:5, 14, 18, 25). Mtu aliyeko katika hali ya nyama kwa muktadha huu anafanya matendo ya dhambi ambayo atapokea adhabu ya kiroho na kifo cha milele (Warumi 7:5). Mtu huyu bado hajaokoka.

Mtu bado anaweza akashawishiwa na anguko la asili hata baada ya kuwa ameokoka, ingawaje hatawaliwi nayo. Wakorintho waliitwa watu wa kimwili baada ya kuzaliwa upya (1 Wakorintho 3:1). Paulo alidokeza katika 3:1 kwamba kuwa katika hali ya kimwili ni jambo la kawaida kwa watoto wachanga katika Kristo, lakini mtu aliyeamini hapaswi aendelee kukaa au kubakia katika hali hiyo. Aliwashutumu Wakorintho kwa kuendelea kuwa watoto wachanga.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 4, kifungu cha 2

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(7:6) Kwa kuwa tumekufa katika sheria katika Kristo, vivyo hivyo sheria nayo kwetu imekufa. Kuwa huru haimaanishi kwamba hatutumiki tena; lakini sasa tunatumika kwa roho yetu kuliko kujaribu kutimiza yanayotakiwa bila ya kukamilisha makusudi yake.

(7:7) Hapo awali alikuwa amesema kwamba sheria hufanya dhambi kuongezeka. (5:20). Katika kifungu hiki alikuwa amesema kwamba dhambi hufanya kazi pamoja na sheria ili kuleta kifo (7:5). Kwa hiyo, ni jambo la kawaida kwamba, swali ni lazima litajitokeza hapa, "Je, sheria ni dhambi?" Anaonyesha kwamba sheria siyo dhambi kwa kuonyesha kwamba sheria ndiyo inayoihukumu dhambi.

(7:8) Sheria ya Mungu humuonesha mwenye dhambi kwamba matendo yake yamehukumiwa. Kwa namna kwamba, sheria hufanya dhambi ionekana mbaya. Mwenye dhambi anapoona kuwa ni mkosaji, dhambi zake anazoendelea nazo (kutokutii sheria ya Mungu) hapo huwa anajua hali yake ya uasi.

(7:9) Kabla ya kuwa ameona kile ambacho sheria ilikuwa inahitaji, hakuwa amejua kwamba amehukumiwa kifo. Lakini dhambi inasababisha kifo hata kwa wale wanaotenda dhambi bila kujua undani wa sheria ya Mungu (ona 2:12 na 5:14).

Katika Warumi 7:7-25 Paulo anatoa maelezo ya uzoefu wake kama Mfarisayo ambaye alikuwa hajaokoka na anafafanua jinsi alivyokuja kuona hitaji lake kwa ajili ya Kristo. Kwenye Warumi 7 anatuambia kwamba kabla Roho Mtakatifu hajafungua macho yake kutokana na ile tamaa aliyokuwa nayo ndani ya moyo wake, alifikiri kwamba alikuwa anaitunza sheria. Ona ushuhuda wake katika Wafilipi 3:6 wakati aliposema, "kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia." Kama alivyosema kwenye Wafilipi 3:9, kama Farisayo alifikiria anayo haki ambayo ilikuwa imetokana na sheria. Baada ya Roho Mtakatifu kumfungua macho yake kwenye tamaa aliyokuwa nayo katika moyo wake, alisema kwamba alijisikia aliyekuwa amekufa kiroho (Warumi 7:9). Hii kwa dhahiri ni taarifa ya kulinganisha: wakati mmoja alikuwa amejifikiria kwamba alikuwa hai kiroho kwa kuishika sheria; alipokuja kujiona alikuwa mwenye hatia kwa kuwa mwenye tamaa na kwa kutozishika sheria, alijitambua kwamba alikuwa amekufa. Paulo anaendelea kuelezea historia yake mwenyewe kwenye Warumi 7:14-25. Alijaribu kujizuia asiwe mwenye tamaa, lakini hakuweza. Ushuhuda wake wote ni mojawapo wa kushindwa kabisa na kuwa mtumwa wa dhambi. Anatuambia kwenye Warumi 7:25 kwamba ukombozi unapatikana peke yake kupitia kwa Yesu Kristo.[44]

(7:10) Sheria likuwa imekusudiwa kuonyesha njia ya maisha. Kamwe sheria haikuwa na njia ya wokovu, lakini ilikuwa iwe ndio mwongozo wa kuishi kwa ajili ya wale waliokuwa wanamjua Mungu. Lakini kwa kuwa mwanadamu aliyeanguka na wa tamaa hawezi kuifuata, inatokea kuwa ndiyo sababu ya kifo badala ya mwongozo kwa ajili ya maisha.

(7:11) Dhambi inadanganya kwa kuonekana kwamba ina faida, inapendeza, na isiyokuwa na madhara. Mtu anapotaka kujiingiza kwenye jaribu la kutenda dhambi, amehukumiwa, hata kama atafanikiwa katika kupunguza matokeo ya dhambi hiyo; kwa sababu hukumu ya Mungu ni kwa sheria, si kwa matokeo ya dhambi.[45]

---

[44] Aya hii iliandikwa na Dr. Allan Brown.
[45] Rejelea maelezo ya 3:5-7

(7:12) Sheria inafunua asili ya Mungu – sheria ni takatifu, yenye haki, na ni nzuri, kama yeye mwenyewe alivyo.

(7:13) Sheria siyo mbaya, lakini matokeo mabaya ya dhambi yalijitokeza wakati dhambi ilipoanza kwa na msuguano na sheria. Dhambi iliitumia sheria kumleta kila mtu kuwa chini ya adhabu ya dhambi. Kwa mujibu wa sheria, dhambi huthibitishwa kuwa kweli ni uovu.

Siyo picha ya Mtu aliyeamini

Watu wengi hufikiria kwamba Warumi 7:14-25 inamwelezea mtu aliyeamini wa kawaida, lakini tafakari maelezo yake.

Ameuzwa chini ya dhambi, kama mtumwa, ikimaanisha kwamba bado hajakombolewa (7:14). Anajua ni kitu gani kilicho sahihi lakini hawezi kukifanya (7:18). Ni mfungwa ambaye hajakombolewa (7:23). Anasumbuliwa na kulia kwa ajili ya ukombozi (7:24).

Katika 7:5-24, ukianzia na kifungu "tulipokuwa katika hali ya mwili" (7:5) na kumalizia na swali "Je, ni nani atakayeniokoa?" (7:24), hakuna kumbukumbu inayorejea kwa Kristo au Roho Mtakatifu, neema, maisha, au ushindi; lakini kuna kumbukumbu zipatazo 52 zinazohusiana na nafsi ya kwanza (mimi, yangu), kumbukumbu rejea 16 za sheria, na 15 zinazohusiana na dhambi.

Hii haiwezekani ikawa ni mtu ambaye ana ukombozi ulioelezwa katika Warumi 6. Sura hiyo, kwa kurudiarudia inasema kwamba mtu aliyeamini siyo mtumwa wa dhambi tena. Huyu ni mtu aliye chini ya sheria, kama ilivyotambulishwa kwenye mwanzo wa sura hii (7:1, 5-6). 7:14 ni kiunganishi kinachoonyesha kwamba sehemu ya sura iliyobakia inaelezea hali inayofanana na ile iliyoelezwa katika aya ya 7:1, 5-6.

Warumi 8:1 inasema kuwa mtu ambaye hajahukumiwa ni mtu aliyeko katika Kristo Yesu. 8:4-5 inasema kuwa mtu huyu hafuati mwili. Mtu aufuataye mwili (kama ilivyo katika 7:25 na 7:5) amehukumiwa. Mtu aliyehukumiwa sio mtu ambaye ni mwamini wa kweli. Mtu aliyeko katika Warumi 7 hana uwezo wa kujisaidia na anatawaliwa na mwili.

8:3 inasema kwamba hali ya udhaifu wa kuwa chini ya sheria umemalizika; kwa hiyo, hali ya kutoweza kujisaidia chini ya sheria katika Warumi 7 haipaswi iwe hali ya mtu aliyeamini.

8:6-7 panasema kwamba kuwa katika nia ya mwili ni mauti, na kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu. Lakini katika 7:14 anaanza kumwelezea mtu wa mwilini. Mtu wa mwilini, kama ilivyomaanisha katika dhana hii, siyo mtu aliyeokoka.[46]

Halafu ni kwa nini Paulo anajiweka mwenyewe kwenye maelezo haya? Kuanzia 7:7 na kuendelea, anamwelezea mwenye dhambi anayejikuta yuko chini ya hatia ya sheria. Sehemu nyingine ya sura iliyobakia inaelezea kuhusu uzoefu wake wa wakati uliopita – ni mapambano yake ya kumpendeza Mungu kwa kufuata sheria. Lakini haikumpa uzima na

[46] Ona kumbukumbu zilizoko katika 3:5-7.Kwa matumizi mengine ya neno mwili, ona mwangalizo hapo juu "unaofafanua kuhusu Nyama /Mwili."

haikumpa chochote cha kumridhisha. Katika Warumi 8 anaanza kwa kuelezea kuhusu maisha yake ya ushindi. Haiwezekani kwamba mtu aliyeelezewa kwenye 8:1-4 aendelee kuwa katika hali ya mtu wa Warumi 7.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba Warumi 7 inaelezea mtu ambaye hajaokoka anayejijua kwamba amehukumiwa kwa sheria ya Mungu lakini hana uwezo wa kuishi kwa kuitii hiyo sheria.

► Kwa maneno yako mwenyewe toa muhtasari mfupi wa yale ambayo tumeyaelezea katika sehemu hii. Hakuna ulazima wa kufanya mdahalo wa jambo hili kwa wakati huu kwa sababu ushahidi wa ziada utatolewa katika somo hili.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 4, kifungu cha 2

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(7:15) Wenye dhambi wengi wanatamani kama wangekuwa wanatenda mambo yaliyo mema. Matamanio hayo hayam aanishi kwamba wao ni Wakristo. Hamu yao ambayo haijatimizwa inaonyesha kwamba bado hawajakombolewa kutoka katika nguvu ya dhambi.

(7:16) Matamanio yao kwamba wangeweza kufanya vizuri zaidi yanaonyesha kuwa wanajua kwamba sheria ni nzuri, ingawaje hawaitii.

(7:17-23) Dhambi inazungumziwa kama ni kitu ambacho kilikuwa kimetawala mapenzi ya mwanadamu. Mwanadamu aliyeanguka kwa asili hana mapenzi ya uhuru ambayo Mungu kwa asili alikuwa amemuumba mwanadamu akiwa nayo. Mapenzi ya mwanadamu ni madhaifu sana kiasi kwamba mwenye dhambi hawezi akamchagua Mungu, labda Mungu, kwa neema yake arejeshe mapenzi yake.

Neema ya awali ni kitendo cha Mungu cha kuwafikia wale ambao bado hawajawa na mwitikio kwake. Neema hii ambayo imetolewa kwa watu wote hujumuisha marejesho ya hiari ya mtu na hali ya kumtamani Mungu, ili kwamba kila mtu aweze kuchagua kiukweli kama aidha aokoke au asiokoke.

Mungu huanzisha kazi ya wokovu kwa kila mtu (Yohane 6:44; Waefeso 2:4-5, 12-13, 17; Tito 2:11, Tito 3:3-5), lakini mtu hawezi kuokoka kabla hajawa na mwitikio kwa Mungu.

(7:24) Hiki ni kilio cha kukata tamaa na kuchanganyikiwa ambacho kinakuja pale mtu anapoona kukosa kabisa uwezo wa kujiokoa mwenyewe. Hiki siyo kilio cha mtu aliyeokoka.

(7:25) Taarifa ya kusifu inaingilia hapa kama nuru katika giza kwa ajili ya maisha ya mwenye dhambi anayekata tamaa.

Kisha inafuata sentensi ambayo inatoa muhtasari wa kifungu hiki. Mwenye dhambi anatoa makubaliano ya akili yake kwamba sheria ni sahihi, na anajifanya kuwa bora zaidi kuliko alivyo; lakini tamaa zake za dhambi zinaendelea kumweka kwenye dhambi. Mtu anahukujiwa kwa kuitumikia dhambi kwa akili yake na mwili (7:5, 8:3).

Kumwelewa Mtu katika Warumi 7:14-25

Katika kifungu hiki Paulo anazungumzia kuhusu nguvu ya uharibifu ya kurithi (sheria ya dhambi) kwenye maisha ya mtu ambaye hajaokoka. Paulo, alipotambua kwamba alikuwa mwenye dhambi, sana alijichanganya ndani yake yeye mwenyewe.[47]

Sheria ya dhambi katika mwili wa Paulo inatoa matokeo yafuatayo:

- Mtu anafanya kile anachokichukia (7:15).
- Mtu anafanya kile asichokitaka kufanya (7:16).
- Kuna tamaa ya kufanya mambo mema, lakini hakuna nguvu ya kuyafanya (7:18).
- Sheria ya dhambi inaizuia sheria ya akili zake (7:23).
- Yeye ni mateka wa sheria ya dhambi (7:23).
- Ni mtu aliyegawanyika: Akili yake inamhudumia Mungu, lakini mwili wake unatumikia sheria ya dhambi (7:25).

Mtu hawezi akatumikia mabwana wawili. Mtu hawezi kuwa huru kutokana na dhambi na mtumwa wa dhambi. Mtu hawezi akawa mtumwa wa Mungu na mtumwa wa Shetani kwa wakati mmoja. Lugha ya Warumi 7:14-25 moja kwa moja ni kinyume cha taarifa iliyoko katika Warumi 6 kuhusu kukombolewa kwa mwenye dhambi kutoka kwenye utumwa wa dhambi. Kwa hiyo, 7:14-25 ni mwendelezo wa maelezo ya uhusiano wa mtu ambaye hajaokoka na dhambi na sheria iliyoanza katika 7:1-13.

Warumi 6 inaelezea kuhusu uhusiano wa mtu aliyeamini na dhambi, yakiwa ni matokeo ya kusulubiwa na kufufuka pamoja na Kristo. Warumi 7 inatumika kama kielezo cha:

- Uhusiano wa mwenye dhambi na sheria.
- Muingiliano wa dhambi ikaayo ndani na sheria.
- Juhudi za mwenye dhambi zinazoamshwa kwa madai ya sheria ya Mungu, lakini akishindwa kufanya hivyo yeye mwenyewe kwa yale ambayo sheria inataka kwa sababu ya kuwa mtumwa wa dhambi ikaayo ndani.

Ufafanuzi wa Warumi 7:14-25 hutofautiana.

Mtazamo wa 1: Baadhi ya wanazuoni waliandika kwamba Paulo alikuwa anafafanua maisha ya **kawaida ya Mkristo**. Wanadokeza kwamba vitenzi ni vya wakati uliopo na siyo vya wakati uliopita; na wanasisitiza kwamba kwenye mtazamo wa Paulo, maisha ya Mkristo yana mambo ambayo hayajatatuliwa.

Mtazamo wa 2: Wanazuoni wengine wengi pia wanaamini kwamba Paulo anaelezea hali ya mtu kabla hajaokoka. Wanasema kwamba maneno ya vifungu kama "kuuzwa chini ya dhambi" na "Ole wangu, maskini mimi" hayapatani na maelezo ya mtu aliyeamini katika Warumi 6 na Warumi 8. Kwa mujibu wa Warumi 6, mwamini amekufa kwa dhambi, amekombolewa kutoka katika dhambi, anatangaza kwa imani na kusalimisha kabisa kwa

[47] Sehemu hii inatoka kwenye masomo ya darasani ya Dr. Allan Brown.

Mungu uhuru unaopatikana ndani ya Kristo kwa ajili ya ushindi dhidi ya dhambi. Kwa mujibu wa Warumi 8, mtu anayetembea katika hali ya mwili hawezi kumpendeza Mungu na hana Roho wa Kristo anayekaa ndani yake.

Mwandishi wa somo hili anadhani kuwa mtazamo wa pili unalingana na mtiririko wa hoja ya Paulo katika Warumi na unaendana na mafundisho yake kwa ujumla.

Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusiana na mtu wa Warumi 7:14-25

Hapa kuna maswali ambayo mara kwa mara hujitokeza kutoka kwa watu ambao kwa makosa hufikiria kwamba Paulo anaelezea kuhusu maisha yake ya Kikristo katika Warumi 7:14-25.

Swali la 1: Je, inakuwaje kuhusu taarifa za Paulo kwamba anaifurahia sheria ya Mungu kwa utu wake wa ndani (Warumi 7:22)? Je, farisayo asiyeamini anaweza kuifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani?

Jibu: Farisayo yeyote angeweza kusema kwamba anaifurahia sheria ya Mungu katika moyo wake. Walitumia muda wao mwingi katika kujifunza sheria ya Mungu na kila siku walitumia masaa mengi katika kujifunza hiyo sheria ya Mungu. Paulo alikuwa ametumia muda wake mwingi katika kujifunza sheria ya Mungu na kwa ukweli alidhamiria kuitii. Lakini wakati Roho Mtakatifu alipomwonyesha Paulo asili ya hali ya tamaa aliyokuwa nayo ndani ya moyo wake, akimzindua kwenye uhalisia wa kweli wa hali ya kiroho, Paulo alijikuta kwamba alikuwa anaendelea kutenda mabaya licha ya kutamani neema iliyowezeshwa ya akili yake ya kufanya yaliyo mema. Sheria ilimwoyesha Paulo jinsi ya kuishi, lakini sheria haikumpa uwezo wa jinsi ya kuifanya.

Swali la 2: Je, vipi kuhusu sarufi ya wakati uliopo kwenye Warumi 7:14-25? Paulo anaandika, "Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni; bali **mimi ni** mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi" (Warumi 7:14).

Jibu: Paulo alikuwa akizungumza katika wakati uliopita katika Warumi 7:7-13 na akabadilisha kwa kutumia wakati uliopo katika Warumi 7:14-25. Walakini, anasimulia hadithi sawa kutoka kwa maisha yake mwenyewe katika sehemu zote mbili. Ukweli kwamba Warumi 7:14-24 iko katika wakati uliopo haimaanishi kwamba Paulo anapitia mambo hayo kwa sasa, wakati yeye ni mtume Mkristo aliyekomaa na mmishenari, akiandika barua hii kwa kanisa la Rumi. 'Historia" au "hali ya kuvutia" ya wakati uliopo lilikuwa ni jambo linaloeleweka la kutumia wakati uliopo kwa Kiyunani wakati mwandishi anapotaka kufanya jambo lililopita au uzoefu uwe wazi kwa wasomaji wake. Kwa hiyo, matumizi ya wakati uliopo ili kufanya wazi kile kilichokuwa cha ukweli kwenye wakati uliopita wa Paulo ambao alikuwa ameokoka hauna maana kwamba Paulo bado anapambana katika utumwa wa dhambi kwa wakati wa sasa. Paulo ameonesha wazi katika Warumi 6 na Warumi 8 kwamba Mkristo siyo wa kuuzwa katika utumwa wa dhambi (Warumi 7:14).

Swali la 3: Je, vipi kuhusu kifungu hiki kwenda sambamba na mapambano mengi ya Wakristo wanayokutana nayo katika maisha yao?

Jibu: Mapambano ya mtu aliyeamini ni tofauti kabisa na mapambano ya mtu mwenye mwovu. Mtu mwovu wa Warumi 7:14-25 hawezi akaacha kutenda dhambi. Ni mtumwa wa dhambi. Hili siyo suala linalomhusu Mkristo wa kweli. Mkristo anaweza akawa na vipindi vya mapambano na kushindwa, lakini maisha yake siyo yale ya kitumwa kwa sheria ya dhambi na kifo. Mkristo ameungana na Kristo na amewekwa huru kutoka kwenye dhambi ikaayo ndani (Warumi 6:1-10).

Hitimisho: Mtu mwovu wa Warumi 7:14-25 inaonekana ni farisayo mtiifu akipambana kumpendeza Mungu. Mtu hawezi kuwa huru kutokana na dhambi akiwa bado mtumwa wa dhambi. Mtu hawezi akawa mtumwa wa Mungu na mtumwa wa dhambi, kwa sababu Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili" (Mathayo 6:24, Luka 16:13). Warumi 7:14-25 ni mwendelezo wa maelezo ya uhusiano wa mtu ambaye hajaokoka na dhambi na kwa sheria ya Musa iliyoanza katika 7:7-13.

► Jadili suala la utambulisho wa mtu aliyeko katika Warumi 7, kwa uangalifu ukichukulia maanani undani wa mambo yote na maelezo yaliyotolewa.

Kutumia Sheria katika Uinjilisti

Mtume anatuambia kwamba katika Warumi 7:7 sheria inatumika katika uinjilisti kwa kuwa mtu huliona hitaji lake la wokovu pale anapotambua kwamba anahukumiwa kwa sheria ya Mungu. Kupitia historia ya kanisa, wainjilisti waliofanikiwa sana wameitumia sheria ya Mungu katika kusababisha wenye dhambi kutamani wokovu.

Nukuu zifuatazo zinaonyesha mambo ambayo wainjilisti walikuwa wamesema kuhusu kutumia sheria.

► Badilishana zamu katika kuzisoma hizi nukuu na kuzifafanua kwa msaada wa wanafunzi wengine katika kikundi.

Kutoka kwa Charles Spurgeon[48]

> Kama utaiondoa sheria utakuwa umeondokana na dhambi, kwa sababu dhambi ni kuvunja sheria; na mahali ambapo hakuna sheria, hakuna uvunjaji wa sheria. Ukiondokana na dhambi utakuwa pia umeondokana na Mkombozi pamoja na wokovu, kwa kuwa kwa vyovyote vile havitahitajika tena. Wakati unapokuwa umeachana na dhambi hadi kwenye kiwango cha chini kabisa, kuna hitaji gani tena la wokovu mkuu na wa utukufu ambao Yesu Kristo alikuja kuuleta kwa ajili ya ulimwengu?
>
> Watu kamwe hawataikubali neema hadi watakapokuwa wametetemeka mbele ya sheria ya haki na takatifu; kwa hiyo, sheria inatekeleza kusudi muhimu na la baraka.[49]

[48] Spurgeon alikuwa ni mwinjilisti na mhubiri mashuhuri sana katika Uingereza kwenye miaka ya 1800.
[49] Charles Spurgeon, "Kudumu kwa sheria ya Mungu"

Kutoka kwa Charles Finney[50]

> Mtu kwa busara zake na kwa moyo wake wote hawezi akauliza au akakubali msamaha hadi pale atakapohisi kwamba ukweli na haki imetendeka katika hukumu yake.
>
> Sheria ya kiroho lazima itumike kikamilifu katika dhamiri mpaka mwenye dhambi aondokane na hali ya kujihesabia haki, na asimame akiwa hana usemi akijihukumu mbele ya Mungu mtakatifu.
>
> Daima, sheria ni lazima iandae njia kwa ajili ya Injili. Ukipuuza jambo hili katika kuelekeza mioyo kwa uhakika utapata matumaini potofu, ni kuanzisha viwango vya vya uongo vya utendaji wa kikristo, na kulijaza kanisa na wakristo bandia.[51]

Kutoka kwa Martin Luther[52]

> Lakini Shetani... ameinua kikundi ambacho kinafundisha kwamba Amri Kumi za Mungu zinatakiwa ziondolewe katika kanisa, na kwamba watu wasisababishiwe hofu kwa ajili ya sheria, lakini wahimizwe kwa upole kwa kuhubiri neema ya Kristo.[53]

Kutoka kwa John Bunyan[54]

> Kwa muda ambao watu wamekuwa wajinga kuhusiana na asili ya sheria na wao kuwa chini ya hiyo sheria – yaani, chini ya laana na nguvu ya kuhukumu iliyo katika hiyo sheria, kwa sababu ya dhambi ya kwenda kinyume na hiyo sheria – ni kwa kiasi hicho hicho wataendelea kuwa wazembe au wasiojali, na wajinga katika kufuatilia kuuliza kuhusu ufahamu wa kweli wa injili.
>
> Mtu ambaye haijui sheria hajui kwa kweli na katika ukweli yeye ni mwenye dhambi, na hajui kwamba katika kuokoa yupo Mkombozi.[55]

Kutoka kwa Jonathan Edwards[56]

> Njia pekee tunayoweza kujua kama tunatenda dhambi ni kwa kuijua sheria ya Mungu ya maadili.[57]

---

[50] Finney alikuwa mwinjilisti katika nchi ya Amerika kwenye miaka ya 1800. Alihusika sana na watu wengi waliookoka kuliko mhubiri mwingine yeyote katika karne ile.
[51] Charles Finney, "Jinsi ya kuvuna roho"
[52] Martin Luther alikuwa mleta mabadiliko nchini Ujerumani ambaye aligundua tena injili ya kibiblia, akisababisha maelfu ya watu kuokoka.
[53] Martin Luther , katika maelezo yake ya ufafanuzi kuhusu Maoni kwa *Kitabu cha Wagalatia*
[54] Bunyan alikuwa mwandishi wa Pilgrim's Progress, kitabu kilichochapishwa sana kuhusu njia ya Mkristo ya kwenda mbinguni.
[55] John Bunyan, *Fundisho la imani la Sheria na Neema Iliyofunuliwa*
[56] Edwards alikuwa mwana teolojia na mhubiri wa wakati wa Uamsho Mkuu wa Kwanza katika Amerika, uliohusika na maelfu ya watu kuokoka.
[57] Jonathan Edwards, "Tahadhari kwa Mkristo: Umuhimu wa Kujipima Binafsi"

Kutoka kwa John Wesley[58]

> Ili kumwua mwenye dhambi, ni lazima kwanza itumike sheria; yaani, kuyaondoa maisha na nguvu ambayo anategemea, na kumthibitishia kwamba yeye yuko chini ya adhabu ya kifo, lakini kiuhalisia amekufa kwa Mungu, akiwa hana maisha ya kiroho, amekufa katika makosa na dhambi (Waefeso 2:1). Matumizi ya pili ya sheria ni kumleta katika uhai, kwa Kristo, ili aweze kuishi.
>
> Usije ukafikiri au ukazungumzia kwa wepesi tu kuhusu [sheria] hiki chombo cha baraka na neema ya Mungu. Badala yake, ipende na uithamini kwa ajili yake ambaye imetoka na kwa ajili ya yule inayokwenda kwake.[59]

► Ni tatizo gani lingetokea ikiwa wahubiri wangezungumza tu kuhusu upendo na msamaha wa Mungu kwa watu ambao hawakuona dhambi yao kuwa nzito?

Maswali ya Mapitio Somo la 7

(1) Taja sababu mbili zinazonesha kuwa sheria za ibada na sheria za kiraia za Agano la kale bado zina umuhimu.

(2) Je, ina maana gani kufa katika sheria?

(3) Je, neno katika mwili lina matumizi gani mawili?

(4) Je, sheria inafanyaje dhambi iwe mbaya Zaidi?

(5) Kwa nini sheria inafaa kwa uinjilisti?

Kazi ya kufanya Somo la 7

Andika mifano ya sheria za Agano la kale ambazo hazikutajwa katika somo hili. Elezea kama ni za ibada, za kijamii au za kimaadili; elezea jinsi ambavyo Mkristo anaweza akazitumia leo.

[58] Wesley alifanya uinjilisti na akawaandaa watu wake waliookoka, na wahubiri waliookoka ambao walimsaidia yeye. Kabla ya kifo chake, watu waliokuwa wameokoka Uingereza jumla walikuwa 79,000, na Amerika walikuwa jumla 40,000.
[59] Iliyofafanuliwa kutoka John Wesley "Asili, Mali, na Matumizi ya Sheria ya Mungu"

Somo la 8
Maisha katika Roho

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 4, Kifungu cha 3

Katika somo hili tunaendelea na Sehemu ya 4 ya Kitabu cha Warumi. Tumejifunza Warumi 6, kuhusu "ushindi dhidi ya dhambi," na Warumi 7, kuhusu "mtenda dhambi mwenye hatia." Katika somo hili tutajifunza Warumi 8, ambayo inaelezea maisha ya Mkristo kwenye hali ngumu za dunia.

Jambo Kuu katika Warumi 8

Ingawaje mwamini anaishi kwenye dunia iliyoanguka, akipata mateso kutokana na hali ya dunia na kutokana na udhaifu wake mwenyewe, Roho Mtakatifu humpa ushindi juu ya dhambi na katika hali zote anazopitia.

Muhtasari wa Warumi Sura ya 8

Sura hii inarejea mara nyingi katika nafsi tatu zilizoko kwenye Utatu Mtakatifu wa Mungu. Nafsi hizi zote tatu zinahusiana kwa karibu sana katika wokovu wetu wa sasa na wa baadaye. Tunaweza kuishi kwa ushindi tukiwa katika hali ya mwili, tunaweza kufurahia kwa uhakika wokovu wetu binafsi, tunaweza kuhimili hali mbalimbali za maanguko zilizopo, tunaweza kuomba kwa msaada wa kiroho zaidi ya akili zetu wenyewe, na tukaendelea kudumu katika uhusiano wetu wa wokovu na Mungu.

8:1-13 zinaunda kifungu ambacho kinaweza kikaitwa "Siyo katika Mwili tena."

Utangulizi wa Warumi 8:1-13

Wale watu wote ambao hawahukumiwi ni wale ambao hawafuati tena mambo ya mwili. Kuwa katika hali ya kimwili haimaanishi ni kuwa mwanadamu; bali inamaanisha ni kuwa chini ya mamlaka ya hali ya asili ya anguko la dhambi.[60]

Kuwa katika *hali ya kimwili* inatofautisha na kuwa katika hali ya kuokoka. Hali ya kimwili ni kifo (8:6) na ni uadui na Mungu (8:7). Mtu aliyeko katika hali ya kimwili hawezi akampendeza Mungu (8:8) na lazima atakufa (8:13). Kuwa katika *hali ya kimwili* ni hali moja inayofanana na ile iliyoelezwa katika 7:7-25 (ona 7:14, 18, 25).

8:12-13 ni hitimisho. Hatupaswi tuishi katika hali ya kimwili, kwa kuwa mtu anayeishi katika hali ya kimwili atakufa, hii ikiwa na maana kwamba ni kupokea hukumu ya Mungu (ona 1:17). Ni lazima tuue matendo ya dhambi ya mwili. Kwa kuwa mtu anayefuata matendo ya

[60] Mwangalizo katika somo la 7 kuhusu "Kufafanua Mwili/Nyama" ni muhimu sana katika kukielewa kifungu hiki.

kimwili ni mwenye dhambi, sio mfuasi wa Yesu, dhambi ni lazima isambaratishwe kabisa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 8:1-13 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(8:1) Mtu anayefuata mambo ya Roho hayuko chini ya hukumu. Mtu anayefuata mambo ya kimwili yuko chini ya hukumu –na hayuko ndani ya Kristo.

(8:2) Sheria ya Roho kuhusiana na maisha ni kwamba mtu aliyesamehewa anakubaliwa kwa neema na anakuwa na maisha ya kiroho. Sheria ya dhambi na kifo ni kwamba mtu ambaye ataonekana kuwa na hatia kupitia hiyo sheria atahukumiwa adhabu ya kifo.

(8:3) Sheria imetoa mahitaji. Haikutoa nguvu. Mwenye dhambi hakufuata sheria; kwa hiyo, sheria haikuwa ndiyo njia ya wokovu. Mungu alimtuma Mwanaye kama Mkombozi.

(8:4) Hatuisahau sheria ya Mungu lakini tunaitii kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

(8:5) Kila mtu hufuata asili yake mwenyewe. Kama hajapokea maisha ya kiroho, basi anatawaliwa na hali ya kimwili.

(8:6) Kutawaliwa na hali ya asili ya dhambi ni kuwa chini ya hukumu. Mbadala wake ni kutembea katika Roho na kumtii Mungu. Hakuna njia nyingine ya mkato ya kupata msamaha wakati mtu anapoendelea kufuata matendo ya dhambi.

> "Wanadamu wanaridhika na kile kilicho nje, kinachoonekana, vitu na vilivyo vya juu. Kilicho muhimu kwa Mungu kina kina, cha ndani, ni kazi ya siri ya Roho Mtakatifu katika mioyo yetu"
>
> - John R.W. Stott,
> *Ujumbe wa Warumi:*
> *Habari njema ya Mungu kwa dunia*

(8:7-8) Mtu aliye katika asili ya hali ya kimwili kwa kawaida ni adui wa Mungu, kwa sababu kwa jinsi anavyoendelea kutawaliwa na hali ya asili ya dhambi hawezi akajitoa kuwa chini ya Mungu. Katika hali hiyo hakubaliki kwa Mungu.

► Orodhesha baadhi ya mambo yanayoelezea kuhusu mtu ambaye yuko katika hali ya kimwili.

(8:9) Kuwa katika *hali ya kimwili* maana yake ni kuwa chini ya mamlaka ya hali ya asili ya anguko la dhambi; mtu aliyeamini hayuko tena katika hali ya kimwili. Bado ataendelea kukumbana na majaribu, lakini hatakuwa chini ya mamlaka, na anao uwezo wa kuzuia jaribu. Aya hii inatuambia kwamba uwezo huu uko hapo kwa sababu Roho wa Mungu naye yuko hapo. Mtu hawezi kudai kwamba anaongozwa na amepakwa mafuta ya upako na Roho Mtakatifu kama hana ushindi dhidi ya dhambi.

> "Hamu nzuri, iliyo chini ya uthibiti, inasaidia afya na ina manufaa. Hamu hiyo hiyo, inayomweka mtu katika utumwa na kutawala maisha yake, inaleta kifungo na dhambi."
>
> - Wilbur Dayton

(8:10-11) Mwili wa mwanadamu bado umeathirika na dhambi ya Adamu pamoja na dhambi zetu zilizopita. Kwa hiyo, matamanio ya mwili yanaweza yakaenda kwenye mwelekeo mbaya. Hatuwezi tukayaamini matamanio ya miili yetu kutuongoza. Lakini nguvu ile ile ambayo ilimfufua Yesu kutoka kwa wafu inafanya kazi ndani yetu, na inatupa uhai ili kwamba miili yetu iweze kuletwa kwenye utii kwa Mungu. Udhaifu wa mwili hauwezi kuwa ni sababu ya kutenda dhambi. Hatupaswi kutenda dhambi, kwa sababu uweza wa Mungu ni mkuu kuliko udhaifu wa miili yetu.

(8:12-13) Kufuata hali ya kimwili kunasababisha kifo cha kiroho. Kupitia Roho Mtakatifu tunayaua matendo yote ya kimwili, na kuyasambaratisha hadi mwisho. Watu wanaofanya hivyo huepuka hukumu ya Mungu. Maandiko haya hayaruhusu mtu aliyesamehewa na kukubaliwa na Mungu kuendelea kutenda dhambi.

Sheria ya Mungu kwa Mkristo

Baadhi ya watu husema kwamba sheria ya Mungu haina umuhimu kwa maisha ya Mkristo. Mambo wanayosema ni kama vile, "Mungu hajali lolote kuhusu matendo yako," na "wakati utakapoingia mbinguni matendo yako yatakuwa siyo chochote." Kwa mawazo yao, neema huchukua nafasi ya utii. Lakini Paulo alisema, "Basi, je! Twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sheria (Warumi 3:31). Kama tutafundisha injili itakayoiona sheria kwamba siyo kitu chochote, hiyo siyo injili ambayo Paulo aliihubiri.

Sheria ambayo Paulo aliizungumzia siyo tu utaratibu wa sheria za Musa. Sheria ya Musa ilikuwa ni utendaji wa mapenzi ya Mungu kwa wakati na mahali maalumu. Mambo yake mengi hayafanyi kazi kwenye maeneo yote na kwa muda wote kwa njia inayofanana, hasa kwenye hali za ibada na sheria zilizotolewa kwa Waisraeli kwa taifa. Kanuni za sheria ya Musa bado zinafanya kazi hata sasa kwa sababu tabia ya Mungu haibadiliki.

Kwa ujumla, sheria ya Mungu ndiyo inayohitajika kwa ajili ya mwanadamu. Sheria ni takatifu, haina upendeleo, na ni nzuri, (7:12) kwa sababu inatoka kwenye asili ya Mungu mwenyewe. Sheria ya Mungu ni ya kiroho (7:14).

Haki ya sheria inakamilika kwa wale watu ambao wanatembea na Roho Mtakatifu badala ya kutembea katika hali ya kimwili (8:4) kwa sababu wanaishi kwa kumtii Mungu.

Biblia inatoa taarifa zifuatazo kuhusiana na sheria ya Mungu:

1. Utii wa sheria unapaswa uwe ni udhihirisho wa upendo kamili kutoka ndani ya moyo (Mathayo 22:37-40).

2. Kusudi la Amri maalumu za Mungu ni kuonyesha hitaji la upendo kutoka katika moyo ulio safi, dhamira njema, na imani ya uhalisia wa kweli (1 Timotheo 1:5). Ni jambo lisilowezekana kwa mtu kuweza kutimiza kwa ukweli kabisa mahitaji yote ya Mungu isipokuwa kwa nia ya upendo, hivyo, kutotii unaonyesha kukosekana kwa upendo.

3. Mtu mwenye upendo huu anatimiza sheria yote; yaani, anatimiza yote ambayo Mungu anahitaji kutoka kwa mtu (Warumi 13:8-10). Kwa hiyo, kuwa na upendo kamili ni kuwa na utii kamili.
4. Upendo hudhihirishwa kwenye utii (1 Yohane 5:2-3). Upendo siyo tu hisia au uaminifu uliotabiriwa kwa Mungu. Upendo hauwezi kuwa badala ya utii lakini unachochea utii.
5. Yesu hakuja kuitangua sheria, na alisema kwamba kama mtu atawafundisha watu wengine kuivunja sheria, ataitwa mdogo sana katika ufalme wa mbinguni. (Mathayo 5:17-20).

Uelewa mzuri wa sheria ni muhimu kwa injili kwa sababu watu kwa ajili ya umilele wameshahukumiwa kwa kuvunja sheria ya Mungu. Mtu hawezi akatubu hadi akubaliane na Mungu kuhusiana na dhambi na sheria. Baadhi ya watu wanatambua mwenye dhambi anastahili kwenda motoni kwa kuvunja sheria ya Mungu, lakini bado wana mawazo ya ajabu kwamba Mungu hajali tena kuhusu sheria baada ya kuwa mtu ameamini.

Sheria siyo kigezo cha kukubalika kwetu na Mungu. Lakini inatupa sisi ufahamu wa kujua ni kwa jinsi gani Mungu anatutaka tuishi.

► Kwa mtu aliyeamini, kuna uhusiano gani kati ya kumpenda Mungu na sheria ya Mungu?

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 4, kifungu cha 3

Utangulizi wa Warumi 8:14-27

8:14 inaunganisha aya zilizotangulia kwenye mada muhimu ya uhakika wa wokovu kwenye aya zinazofuata. Utambulisho wa watoto wa Mungu ni kwamba wanamfuata Roho Mtakatifu na wanaishi kwa ushindi badala ya kufuata hali ya mwili na kuishi katika dhambi.

8:14-27 ni kifungu ambacho kinaweza kupewa kichwa cha habari "Msaada wa Roho Mtakatifu katika Ulimwengu Ulioanguka."

► Mwanafunzi atapaswa asome Warumi 8:14-27 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(8:14) Utambulisho wa mtoto wa Mungu ni kwamba anamfuata Roho Mtakatifu na anaishi kwa ushindi badala ya kufuata hali ya mwili na kuishi katika dhambi.

8:14-17 inaelezea uhakika wa wokovu binafsi unaoletwa na Roho Mtakatifu.

(8:15) Kama watu ambao tumeamini, hatupaswi kurudi tena kwenye hofu ya sheria. Badala yake, tunaishi na uhakika wa wokovu kwa neema. Tumerithiwa kama watoto wa Mungu. Utii wa Mkristo siyo suala la kurudi nyuma na kuwa chini ya sheria kama njia ya wokovu bali ni suala la uhusiano na Mungu.

> Ni sehemu ndogo tu ya Wakristo wa sasa wanaojinasibu kuwa waumini ambao kwa kweli wanachukua kwa umakini kazi ya kuhesabiwa haki kupitia Kristo katika maisha yao. Wengi wao wana ufahamu hafifu sana wa utakatifu wa Mungu na uzito wa dhambi zao kiasi kwamba kwa dhahiri hawaoni haja kubwa ya kuhesabiwa haki, ingawa katika undani wa maisha yao wanajawa na hisia za hatia na kutokuwa na usalama. Wengine wengi wanajitolea kinadharia tu kwa mafundisho haya, lakini katika maisha yao ya kila siku wanategemea utakaso wao kwa ajili ya kuhesabiwa haki, kwa mtindo wa Augustino, wakipata uthibitisho wa kukubalika kwao na Mungu kupitia unyofu wao, uzoefu wao wa zamani wa kugeuka, utendaji wao wa hivi karibuni wa kidini, au mara chache kwa makosa yao ya dhahiri na ya makusudi. Wachache wanajua vya kutosha kuanza kila siku kwa kusimama thabiti juu ya msingi wa Luther: kwamba wamekubaliwa, wakiangalia nje kwa imani na kudai haki ya Kristo, ambayo si yao wenyewe, kama msingi pekee wa kukubalika kwao, na kupumzika katika aina hiyo ya imani ambayo italeta utakaso unaozidi kuongezeka kadri imani inavyofanya kazi kwa upendo na shukrani.[61]

(8:16) Aya hii inaelezea kitu ambacho wainjilisti walioamini wanaita "ushuhuda wa Roho." Roho wa Mungu anatuthibitishia kwamba tuko kwenye uhusiano wa upendo na utii pamoja na Mungu na ni shuhuda kwamba tumeokoka. Roho zetu wenyewe zinatambua kuhusu ukweli huo. Mkataba huo wa Roho wa Mungu na roho zetu ndio msingi wa uhakika tulio nao ili kwamba tusiwe watu wa kuishi kwa mashaka, tukijifikiria kama kweli tumeokoka.

Dini na madhehebu ambayo hayahubiri kuhusu uhakika wa wokovu wanawaweka watu wao kwenye mashaka. Watu wanakuwa na mashaka kwamba hawajafanya lolote la kutosha ili waokoke. Injili inaleta ukombozi wa kutoka kwenye mashaka kwa sababu tunajijua kwamba tumesamehewa. Utii wetu umejikita katika kumfuata Roho Mtakatifu ili kumpendeza Mungu ambaye tayari ameshatukubali sisi, kuliko kushika sheria kama njia ya kuweza kukubalika kwake.Tunaweza tukajijua kwamba tumeokoka kwa sababu tunaishi kwa utii kwenye uhusiano pamoja na Mungu na kuwa na ushuhuda wa Roho Matakatifu kwamba ni kweli tumeokoka. (Ona 1 Yohane 2:3, 29; 1 Yohane 3:14, 18-21, 24 kwa ajili ya msingi wa kimaandiko kuhusu uhakika wa wokovu.)[62]

► Ni ushauri gani utakaoweza kumpa mtu ambaye hana uhakika kwamba ameokoka?

(8:17-18) Tutarithi pamoja na Kristo utukufu na ufalme wa Mungu. Utukufu wake utadhihirishwa ndani yetu kwa mambo mengi na makubwa ambayo amefanya ndani yetu, akibadilisha asili yetu iwe kama vile alivyopanga tuwe. Tutarithi uzima wa milele, ikimaanisha tutaishi maisha ya Mungu. Tutatawala pamoja na Kristo. Hata hivyo, siyo marupurupu yetu yote yatapatikana kwa sasa. Utukufu unaotajwa hapa bado ni siku za

---

[61] Richard Lovelace, *The Dynamics of Spiritual Life*, (Downers Grove, IL: Intervarsity Press, 1979) 101.

[62] Picha: "roman road to arch" ilipigwa na Steven Damron mnamo Januari 5, 2010, imepatikana kutoka https://www.flickr.com/photos/97719890@N00/4249691365, imepewa leseni chini ya CC BY 2.0, imeshushwa rangi kutoka kwenye asili.

baadaye. Mateso ni sasa, na utawala ni baadaye. Hata hivyo, utukufu wa mwisho ni mkuu mno kiasi kwamba hali zetu za sasa siyo muhimu ukilinganisha na hatima yetu.

8:19-25 zinaelezea kuendelea kudumu katika imani wakati tukiwa tunamsubiri Mungu arejeshe tena uumbaji wake kwa ukamilifu.

(8:19) Kila kitu kilichoumbwa bado kinasubiri muda ambao Mungu atawatukuza kikamilifu watoto wake. Mtume Yohane anasema kuwa hatujaona muundo wa miili yetu tutakayokuwa nayo mbingunini (1 Yohane 3:2).

(8:20-21) Kila kitu kilichoumbwa bado kinateseka na matokeo ya dhambi. Mungu ameruhusu laana iendelee kubakia kwa mategemeo kwamba wenye dhambi watatubu kwa sababu ya kuona matokeo ya dhambi. Viumbe vilivyoumbwa hatimaye vitarejeshwa na kuletwa kwenye ukamilifu wa mwisho wa mpango wa Mungu. Hii haitawahusu wale watu ambao hadi mwisho wameyakataa mapenzi ya Mungu, wakikataa kutubu.

Barabara za Kirumi

Warumi walijenga barabara nyingi za njia kuu katika nchi zote walizotawala. Ubunifu wa ujenzi ulizifanya kuwa mororo na kudumu kwa muda mrefu. Barabara hizo zilikuwa sehemu ya mtandao uliounganisha katikati ya jiji la Roma, jambo lililosababisha kusema, "Barabara zote zinaelekea Roma."

(8:22) Laana ya dhambi ilivuruga uumbaji wote. (Mwanzo 3:17-19). Kazi ni ngumu. Ardhi haizalishi tena kwa ajili ya mwanadamu kama ilivyokuwa kabla ya anguko. Magonjwa, uzee na kifo huja kwa viumbe vyote vinavyoishi.

(8:23) Hata watu walioamini bado wanateseka kwa matokeo ya dhambi kwa sababu miili yao bado haijarejeshwa kwenye hali ilivyokuwa kabla ya anguko. Tunaye Roho Mtakatifu kama sehemu ya kwanza, aliye mfano, na shahidi wa mwisho wa urejeshaji wa Mungu. Mwisho wa yote, urejeshaji mkamilifu wa uumbaji utakuwa wokovu wa mwisho. Tunaweza kusema kwamba tayari tumeokoka, lakini bado tunangojea kwa ajili ya wokovu wa mwisho.

► Je, ni mambo gani unayoona ni dalili zinazoonesha kwamba uumbaji uko chini ya laana ya dhambi?

Sera ya Shetani kwa wenye dhambi ni kuwapa kitu kilicho kizuri sana atakachoweza pale mwanzoni, kisha kwapa kibaya na kibaya tena, akiwahadaa na ahadi ambazo hawezi kuzitekeleza na mwisho wake kuishia motoni. Mungu anatupa sisi mfano wa mbinguni kwa sasa na anaweka akiba ya vitu vizuri zaidi kwa ajili yetu baadaye.

(8:24-25) Aya hizi zina ujumbe kwamba tunangojea kuona vitu ambavyo bado hatujawahi kuviona au kuvipokea.

Kufufuliwa kwa mwili ni fundisho la imani muhimu la Kikristo, na kulikataa kunapelekea kuishi maisha ya dhambi.

Baadhi ya watu katika kanisa la Korintho walikana ufufuo. Katika hilo ikaotokea misimamo miwili mikali.

1. Msimamo mkali wa kukandamiza tamaa za kimwili kwa sababu walifikiri kuwa wao ni waovu.
2. Msimamo wa uzembe na kudekeza tamaa za mwili kana kwamba hazina madhara yeyote

Baadhi walifikiri kwamba ikiwa mwili utaenda kutupwa kama kitu kisichofaa na kiovu, basi kuwa na tamaa za mwili ni dhambi. Kwa hoja hii, walisema mtu asioe bali awe bikira. Wengine walikuwa wazembe na waliachilia na walitii tamaa zao za kimwili, kwa sababu walifikiri hazikuwa na madhara. Mikazo hii inapitiliza kiwango na siyo ya Kikristo. Imani hizi zenye uharibifu, za uongo zinatokana na kukana fundisho la ufufuo wa mwili.

8:26-27 zinaelezea kazi ya Roho Mtakatifu kwenye maombi ya mtu aliyeamini.

(8:26-27) Hali yetu ya kuanguka inaleta madhara kwenye mtazamo wa akili na kiroho. Hatuwezi tukaelewa kwa ukamilifu wote kweli zote za kiroho. Hatuwezi tukaelewa kwa ukamilifu wote ni nini Mungu anachokusudia kukifanya kwa ajili ya dunia. Tunapoomba, Roho Mtakatifu hufidia udhaifu wetu kwa kuomba pamoja nasi maneno ambayo hatuwezi kuyasema. Anajua jinsi ya kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu.

Aya hizi hazina maana ya kuomba katika lugha isiyojulikana. Taarifa ni kwamba Roho Mtakatifu anasema maombi kwa ajili yetu kwa sababu hatuwezi kuyasema. Aya hizi hazisemi kwamba tunaomba katika njia fulani isiyokuwa ya kawaida.

Utangulizi wa Warumi 8:28-39

Kifungu hiki kinaelezea kwamba waumini wako kwenye mpango wa Mungu, na anakusudia kuwapa neema ya kumaliza safari yao ya Ukristo na kubadilishwa kuwa katika sura ya Kristo. Hakuna hali zozote ambazo ziko duniani zinazoweza kututenganisha na Mungu kwa sababu neema na nguvu zake ni kuu mno.

Kifungu hiki kinaweza kikapewa kichwa cha habari "Usalama wa Kiroho wa Mtu Aliyeamini."

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 8:28-39 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ay Aya-kwa-Aya

(8:28) Kifungu cha maneno "mambo yote " kinahusisha mambo yote ambayo tunapitia katika mateso. Haimaanishi kwamba Mungu ametoa amri kwa mambo yote yanayotokea, ikiwemo dhambi. Inamaanisha kwamba Mungu huleta matokeo mazuri kutoka katika mambo hayo yote kwa ajili ya watu walioamini. Katika 8:37, baada ya kuorodhesha aina zote za mateso, akasema kwamba, katika mambo hayo yote sisi ni zaidi ya washindi. Mungu

huyatumia mateso kwa ajili ya makusudi yake mwenyewe na hutujenga sisi kwa kupitia hayo.

Mungu hatoi amri au maagizo kwa kila kitu kinachotokea. Huwa anaruhusu mapenzi huru yafanye kazi, anaruhusu uthubutu wa kweli uweze kuchukuliwa ambayo yanategemea uwepo wa nafasi, na hata wakati mwingine anaruhusu dhambi itendeke. Lakini bado kwa mtu aliyeamini, Mungu huleta matokeo mazuri kutoka katika matukio yote – ikiwa ni kutoka hata katika dhambi za watu wengine walizozifanya kwa madhumuni mabaya ya kusababisha madhara.

(8:29) Tunatambua kwamba siyo kila mtu katika ulimwengu huu ameokoka. Kwa hiyo, wale aliowajua tangu asili ni wale ambao aliwajua kwa mambo maalumu. Tunatambua kutoka katika muktadha wa kitabu cha Warumi kwamba Mungu huchagua wale watu ambao wanaamini. Anajua mambo ya mbeleni ni mtu gani atakayeitikia wito wake wa wokovu kwa imani. (Ona pia 11.2 na maelezo yake.) Ni jambo la muhimu kuelewa kwamba Mungu alijua kwanza ndipo alikuja kuchagua au kupanga. Mungu alipanga kuokoa watakatifu (Ona Zaburi 1:6, 1 Wakorintho 8:3, Wagalatia 4:9, na 2 Timotheo 2:19 kwa ajili ya mifano ya Mungu "kujua.")

Alipanga kwa ajili yao kufanana kama Kristo. Kufanana kama Kristo inamaanisha kwamba tutatafanywa tufanane na Kristo katika mwenendo wetu.

(8:30) Ni kazi ya Mungu inayotuleta kutoka kote huko tuliko hadi kwenye wokovu wa milele. Hakuna chochote kinachohitajika kutoka kwetu isipokuwa nia yetu tu.

(8:31-32) Hakuna hali zozote zinazoweza kuwa ngumu za kumshinda Mungu. Tayari alishafanya dhabihu ya hali ya juu sana, kwa hiyo sasa atatupa sisi kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya ushindi wetu.

(8:33) Hakuna mtu yeyote anayeweza kutuhesabia wenye hatia ya dhambi katika kumbukumbu zetu kwa sababu zimefutwa kwa kuhesabiwa wenye haki kulikotolewa na Mungu.

(8:35-39) Kifungu hiki kinatoa matumaini makubwa na faraja kwa wale wanaomfuta Yesu. Hakuna kinachoweza kukutenganisha na Mungu. Paulo anasema kwamba tunalindwa kiroho kutoka kila kitu ambacho tunaweza kukabiliana nacho katika ulimwengu huu. **Usalama wa mtu aliyeokoka ni ahadi ambayo kamwe Mungu hawezi kushindwa kumpa nguvu ya kuvumilia katika imani yake na hakuna nguvu nyingine yeyote itakayoweza kumtoa kutoka kwa Mungu.**

► Je, nii kwa jinsi gani unaweza kuelezea namna amabavyo Mungu humsaidia mwamini kukabiliana yote kwa imani

Maswali ya Mapitio Somo la 8

(1) Kwa nini haiwezekani sheria iwe ni njia ya wokovu?

(2) Je, ina maana gani kusema mwamini hatawaliwi tena na mwili?

(3) Je, ni kwa jinsi gani sheria inaelekeza maisha ya mkristo?

(4) Je, ushuhuda wa Roho ni nini?

(5) Wokovu wa mwisho ni nini?

(6) Je, kama watu watakana ufufuo wa mwili matokeo yake ni nini?

(7) Je, ni nini usalama wa mwamini?

Kazi ya kufanya Somo la 8

Andika ukurasa mmoja kuelezea matatizo ya kuishi kama Mkristo katika ulimwengu ulioanguka na pia toa maelezo ni nini Roho Mtakatifu anafanya kwa Mkristo.

Somo la 9
Uteuzi wa Mungu

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 5

Barua kwa Warumi inalezea jinsi mtu anavyoingia katika uhusiano na Mungu ili kupokea wokovu na baraka. Uhusiano na Mungu umejikita katika neema inayopokelewa kwa Imani. Kifugu hiki kinasababisha maswali yanayohusu Israeli. Kunatokea nini katika uhusiano maalumu kati ya Mungu na Israeli? Je, Myahudi nawezaje kuokoka? Je, Mungu bado ana mpango kwa Waisraeli? Sura hizi zinajibu maswali hayo Paulo anapoendelea kuelezea ujumbe wa injili.

Haki ya Mungu katika Kesi

"Ee binadamu; wewe u nani umjibuye Mungu?" (Warumi 9:20). Baadhi ya watu wameitumia aya hii katika kukemea mtu yeyote ambaye anajaribu kuihoji au kuipima haki ya Mungu. Wanasema kwamba haki ya Mungu iko juu sana kuliko haki yetu kiasi kwamba hatuwezi kabisa kuifahamu.

Je, kuna aina ya kiwango kingine cha juu cha haki ambacho nyeusi inakuwa nyeupe na uovu unakuwa mzuri? Ikiwa hakimu wa kibinadamu angehukumu watoto wachanga, makosa yaliyohukumiwa na atakuwa dhalimu. Ikiwa angehukumu makosa na uhalifu wa makusudi sawa, atakuwa dhalimu. Lau angewaadhibu watu kwa kufanya yale wasiyoweza kuyazuia, tusingesema kuwa anahukumu kwa kiwango cha juu cha uadilifu, bali alikuwa dhalimu.

> "Ili Mungu awe wa milele, ni lazima awe na uwezo wa kusimamia mashitaka yote yatakayohusu mashetani yote, malaika wote, na wanadamu wote. Hakuna yeyote atakayekuwa na uwezo wa lazima wa [haki ya] kumlaumu kwamba hatendi haki."
>
> - R.G. Flexon, *Rudiments of Romans*

Haki ya Mungu ni ya kiwango cha juu lakini haitofautiani na haki yetu. Ufahamu wetu kuhusiana na haki unatoka kwake na uko kwenye misingi ya viwango vyake. Anatuamrisha sisi tuwe watakatifu kwa maana ile ile iliyo sawa kwamba na yeye ni mtakatifu. Kama kwa wakati mwingine hatua zake zinaonekana kutokuwa za haki kwetu ni kwa sababu hatutazami ukweli wote uliopo, kwa sababu maadili yetu ni ya muda sana, na kwa sababu mitazamo yetu imepotoshwa na matamanio yetu wenyewe.

Mungu hajinadi tu kuwa mwenye haki na kukataa kuelezea njia zake kwa viumbe wake. Badala yake, Kitabu cha Warumi kinaweka msisitizo kwamba haki ya Mungu ni kitu kinachoonekana. Wale wanaomkataa Mungu "hawatakuwa na udhuru" (1:20) kwa sababu ya kile wanachokijua kuhusiana na Mungu. Wenye dhambi wanajua kwamba wanastahili hukumu (1:32). Warumi 2 inaeleza wazi kabisa kuhusu kutopendelea na hukumu za Mungu

hazibadiliki badiliki. Kazi ya upatanisho iko hivyo kwamba Mungu hana upendeleo ingawaje huwahesabia haki wenye dhambi. (3:26).

Ni jambo lililo wazi kwamba Mungu anataka tumwone yeye kuwa ni mwenye haki. Kwa sababu hiyo, Mungu ameelezea sera zake za wokovu, akielezea ni kwa nini ni za haki. Itakuwa ni jambo lisilowezekana kwetu sisi kumwabudu Mungu katika kweli kama hatutamwona yeye kuwa ni mwenye haki. Kama hatutaweza kumwamini Mungu kwamba ni mwenye haki, utiifu wetu kwake utakuwa ni sawa na utiifu kwa jitu katili au jambazi.

Kwa hiyo, Mungu mwenyewe huruhusu awekwe katika mashitaka, au hata anajiweka mwenyewe kwenye hali hiyo. (3:4). Mungu ana uhakika kwamba matendo yake yanaendana na haki ya kweli. Jaribio la uaminifu la matendo ya Mungu litaonesha kuwa Mungu ni mwenye haki na kuwa mwenye dhambi ni mwenye hatia.

► Je, kwa nini ni muhimu kwetu sisi kuelewa matendo ya haki ya Mungu? Je, tunajuaje kwamba Mungu anatutaka sisi tuelewe kuhusu haki yake?

Mtazamo wa Biblia kuhusiana na ukuu wa Mungu:

- Mungu amechagua kuruhusu watu kufanya chaguzi za kweli pamoja na matokeo yake.
- Mungu huwaacha watu wakae na chaguzi zao walizozifanya (Warumi 1:24, 26, 28).
- Mungu ni mwenye nguvu na hekima ya kutosha katika kukamilisha mpango wake wa mwisho licha ya yale ambayo mtu mwingine yeyote anayafanya.

Ngome ya Kirumi

Ngome hii imesimama huko Rumi tangu nyakati za kale.

Kila mtu anaamua aidha kutokuikubali au kuikubali injili na akaokoka au akakataa kuokoka katika msingi huo. Mungu hutoa wokovu, huwapa watu kutambua kuhusu wao kuwa na hatia, huwapa watu matamanio ya neema, na huwapa uweza wa kuamini. Huwatuma wajumbe wake kuwashawishi wasioamini watubu. Lakini mtu binafsi anafanya maamuzi yake mwenyewe kuhusiana na wokovu wake.[63]

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 5, kifungu cha 1

Jambo Kuu katika Warumi 9

Mungu amechagua njia ya wokovu, na hakuna njia nyingine yeyote ambayo mtu anaweza akaitumia katika kupata wokovu.

[63] Picha: "Porta San Paolo front", by Joris, Machi 1, 2005, imepatikana kutoka https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Porta_San_Paolo_front.JPG, mali ya umma.

Muhtasari wa Warumi Sura ya 9

Mara nyingi sura hii hufasiriwa kumaanisha kwamba Mungu huwa anachagua ni nani wa kuokoka na ni nani wa kupotea kwa msingi ambao hatuwezi kuujua. Kwa kweli, jambo halisi ni kwamba Mungu amechagua njia ya wokovu, na kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kuokoka kwa njia nyingine yeyote. Ukuu wake Mungu hauonyeshwi kwa kuchagua baadhi ya watu na kukataa wengine bila vigezo vyovyote. Ukuu wake unaonyeshwa kwa uwekaji wake wa vigezo – muundo wa njia ya wokovu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 9:1-5 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(9:1-3) Paulo alionesha huzuni kubwa kwa ajili ya Israeli kwa sababu kiroho walikuwa wamepotea. Alitaja kwamba alikuwa ndugu yao. Paulo alikuwa ametokana na dini ya Kiyahudi. Aliwaheshimu wanazuoni wake. Alihuzunishwa kwa kutambua kwamba wengi wa waalimu na viongozi na wengi wa watu waliowatumikia walikuwa wamemkataa Kristo.

(9:4-5) Israeli lilikuwa taifa lililokuwa na faida nyingi za kiroho.

- Kwanza walikuwa na Mungu kama Baba.
- Kwanza walikuwa wameuona utukufu wa Mungu ukifunuliwa.
- Walikuwa na
  - Maagano kama masharti ya baraka zake.
  - Sheria.
  - Aina za kuabudu.
  - Ahadi za wokovu mkuu.
- Mababa wa ahadi walikuwa Wayahudi.
- Yesu alizaliwa kama Myahudi.

Mwanzoni Paulo alisema katika 3:1-2 kwamba Wayahudi walikuwa na faida nyingi sana.

Uyahudi, Chimbuko la Ukristo

Uyahudi unaweza kusemwa kwamba ndio chimbuko la Ukristo. Hata sasa Uyahudi una mambo yanayofanana zaidi na Ukristo kuliko dini nyingine yeyote. Uyahudi haukuwa kwenye kundi la dini za uongo hadi ilipokuja kumkataa Kristo.

Orodha inayooneshwa hapa chini ni mahusiano yaliyopo kati ya Ukristo na Uyahudi:

1. Wakristo na wafuasi wa Uyahudi wote kwa pamoja wanamwabudu Mungu mmoja wa kufanana na wamepokea ufunuo kutoka kwa Mungu

2. Uyahudi ndio uliotoa msingi wa teolojia na falsafa ya Ukristo. Waisraeli walikuwa wanaamini Mungu mmoja aliye wa milele, asiyekuwa na asili na aliye mtakatifu. Mungu aliumba kila kitu kikiwa kizuri, lakini uovu na mateso vikawepo kwa sababu ya dhambi. Mwanadamu ni kiumbe maalumu kilichoumbwa katika sura au mfano wa Mungu, akiwa na hatima yenye utukufu baada ya kuwa amekombolewa.

Tunachukulia hizi kweli zote, lakini zinatofautiana na dini nyingine zote zilizoizunguka Israeli ya kale. Kweli hizi zote mwanzoni zilikuwa zimefunuliwa kwa Waisraeli.

3. Wakristo na wafuasi wa Uyahudi wanakubaliana na Agano la Kale kama ndiyo Maandiko, lakini wafuasi wa Uyahudi hawakubaliani na Agano Jipya.

4. Yesu, mwanzilishi wa Ukristo, alikuwa ni Myahudi na aliithibitisha dini ya watu wake. Alielezea vipaumbele vyake vya kweli na akalaumu uharibifu uliokuwa ukifanywa na Mafarisayo. Hakudai kutaka kuanzisha dini mpya bali kuikamilisha ile ya zamani.

5. Moyo wa Uyahudi ulikuwa unamtarajia Masihi. Wakristo wa kwanza walikuwa ni Wayahudi ambao waliamini kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi wa Wayahudi.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 5, kifungu cha 1

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 9:6-16 kwa ajili ya kikundi.

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(9:6-9) Baadhi yao walikuwa wameokoka; Neno la Mungu lilikuwa limeleta mabadiliko kwao. Watu wa Mungu sio tu wale ambao ni wazao wa kibiolojia wa Ibrahimu. Ni wale watu waliookoka kwa kuziamini ahadi za Mungu.

Tangu wakati ambao Mungu alimchagua Ibrahimu, wokovu ulikuwa umepangwa uwe wa njia hii. Mpango wa Mungu wa wokovu, ambao ulikuwa uendelee hadi kwa Isaka, ilikuwa ni kazi ya Mungu iliyokuwa inategemea mwitikio wa imani. Mfumo wa Mungu wa wokovu ni ahadi, kisha imani, kisha muujiza. Kuzaliwa kwa Isaka kulikuwa ni muujiza.

Ismaili alizaliwa katika hali ya kawaida ya asili, na siyo kimuujiza, na Mungu hakumtumia kwenye mpango wa ukombozi. Kwa kanuni hiyo hiyo, Mungu hakubaliani na wokovu kwa njia ya matendo. Wayahudi waliokuwa wanataka wokovu kwa matendo yao walikataliwa na Mungu kama na vile Ismaili alivyokataliwa kuwa mtoto wa ahadi.

► Je, vipi kuhusu suala la Yakobo na Esau? Baadhi ya watu wanafikiri kwamba aya hizi zinasema kwamba kabla hawajazaliwa, Mungu alishamchagua ni nani atakayetumika. Aya hizi kimsingi zinasema nini?

(9:10-13) Wakati Mungu alipomchagua Yakobo badala ya Esau, hakuwa akichagua mtu yupi wa kuokoa. Alihitaji kuchagua yule ambaye ataweza kumtumia katika kutimiza mpango wa wokovu. Hii ndiyo mada ya sura hii: Haki ya Mungu ya kuchagua njia ya wokovu. Kumbukumbu za maisha ya Esau katika Agano la Kale zinaonyesha kwamba kwa ukweli alikuwa na badiliko la moyo wake na ingewezekana akaokoka. Alikuwa hajakataliwa kwenye wokovu, bali alikataliwa kuwa baba wa taifa teule na Masihi. Neno *nimemchukia* linamaanisha tu kwamba "kukataliwa kwa ajili ya mtu mwingine," kama ilivyomaanisha wakati Yesu aliposema kwamba ni lazima kumchukia baba au mama katika kuweka ulinganifu wa utii wetu kwake (Luka 14:26).

Mungu hakumchagua Yakobo kwa sababu ya sifa zake au hakumkataa Esau kwa ajili ya makosa yake. Kifungu hiki kinaweka msisitizo kwamba walikuwa hawajafanya jambo lolote jema au baya wakati Mungu alipofanya chaguo lake. Bila shaka, Mungu alikuwa anajua hatima zao. Jambo la msingi hapa ni kwamba Mungu alichagua kutokana na mpango wake mwenyewe.

► Baadhi ya watu wanasema kwamba 9:14-16 inathibitisha kwamba Mungu huchagua ni nani wa kuokolewa kwa sababu ambazo sisi hatuzijui. Wanasema kwamba matendo yetu na mambo tunayochagua haviwezi kuamua kama tunaweza au hatutaweza kuokoka. Aya hizi kwa uhakika zinasema nini?

(9:14-16) Mungu huchagua ni nani atakayemwonyesha rehema. Hiyo haimaanishi kwamba anafanya bila ya kuwa na msingi au kwenye msingi ambao hatutaweza kuujua. Mungu ameonyesha msingi wa rehema zake: "Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa" (Isaya 55:7).

Anatueleza kwa uwazi kwamba tumechaguliwa kwa ajili ya wokovu kama tutaamini na tutakataliwa kama hatutaamini. Kwa hiyo, siyo kutokana na mapenzi ya mtu atake kujiamulia ni kwa jinsi gani anavyotaka aokoke. Wokovu ni lazima utokane na rehema za Mungu, na upokelewe kama alivyoagiza.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 9:17-23 kwa ajili ya kikundi. Je, Mungu alimwumba Farao ili awe mtu mwovu na amthibiti ili kwamba aweze kutenda mambo ya uovu?

(9:17-18) Farao hakuzaliwa kwa ajili ya kuhukumiwa, lakini Mungu alimweka kwenye nafasi ya mamlaka kwa sababu Mungu alijua ni kitu gani anakwenda kukifanya. Neno *nilikusimamisha* halirejelei kwenye uumbaji wake bali kwenye kumsimika mtawala. Mungu ni mwenye rehema kwa wale wanaoamini na huifanya mioyo ya watu wasioamini kuwa migumu. Kufanya moyo kuwa mgumu haina maana kwamba Mungu anambadilisha mtu mzuri kuwa mtu mbaya. Mungu alimpa Farao jukumu la kutekeleza kile ambacho tayari alishakusudia kukifanya.

Wale watu ambao wanafanywa kuwa na mioyo migumu wanafikiriwa kama wenye hatia kwa ajili ya hali zao. Kwa hiyo, kwa mujibu wa haki, kuchagua kwao ni halisi. Mwanzoni, katika Warumi 2:4-5, Wamataifa wanahukumiwa kwa ugumu wa mioyo yao ambako kumeunganishwa na kuukataa ukweli kwa mapenzi yao wenyewe. (Ona pia Yeremia 19:15, Nehemia 9:25-29, Marko 16:14, na Waebrania 3:7-13). Farao hangekuja kuwa na moyo mgumu kama siyo kule kumkataa Mungu kuanzia mwanzo.

(9:19) Hapa mtu anainua upinzani: "Kama Mungu anadhibiti watu, kama alivyofanya kwa Farao, mtu kama huyu atahukumiwaje? Hakuna mtu yeyote ambaye amepingana na mapenzi yake kwa mafanikio." Mwenye kuinua upinzani anazungumza kana kwamba mtu anapaswa asamehewe kwa kumpinga Mungu kama hatimaye alilazimika kufanya kile

ambacho Mungu alikuwa ametaka kifanyike. Lakini Mungu ni mwenye uwezo wa kutofautisha kati ya wale wanaokubaliana naye kwa hiari yao wenyewe na wale ambao hawako hivyo.[64]

(9:20-23) Mungu ni mwenye uwezo wa kuchagua baadhi ya watu kwa ajili ya hukumu na wengine kwa ajili ya rehema, ingawaje mwisho wa siku atatukuzwa na watu wote (kwa sababu yeye anatukuzwa kwa pamoja kwa ajili ya hukumu yake na rehema zake). Ana msingi wa uchaguzi wake na ana haki ya kuchagua. Mungu huweka vigezo vyake kwa ajili ya kukubalika, na havibadiliki.

Mfinyanzi anaweza akaamua afanye nini na udongo. Anaweza akatumia sehemu ya udongo kutengeneza jagi la kuwekea maua na sehemu nyingine ya udongo huo akaamua atengeneze gudulia la kuwekea takataka. Ni kwa njia hiyo hiyo, Mungu huamua kwamba baadhi ya watu wanafaa tu kwa ajili ya hukumu na watu wengine wanastahili rehema. Kitenzi cha Kiyunani hakioneshi ni nani anayefanya tendo. Inaweza kumaanisha kuwa watu wenyewe wanajitayarishia hukumu. Hiyo itakuwa sawa na taarifa kwamba Mungu huvumilia maasi yao hadi wakati ambapo hukumu itakuja. Mungu hakuwaumba kwa ajili ya hukumu au kwa ajili ya kuwafanya wawe watenda dhambi. Hukumu zao zitatokana na jinsi walivyojichagulia wao wenyewe. Ukweli kwamba Mungu ni mwenye mamlaka katika kuchagua kwake haimaanishi kwamba anachagua kwa upendeleo lakini anachagua kwa viwango vyake yeye mwenyewe. Anachagua watu waovu kwa ajili ya hukumu na watu walioamini kwa ajili ya wokovu.

Swali kwamba "Kwa nini Mungu amenifanya niwe hivi?" haimaanishi kwamba "kwa nini umeniumba mimi kwa ajili ya kuhukumu," bali "Kwa nini uliamua kwamba nilikuwa nafaa kwa ajili ya hukumu?" Lakini Mungu anayo haki ya kuamua na kudhihirisha haki yake.

Mfano wa mfinyanzi unapatikana kutoka Yeremia 18:1-18. Aya muhimu ni 18:7-10. 18:8 inasema, "Ikiwa taifa lile nililolitaja litageuka, na kuacha maovu yake nitaghairi, nisitende mabaya yale niliyoazimia kuwatenda."

► Je, ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea mfano wa mfinyanzi na udongo? Je, Mungu aliwaumba watu wengine kwa kusudi la kuwatumia kuonesha ghadhabu yake? Je, Inamaanisha nini kusema kwamba anatengeneza vitu mbalimbali kutoka katika udongo?

Hitimisho Binafsi la Mtume

Baadhi ya watu wamehitimisha kutoka katika sura hii kwamba Mungu huumba watu wengine kwa kusudi la kuhukumiwa na wengine kwa ajili ya kupata rehema. Hata hivyo, Paulo mwenyewe anaelezea kwamba hitimisho lake kuu liko katika sura hii (9:30-33). Ni muhimu kwamba tumwachie mwandishi na jambo kuu alilo nalo kutokana na mfano wake alioutoa mwenyewe. Hatupaswi kubishania matumizi ya maelezo ya mwandishi ambayo yako kinyume na yale ambayo mwenyewe ameyaelezea. Hoja kuu ya Paulo ni hili: Mungu

[64] Ona maelezo ya kumbukumbu juu ya kifungu kinachofanana katika Warumi 3:5-8.

atamhukumu mtu binafsi katika msingi kwamba aidha ameamini au hajaamini. Kama mfinyanzi, ana haki ya kuamua msingi wa kukubalika.

Tunaweza tukafurahia katika ukuu wa Mungu kwa sababu kila siku ni mwenye hekima, ni mzuri, ni mwenye upendo na haki katika kila analolitenda. Ingawaje anayo mamlaka yote kabisa, hafanyi jambo lolote lisilokuwa la haki. Matendo yake siku zote ni sawa na asili yake mwenyewe.

Jambo lililopo kwenye sura hii siyo kwamba Mungu huchagua kila mtu binafsi anayemtaka bila ya kuzingatia vigezo. Jambo kuu katika Warumi 9 ni kwamba Mungu anaweka vigezo vyake ambavyo huamua ni nani amchague kwa ajili ya kuokoka. Kigezo muhimu ni imani inayookoa.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 5, kifungu cha 1

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 9:24-33 kwa ajili ya kikundi.

Mwendelezo wa maelezo ya Aya–kwa-Aya

(9:24-26) Wamataifa wengi hufanyika kuwa sehemu ya watu wa Mungu, ingawaje walikuwa hawaitwi ni watu wa Mungu kwenye misingi ya utaifa wao. Hali hii inaunganisha mada kuu ya umishenari ya Waraka huu: Injili inaweza kupelekwa kwa mtu yeyote katika ulimwengu huu.

(9:27-29) Wayahudi wengi watakataliwa, na masalia peke yao ndio watakaookolewa. Wayahudi hawataokolewa moja kwa moja kisa tu kwa sababu wao ni Wayahudi. Kama Mungu atakuwa ametenda kwa mujibu wa haki bila ya kuweka hapo rehema yake, wangeangamizwa kabisa kama ilivyokuwa kwa Sodoma.

(9:30-33) Hapa ndio hitimisho la hii sura. Mwandishi anapaswa apewe nafasi ya kutoa hitimisho lake mwenyewe. Mada ya sura hii ni kwamba Mungu ameweka mpango wake wa wokovu. Watu wengine wote waliojaribu kuanzisha njia zao nyingine za haki kwa msingi wa sheria walishindwa. Wale wote wanaotafuta haki kwa njia imani wanafanikiwa. Mtu anayejaribu kuanzisha haki yake wenyewe hujikwaa juu ya jiwe kuu la pembeni ambalo Mungu ameliweka, lakini atakayeamini hatatayarika au hataaibika.

Maswali ya Mapitio Somo la 9

(1) Je, tunajuaje kuwa Mungu anataka tuelewe anavyotenda haki?

(2) Je, ni kwa nini ni muhimu kwetu kuona kwamba Mungu ni wa haki?

(3) Je, mtazamo wa kibiblia kuhusu ukuu wa Mungu ni upi?

(4) Je, jambo kuu katika Warumi 9 ni nini?

(5) Je, manufaa ya kiroho ya Israel ni nini?

(6) Je, kuna mahusiano gani matano kati ya Ukristo na Uyuda?

(7) Je, Warumi 9 inasemaje kuhusu Mungu kumchagua Yakobo?

(8) Je, kwa nini tunafurahia ukuu wa Mungu?

Kazi ya kufanya Somo la 9

(1) Andika ukurasa mmoja ukielezea ni kwa jinsi gani Mungu ni mkuu mno na bado anaitikia uchaguzi wanaofanya wanadamu. Tumia Warumi 9, lakini pia waweza kutumia maandiko mengine.

(2) Unapaswa kuandaa angalau mazungumzo mawili kati yako na waamini wengine kutoka makanisa mengine. Unapaswa uwaulize wafafanue wanafikiri nini kuhusiana na ukuu wa Mungu. Unapaswa uwaelezee kifungu kutoka katika Warumi ambacho kinaendana na mada husika. Unapaswa uandike maelezo ya mazungumzo yenu na kisha yakabidhiwe kwa kiongozi wa darasa.

Somo la 10
Ujumbe wa Haraka

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 5, kifungu cha 2-3

Warumi 10 ni kilele cha kitabu cha Warumi. Mtume tayari alishaeleza kwamba wokovu ni kwa neema kwa njia ya imani na kwamba kila mtu katika ulimwengu huu anauhitaji. Kwa kuwa imani ni ya lazima, ujumbe wa injili ni muhimu: Watu wanahitaji kusikia ujumbe ili kwamba waweze kuuamini. Sura hii ni ya muhimu katika kusudi la kitabu kwa sababu kitabu chote kinatoa msingi wa kazi ya umishenari.

Warumi 11 inahusika na mahusiano kati ya Waisraeli na Kanisa. Wayahudi wengi waliikataa injili. Paulo alielezea kwamba mpango wa Mungu ulikuwa ni dunia yote pamoja na Wayahudi waweze kuokolewa. Waisraeli kwa ujumla wao kuna siku moja watakayomkubali Kristo.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 5, kifungu cha 2

Jambo Kuu katika Warumi 10

Haki ni lazima ipatikane kwa imani, na umuhimuwa imani uhafanya ujube wa injili uwe na umuhimu wa haraka.

Muhtasari wa Warumi Sura ya 10

Ni kosa kujaribu kuhesabiwa haki kupitia kujihesabia haki binafsi. Haki ambayo Mungu huikubali kutoka kwa mwanadamu, yeye kwanza anampa mwanadamu kutokana na mwitikio wake wa imani. Ujumbe wa injili unatoa nafasi kwa ajili ya imani.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 10 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(10:1-5) Wayahudi bado wanahitajika waokoke kwa sababu hawakuelewa haki waliyoihitaji ni kitu gani. Walijaribu kujihesabia haki wenyewe kwa kuanzisha kumbukumbu mahususi za haki binafsi, bila kutambua kwamba jambo hilo lilikuwa haliwezekani. Haki ambayo Mungu anaikubali ni ile ambayo yeye anaifanyia kazi ndani ya mtu kwa mwitikio wa imani.

Kusudi la sheria ni kutuleta sisi kwa Kristo kwa kulaani dhambi na kuonesha hitaji kwa ajili ya Mkombozi. Wakati mtu anapokuja kwa Kristo, sheria haiwi tena kwamba ndio msingi wa kukubalika kwake na Mungu, hivyo Kristo huwa ndio mwisho wa hiyo sheria (10:4). Hiyo haimaanishi kwamba sheria haituoneshi tena njia ya kumtii Mungu, lakini kukubalika kwetu na Mungu hakutegemei sisi kuwa na kumbukumbu ndefu ya utii uliokamilika na wa muda mrefu.

Nadharia kwamba watu walioishi kabla ya Kristo kuja waliokolewa kwa matendo yao moja kwa moja inakataliwa na kifungu hiki. Paulo anaelezea waziwazi kwamba watu wote waliojaribu kutengeneza haki yao wenyewe kwa njia ya matendo walikuwa wamepotoshwa na kupotea. Wangepaswa waamini ukweli wa injili ambao Paulo aliunukuu kwenye 10:6-8 kutoka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati.[65]

Vatikani

Baada ya mateso kuisha mwaka wa 313, Rumi muda mfupi ikawa mji mkuu wa kanisa, kama ilivyokuwa kwa dola. Bado ni mji mkuu wa Kanisa Katoliki. Picha inaonyesha Vatikani, makao makuu ya Ukatoliki.

(10:6-11) Hii ni nukuu ya Kumbukumbu la Torati 30:11-14. Musa aliwaambia Waisraeli kwamba kuzishika amri za Mungu na maagizo yake hakutegemei kiwango fulani cha ushujaa au nguvu za kibinadamu zisizo za kawaida, kama vile kupaa mbinguni au kuvuka bahari. Badala yake itakamilishwa ndani yao na Mungu kupitia katika imani yao.[66]

Paulo alitohoa taarifa hii akirejelea kwenye matendo ya ajabu ya kupaa kwenda mbinguni au kushuka duniani na akaonesha kwamba Kristo alishatimiza mambo yote yaliyokuwa muhimu.

Wokovu kwa njia ya neema ni karibu mno kiasi kwamba uko ndani ya mioyo na midomo yetu kwa sababu tunaupokea kwa imani (mioyoni mwetu) na kwa kuukiri (kwa vinywa vyetu).

(10:12-13) Hapa kuna msisitizo mwingine kwamba njia hiyo hiyo ya wokovu inapatikana kwa kila mtu. Yesu ni Bwana juu ya kila kitu, na mtu yeyote aliyeko mahali popote katika dunia hii anaweza akamwita.

(10:14-15, 17) Huu ni wito kwa ajili ya kazi ya umishenari. Ujumbe wa mishenari ni wa haraka - Kwa kuwa watu wanaokoka kwa imani, wanahitaji kusikia ujumbe ambao utawapeleka katika kuamini. Aya hizi ni za umuhimu wa kina kwa kusudi la kitabu hiki.

"Barua za Paulo zinaonesha kuwa uinjilisti wake ulikuwa na misukumo miwili: hali ya uwajibikaji inayokuja kutokana na yale ambayo Mungu alimfanyia na kumpa jukumu la kuwafanyia wengine, na hamu kwamba Mungu atatukuzwa na watu wengi kadiri inavyowezekana.Tunapaswa kumwiga Paulo kwa kutoa neema ya Mungu katika injili kama alivyofanya."

- Douglas J. Moo, *Romans*

[65] Ona sehemu inayofuata.

[66] Picha: "St Peters. Rome" ilipigwa nailipigwa na Brian Dillon mnamo Desemba 12, 2010, retrieved imepatikana kutoka https://www.flickr.com/photos/28805679@N03/6375448359/, imepewa leseni chini ya CC BY 2.0, imeshushwa rangi na kukatwa kutoka kwenye asili.

Paulo anaonesha shauku kubwa kwa ajili ya kazi ya mmishenari na anaelezea mkasa kwa wale ambao watakuwa hawajaisikia injili. Wanaweza wakaokoka kwa kuamini, lakini wataaminije wasiposikia, na watasikiaje kama hakutapelekwa mmishenari?

► Paulo alizungumzia hitaji la kutuma wamisionari, yaani kusaidia katika kuwawezesha na kuwapa misaada inayotakiwa. Wewe utakuwa unafanya nini kwa ajili ya kumsaidia kupeleka injili kwa watu ambao hawako karibu na wewe?

(10:16, 18-21) Kuingizwa kwenye wito wa umisheni ni ukumbusho kwamba siyo watu wote watakaokubali mwitikio huo. Watu hawaokoki kwa taarifa ya injili peke yake. Wamataifa walikuwa na taarifa ya Ufunuo wa Ujumla (uliojadliwa katika 1:18-20), lakini hilo halikuweza kuwa sababu ya wao kuokoka kwani walilikataa (10:18 ni nukuu kutoka Zaburi 19:4). Waisraeli walikuwa na ufunuo wa zaidi, hata hivyo, hawakuokoka kisa tu kwa kuwa walikuwa na ufunuo huo. Isaya alikuwa ametabiri kuhusu Waisraeli kumkataa Masihi (Isaya 53:1, 3).

Mtume anajibu hizi pingamizi. Kwanza, kuhusu Wamataifa, mtu anaweza akasema, "Lakini kweli hawajui?" Paulo anajibu, "Ndiyo, ufahamu wa Mungu uko kila mahali," kama alivyoeleza katika 1:20. Kisha, mpinzani anauliza kuhusu Wayahudi: "Je, Israeli haikujua?" Paulo anajibu kwamba Mungu anaendelea kuwafikia Waisraeli, lakini, walikataa kutii. Mpinzani ana mashaka na ufanisi wa ujumbe wa injili kwa sababu wengi waliusikia na hawakuokoka.

Paulo alielezea kwamba Waisraeli wengi hawakuitikia kwa imani.[67] Watu hawaokoki kwa ujumbe hadi wawe wameitikia.

Kuhubiri hakuwezi kumfanya mtu aliyekataa aweze kuokoka – Neema ya Mungu si kitu ambacho hatuwezi kupinga. Hata hivyo, inatoa nafasi ya wokovu. Ingawaje kila mtu anajua chochote kuhusiana na Mungu, injili inakuja na nuru kubwa zaidi na nguvu kubwa ya kuona hatia kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu 5, kifungu cha 3

Jambo Kuu katika Warumi sura ya 11

Hakuna mtu yeyote anayeweza kuokoka bila ya kukubaliana na vigezo vya Mungu vya wokovu.

Muhtasari wa Warumi 11

Waisraeli kwa ujumla hawakuokoka kwa sababu walikataa kuokolewa katika njia ya Mungu. Wengi wa Wamataifa waliokoka, lakini yeyote aliyeanguka kutoka katika imani aliupoteza wokovu wake. Wayahudi wanaweza wakaokoka kama wataamua kuchagua hivyo, na Israeli

[67] Ona sehemu iliyoko katika somo la 4 yenye kichwa cha habari "Neema katika Agano la Kale."

kwa ujumla wake kuna siku moja wataikubali injili. Mungu atatimiza ahadi zake alizozitoa kwa mababu zao.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 11:1-15 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(11:1) Swali ni kwamba, "Je, Mungu amewakataa Wayahudi?" Paulo anajibu, "Hapana, Na mimi pia ni Myahudi." Baadhi ya Wayahudi waliokoka.

(11:2-5) Wale amabo Mungu aliwajua hawakataliwi. Bila shaka, Mungu alimjua kila mtu kwa mantiki kwamba yeye ni mjuzi wa mambo yote, lakini wale aliowajua kwa mantiki ya aya hii haiwezekani ikawa ni kila mtu kwa sababu aya inazungumzia kuhusu watu maalumu wa Israeli. Aya inahusiana na wale ambao Mungu anajua watakuwa na mwitikio wa neema yake.[68] Paulo anatoa mfano wa watu ambao Mungu aliwajua katika mantiki hii na wakakubalika – watu 7,000 ambao hawakumwinamia Baali.

Masalia ambao wamechaguliwa na Mungu (11:5) hawakuchaguliwa kiholela au bila ya utaratibu maalumu. Walikuwa na watu ambao Mungu aliwajua kwamba watamwamini yeye.

(11:6) Matendo na neema siku zote huenda kwa pamoja katika maisha ya Mkristo, lakini vyote vinatofautiana katika msingi wa wokovu. Huwezi kuvichanganya pamoja kwa msingi wa kukubaliwa na Mungu, kama dini za uongo zinavyofundisha.

(11:7-10) 11:8, ambayo ni nukuu kutoka Isaya 29:10, inaonesha kuwa watu kutokuwa waaminifu kuliwafanya wawe vipofu kiroho. Mioyo yao ikawa migumu kwa kuwa waliendelea kuikataa kweli. Isaya 6:9-10 vile vile inasema kwamba watu huwa vipofu wanapoendelea kusikia na kukataa rehema inayooneshwa. Mistari hii katika Warumi haina maana kuwa Mungu alikataa kuonesha rehema kwa baadhi ya watu. Laana ya Daudi (Zab 69:22, 23), ambayo Paulo ananukuu katika Warumi 11:9-10, haikuwa ni kutubu ambayo watu wangekataliwa, lakini watu waovu wangehukumiwa.

(11:11) Je, Mungu amewaruhusu kuanguka kiasi cha kutokuwa na matumaini tena? Hapana. Suala la Waisraeli kumkataa Kristo lilisababisha kusulubiwa kwake, ambao ulikuwa ni mpango wa Mungu wa wokovu. Katika mantiki hii, kukataa kwao kulisababisha kukubaliwa kwa Wamataifa. Wakati Wayahudi watakapowaona Wamataifa wakiokoka, wataelewa kwamba hata wao wanaweza wakaokoka kwa njia hiyo.

(11:12-15) Wamataifa watafaidika zaidi endapo Waisraeli watamrudia Mungu. Siyo muhimu kwa Mungu kuchagua kati ya Wayahudi na Wamataifa. Anataka awaokoe wote.

► Baadhi ya wanateolojia wanaamini kwamba kwa kuwa Mungu huchagua kutokuwaokoa baadhi ya watu, ameiondoa neema yake kwao, jambo linalofanya wasiwe na uwezo wa kuokoka. Je, utajibuje wazo hilo kutoka katika 11:12-15?

[68] Ona kumbukumbu katika Warumi 8:29

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 11:16-24 kwa ajili ya kikundi.

(11:16-24) Aya hizi zinatumia mfano wa kuchukua tawi la mti na kulipandikiza katika mti mwingine. Waisraeli walikuwa kama ni matawi yaliyokatwa kutoka kwenye mti wa Mungu, na Wamataifa kama matawi yaliyoongezwa kwenye mti huo, ambayo hayakuwa sehemu ya mti hapo awali. Wayahudi walikatwa kwa sababu ya kutoamini kwao. Mtu yeyote aliyeletwa katika mti huo atakatiliwa mbali pia kama hataendelea kuwa ndani ya imani katika mti huyo. Wale ambao walikataliwa mbali wanaweza pia wakarejeshwa tena.

Paulo hakusema kwamba Mungu huamua ni nani awe kwenye mti na kwamba uamuzi wake haubadiliki. Alisema kwamba Mungu huwaondoa wale watu ambao hawajaamini, lakini atawaingiza tena kama wakiamini. Wamataifa wanaoamini wanaingia, lakini watakatiliwa mbali endapo wataangukia kwenye kutoamini. Mungu huitikia kwenye chaguo la wanadamu wenyewe.

► Kutokana na aya hizi, jinsi gani ungeweza kuelezea mfano wa matawi yanayoongezwa au kuondolewa?

Hatari ya Kuachana na Wokovu

Ni muhimu kufahamu ni kitu gani Biblia inafundisha kuhusu usalama wa mtu aliyeamini. Biblia ina maonyo mengi mazito kwa ajili ya watu walioamini.

Katika Yohane 15:2-10 ni mfano uliokuwa maarufu sana wa mzabibu na matawi. Mfano huu unajibu baadhi ya maswali mengi.

Je, tunakaaje ndani ya Kristo? "Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu" (15:10). Kuacha kukaa ndani ya Kristo inamaanisha kwamba ni mtu aliacha kumtii yeye. Kisha, ni nini kinachotokea baadaye?

"Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea" (15:6). Kama mtu ataacha kutii na hapo akaacha kukaa ndani ya Kristo, atakataliwa. Mfano wa matawi yakianguka kutoka kwenye mzabibu kisha yakakusanywa na kutupwa motoni inaonyesha kukataliwa kabisa kwa kiasi ambacho hatuwezi hata kufikiria.

"Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu (15:4) "Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa" (15:2). Kuzaa matunda ni kuishi maisha yaliyobadilishwa, yaliyobarikiwa, na kuongozwa na neema ya Mungu. Kama hatutakaa ndani ya Kristo kwa njia ya utiifu, hatuwezi kuzaa matunda. ikiwa na maana ya kuishi maisha yaliyobadilishwa, yaliyobarikiwa, na yanayoongozwa na neema ya Mungu. Mtu asiyezaa matunda atakataliwa

Biblia haijatuambia mahali popote kwamba tutaendelea kuwa na wokovu bila kujali ni jambo gani tumefanya. Neema endelevu kwa kuishi kikristo inakuwepo kupitia uhusiano wetu na Mungu kwa njia ya Kristo. Kristo ni kama mzabibu ambao ni lazima tuendeleze maisha kutokea hapo. Mfano wa mzabibu unaonyesha kwamba kipawa cha wokovu kinapatikana

kwa njia ya uhusiano. Kutengwa kutoka kwa Kristo ni kutengwa kutoka kwenye wokovu. Tunadumisha huu uhusiano wa wokovu wetu kwa kumtii Mungu.

Glopu ya umeme na umeme wenyewe inaweza kwa mfano wa kisasa. Glopu ina mwanga wakati umeme unakuwa unatiririka ndani yake. Glopu haiwezi ikawaka kama itakuwa imezimwa kutoka kwenye chanzo chake cha kupata umeme. Vivyo hivyo, tunao uzima wa milele kwa kuwa tuna uhusiano wetu na Kristo. Uhai wake unatiririka ndani yetu. Hatuwezi kuuendeleza na kuudumisha uhai huo wa maisha kama tutajitenganisha kutoka kwake.

Maandiko yanatuonya kwamba mtu aliyeokoka anaweza akapoteza wokovu wake kama mwishoni atashindwa katika dhambi. "Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima (Ufunuo 3:5). Hawa walikuwa ni watu waliokuwa wameokoka, lakini bado wokovu wao utapotea kama watakuwa wameshindwa katika dhambi.

Wakati fulani, Paulo alikuwa na mashaka kwamba watu wake walioamini na kuokoka katika Thesalonike watakuwa wameachana na imani. Alisema kwamba kama hali hiyo itakuwa imetokea, kazi yao ya uinjilisti itakuwa haina faida (1 Wathesalonike 3:5). Hii inaonesha kwamba kuna uwezekano wa mtu aliyeamini kuanguka kabisa kutoka katika imani yake kiasi kwamba kuokoka kwake kutokea mwanzo hakuna faida tena.

Katika 2 Petro 2:18-21 tunaona kwamba kuna waalimu wa uongo ambao huwadanganya watu walioamini, yaani "wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo." Watu hawa waliokuwa wameamini walikuwa wameijua njia ya haki lakini wakaiacha. Andiko hili linasema kwamba ingekuwa afadhali wasingejua njia kuliko kurudi kwenye maisha ya dhambi. Hii inaonyesha kwamba inawezekana mtu kupoteza wokovu wake kwa kurudi tena dhambini. Kama ingekuwa haiwezekani kwa mtu aliyeamini kuupoteza wokovu wake, mtu hawezi kamwe kuwa mbaya zaidi kuliko kabla ya kuokolewa.

Mungu anataka watu walioamini wajisikie wako salama, lakini siyo kuwekeza hisia zao kwenye uhakika potofu au wa kudanganyika ambao unawaweka katika hali halisi ya hatari ya kiroho. Hatupaswi kuwaahidi watu walioamini kitu ambacho Mungu hajawahi kuwaahidi. Mungu hajawahi kutoa ahadi kwamba tutakuwa salama endapo tutapoteza wokovu wetu kutokana na lolote lile tutakalolitenda.

Mungu anaahidi kuwa pamoja nasi, kutuongoza, na kutupa uwezo wa kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi. Anaahidi kwamba tutapokea maisha ya kiroho kutokana na uhusiano wetu pamoja naye. Mtu aliyaeamini anaweza kuishi bila hofu ndani ya ahadi ya Mungu ya neema endelevu ambayo mwamini hupokea akiwa kwenye mahusiano na Mungu.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 5, kifungu cha 3

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(11:25-29) Israeli kama taifa (Waisraeli wote) wataokoka. Hii haimaanishi kwamba kila Myahudi binafsi ataokoka, lakini kwa muda wa mbele baadaye masalia wa imani katika taifa

hilo watamgeukia Mungu. Ukamilifu wa watu Wamataifa umeelezwa katika Luka 21:24. (Taarifa nyingine kuhusiana na wokovu kwa Waisraeli kama taifa unapatikana katika Isaya 2:2-5, Isaya 60:1-22; Zekaria 12:7-13:9).

(11:30-31) Ona maelezo katika 11:11.

(11:32) Mungu amewaweka katika kundi moja wote kama watu wasioamini walioko katika hali moja. Mungu amehukumu wote na kutamka hukumu juu yao, ili wawe ni stahiki sawa ya kuwarehemu. Neno *wote* limetumika mara mbili katika aya hii. kuwa watu wote walivyo ni wenye dhambi, Mungu anataka awarehemu wote. Kama vile alivyowahukumu wote, ametoa rehema zake kwa wote.

Watu wote wamewekwa katika kundi moja linalofanana ili kwamba waweze kupokea wokovu unaofanana (Ona Warumi 3:19-23). Jambo la muhimu hapa ni kwamba amewaweka watu wote chini ya hukumu ili kwa njia hiyo hiyo, aweze kutoa rehema kwa watu wote.

(11:33-36) Aya hizi ni mshangao wa sifa kwa ajili ya hekima ya Mungu. Mpango mkubwa wa wokovu uko juu ya uwezo wetu kiasi ambacho hatungeweza kubuni. Tunapaswa tuupokee katika njia ile ambayo yeye mwenyewe anataka kutupa sisi, kwa sababu hatudai chochote (11:35). Watu wengine wanakwazwa na mpango wa Mungu wa wokovu, kama vile ni mwamba unaoleta kizuizi; lakini ndio jiwe kuu la msingi la rehema.

Mpango wa Mungu kwa Vipindi Maalumu (Dispensationalism) dhidi ya Teolojia ya Agano

Wanateolojia wamejaribu kuelewa uhusiano ulioko baina ya Israeli na Kanisa.

Maswali yenyewe ni pamoja na haya: Je, Watu waliokuwepo wakati wa Agano la Kale walikuwa wanaokoka kwa njia tofauti na wanavyookoka watu wa Agano Jipya? Je, ahadi za Mungu kwa Israeli zinatumika pia kwa Kanisa? Je, Israeli bado ni maalum katika mpango wa Mungu?

Mojawapo ya uhusiano kati ya Israeli na Kanisa umekuwa ukiitwa "Mpango wa Mungu." Wanateolojia wengine wamekataa kukubaliana kwamba ni "Mpango wa Mungu" na wamekuza maelezo mengine ambayo wakati mwingine wamekuwa wakiita "Teolojia ya Agano."

Mpango wa Mungu katika kipindi maalumu.

Mpango wa Mungu katika kipindi fulani maalumu unatokana na dhana kwamba kuna vipindi tofauti vya historia ya mwanadamu ambapo Mungu anashughulika kwa njia tofauti na watu, akitoa wokovu kupitia njia tofauti. Muda ambao Mungu anatumia mpango maalumu wa wokovu ndio unaoitwa Mpango wa Mungu katika kipindi fulani maalumu.

Baadhi ya wale wanaoamini katika mpango wa Mungu katika vipindi maalumu wanagawa historia ya mwanadamu katika vipindi maalumu. Vipindi viwili ambavyo vinaathiri sana

tafsiri ya Biblia viko kwenye msingi wa tofauti kati ya Israeli na Kanisa. Waisraeli wa Agano la Kale waliokoka kufuatana na sheria ya Musa na utaratibu wa utoaji wa dhabihu mbalimbali; Waamini wa Agano Jipya wanaokolewa kwa neema kwa njia ya imani. Kanisa ni tofauti sana na Israeli, na Mungu hushughulika nao kwa pamoja kwa njia tofauti.

Ingawa kuna tofauti nyingi za dhana ya mpango wa Mungu katika vipindi maalumu, wale hasa wenye dhana hii wanafundisha kuwa ahadi zote za Mungu kwa Israeli kuhusu ardhi na ufalme zitatimizwa kiuhalisia.

Watu wanaoamini katika mpango wa Mungu katika vipindi maalumu wanafikiri kwamba mipango yote haiwezi ikafanyika kwa wakati mmoja katika dunia; kwa hiyo, wanaamini kwamba Kanisa litaondolewa duniani kwa kipindi cha miaka saba. Katika kipindi hicho, Israeli watamkubali Yesu kama Masihi wao. Baada ya kipindi hicho, kutakuwepo na kipindi kingine cha miaka 1,000 ambacho Yesu atatawala akiwa Yerusalemu.

Wanaoamini katika kipindi fulani maalumu wanalifanya Agano la Kale lisiwe na nguvu ya kutumika kwa Wakristo kwa sababu wanaamini kwamba lilikuwa limeelekezwa kwa Waisraeli tu katika kipindi kingine maalumu tofauti. Wanatumia taarifa zilizoko kwenye Agano la Kale kuelezea ukweli uliopo, lakini mara nyingi hukataa ushahidi wa mafundisho ya imani kutoka katika Agano la Kale na wanajaribu kufuata tu Agano Jipya.

Watu wengi ambao hawana ufahamu wa Mpango wa Mungu katika kipindi fulani maalumu wamekuwa wakishawishika na mawazo yake. Mara nyingi watu hukataa kukubali mamlaka ya Agano la Kale, ingawaje waandishi wa Agano Jipya kwa uhalisi walilichukulia kama ndio mamlaka yao.

Teolojia ya Agano

Kwa mujibu wa teolojia ya agano, watu wa Mungu ni wale ambao wanampenda Mungu na kumtumikia, bila kujali wanaishi katika kipindi gani cha historia. Watu waliookoka, aidha kwenye nyakati za Agano la kale au Agano Jipya, wanachukuliwa ni wale waliotubu na kumwamini Mungu kwa ajili ya wokovu.

Kwa mujibu wa teolojia ya agano, Kanisa kwa sasa ni watu wa Mungu na wanapokea ahadi zinazotolewa kwa ajli ya watu wa Mungu, ikiwa ni pamoja na ahadi zilizotolewa kwa Israeli Katika Agano la Kale. Taifa la Israeli kwa kipindi hiki halina umuhimu wowote maalumu.

> Maana yeye si Myahudi aliye Myahudi kwa nje tu, wala tohara siyo ile ya nje tu katika mwili; bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani, na tohara ni ya moyo, katika roho, si katika andiko; ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu (Warumi 2:28-29).
>
> Fahamuni basi, ya kuwa wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu. Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani, lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, Katika wewe Mataifa yote

watabarikiwa. Basi hao walio wa imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu aliyekuwa mwenye imani (Wagalatia 3:7-9).

ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani (Wagalatia 3:14).

Hapana Myahudi wala Myunani… Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi (Wagalatia 3:28-29).

Kwa mujibu wa teolojia ya agano, ahadi hizi zitatimizwa kwa kanisa badala ya Israel:

- Kiti cha kifalme cha Kristo kuanzishwa Yerusalemu,
- Amani
- Israeli kama kiongozi wa dunia
- Mataifa yote kufundishwa na Israeli
- Kumilki wa milele wa nchi ya ahadi, upole wa wanyama pori.

Ahadi zote zilizotolewa kwa Israeli zimetafsiriwa kuwa na maana ya kiroho, badala ya maana halisi ya kawaida. Ahadi hizi lazima zitimizwe kwa faida ya kiroho ili zitimie kwa kanisa.

Watu wengi ambao wanaamini teolojia hii hawaamini katika utawala wa kawaida wa Kristo duniani kwa kipindi cha miaka elfu moja. Wanaamini kwamba Kristo na watakatifu wanatawala sasa kiroho kupitia ushawishi wa injili. Wanaamini kwamba ahadi kwa Ibrahimu kwamba wazao wake wataimiliki Kanani milele inakamilishwa sasa na watu walioamini na kuupokea wokovu.

Kwa mujibu wa teolojia ya Agano hakuna umuhimu wowote wa Israeli katika kipindi hiki cha sasa, kwa sababu walimkataa Kristo. Wayahudi wanaweza kuwa sehemu ya watu wa Mungu kwa kupokea wokovu binafsi, kama ilivyo kwa Wamataifa.

Uwezekano wa tafsiri nyingine

Wanateolojia wengi kwa wakati wa sasa wamejaribu kuja na mtazamo wa uwiano baina ya Mpango wa Mungu katika kipindi fulani maalumu na teolojia ya agano.

Kuna matatizo kwenye Mpango wa Mungu katika kipindi fulani maalumu. Mtume Paulo alimwambia Timotheo kwamba Maandiko ya (Agano la Kale) yalifundisha wokovu (2 Timotheo 3:15). Yesu alisema kwamba Nikodemo tayari alishajua juu ya kuzaliwa mara ya pili kwa sababu alikuwa mwalimu wa Agano la Kale (Yohane 3:10). Agano Jipya linasema kwamba mtu aliyeamini kwa sasa ni Mwisraeli wa kweli na mtoto wa Ibrahimu (Warumi 2:28-29, Wagalatia 3:28-29). Linasema pia kwamba dhabihu za Agano la Kale hazikuwa na uwezo wa kuondoa dhambi (Waebrania 10:4). Maandiko haya yanadhihirisha kuwa Mungu hajatoa njia tofauti za wokovu katika vipindi tofauti vya kihistoria.

Kuna matatizo pia kwenye teolojia ya agano. Kusema kwamba ahadi za Agano la Kale zinakamilishwa kiroho ni kuruhusu tafsiri za kufikirika ambazo haziwezi kukidhi majaribio. Pia, tafsiri hii inapoteza maana halisi ya tafsiri ya asili. Ingekuwa ni jambo lisilowezekana

kwa Ibrahimu au watu wengine kuzielewa ahadi, ingawaje walifikiria kwamba walikuwa wanajua. Kwa mfano, Mungu alimwahidi Ibrahimu kwamba wazao wake watamiliki ardhi fulani milele; je hiyo inaweza ikamaanisha kwa kwamba Wamataifa wanaweza wakaokoka?

Teolojia ya agano inakataa kwamba Israeli bado muhimu kwenye mpango wa Mungu, lakini mtume Paulo alisema kwamba Waisraeli kama taifa siku moja wataokoka (Warumi 11:26).

Mtazamo wa uwiano wa Israeli na Kanisa utajumuisha ufahamu wa ahadi mbalimbali katika Agano la Kale:

1. **Ahadi za Wokovu.** Wokovu ni kwa neema na unapatikana kwa kutubu na imani ikiwa ni kwa Myahudi au mtu wa Wamataifa katika kipindi chochote cha historia. Msingi wa Mungu kumkubali mtu binafsi ulikuwa siku zote unafanana (Warumi 4:3, Waefeso 2:8). Hakuna haja kwa Israeli na kanisa kuwa na utengano hapa duniani kwa sababu wokovu unafanana kwa wote.

2. **Ahadi za Mungu za utunzaji wa watu wake.** Ahadi nyingi zinaelezea njia za kawaida za Mungu za kuwatunza watu wake, kwa yeyote ambaye yuko kwenye uhusiano wa utii na yeye. Mfano mzuri ni Zaburi ya 23. Ahadi hizi zinaonyesha asili ya Mungu Iliyofunuliwa katika uhusiano. Kanuni hizi zina matumizi yake wakati wowote na mahali popote kwa Israeli au kwa Kanisa.

3. **Ahadi kwa Israeli kama Taifa.** Yesu alikuwa ni Masihi kwa Wayahudi. Siku moja Israeli kama taifa litamgeukia Kristo (Warumi 11:26). Ahadi ambazo Mungu alizitoa kwa ajili ya taifa la Israeli zitaenda kutimia kama kawaida kwa ajili ya masalia ya Wayahudi walioamini.

► Je, ni taarifa gani kwenye maelezo ya uwiano yanayoendana na Mpango wa Mungu katika kipindi fulani maalumu, na ni taarifa gani zinazotofautina katika hiyo? Ni taarifa gani zinaendana na teolojia ya agano na ni zipi zinayotofautiana nayo?

Maswali ya Mapitio Somo la 10

(1) Je, jambo kuu katika Warumi 10 ni nini?

(2) Je, ni jinsi gani Wayahudi walijaribu kujihesabia haki?

(3) Je, tunajuaje kuwa watu walioishi kabla ya Kristo kuja walikuwa hawaokolewi kwa njia ya matendo?

(4) Je, ina maana gani kuwa wokovu uko mioyoni na midomoni mwetu?

(5) Je, ni kwa nini ujumbe wa mishenari ni wa haraka?

(6) Elezea mfano wa matawi ya mti katika Warumi 11.

(7) Orodhesha aina tatu za ahadi za Agano la Kale.

Kazi ya kufanya Somo la 10

(1) Andika ukurasa mmoja ukielezea ni kwa nini wakati wa leoa Agano la Kale ni muhimu kwa ajili ya Wakristo. Onyesha mifano iliyoko kwenye Maandiko ya Agano la Kale ambayo yana thamani hasa.

(2) Kumbuka kutoa taarifa ya mazungumzo yako na angalao watu wawili kutoka katika makanisa mengine.

Somo la 11
Huduma na Mahusiano

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 6

Sehemu ya 6 ya Warumi (12:1–15:7) ina maelekezo mengi ya vitendo kwa ajili ya maisha ya kanisa, huduma, mahusiano ya Kikristo, na mahusiano na serikali.

12:1-2 inatambulisha sehemu ya 6, ikituambia kwamba tunapaswa kujitoa kabisa kutumika kwa ajili ya Mungu. Hii inafuatia kutoka maelezo ya Paulo katika sura iliopita: Kwamba tuna deni kwa kila kitu kwa Mungu (11:35), na kwamba njia za Mungu ni za hekima kabisa (11:33).

Paulo anatumia mfano wa dhabihu iliyo hai (12:1). tumejitolea kabisa kama dhabihu inayopaswa kuuawa, lakini badala ya kufa, tunaishi kwa ajili ya Mungu. Hiyo ina maana kwamba msimamo huo ni lazima uzingatiwe. Siku hadi siku ni lazima tukatae kuondoka katika uaminifu wetu. Mfano wa dhabihu iliyo hai unasisitiza kujitoa kwetu kabisa kama sadaka. Hatuwezi tukahifadhi sehemu ya maisha yetu kwa ajili yetu wenyewe nje ya mapenzi ya Mungu. Hatuwezi kulinda baadhi ya matamanio au matarajio kutokana na madai ya kujitolea kabisa kwa Mungu.

Kujitolea huku binafsi kama dhabihu iliyo hai ni ibada ya kiroho, tofauti na mapokeo tu ya dini.[69]

Huduma ya kujitolea kabisa haitawezekana bila ya kuwepo na mabadiliko yaliyoelezwa katika 12:2. Ni lazima tubadilishwe kwa kufanywa upya nia zetu. Hatupaswi kuifuatisha dunia hii katika maadili yake, tabia zake, au maoni yake. Mtu anayetafakari kila swali katika mustakabali wa mapenzi makamilifu ya Mungu atatofautiana na dunia. Hatatoa ruhusa kwa matamanio yeyote ya dhambi; hawezi akayavumilia kana kwamba ni mambo ya kawaida tu.

Tambua kwamba mwili unapaswa uwe mtakatifu. Dhambi siyo kipengele muhimu cha mwili ambacho hakiwezi kutakaswa na Mungu. Mwili siyo wenye kuwa na dhambi wenyewe na hauwezi kutenda dhambi pasipokuwa na mapenzi binafsi ya kufanya hivyo lakini unaweza kutumiwa katika kutenda dhambi.

Aya za kutoka 12:1-15:7 zinaelezea jinsi ya kuishi maisha ya kujitolea kabisa na yaliyobadilishwa.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 12 kwa ajili ya kikundi.

[69] Ona maelezo ya kumbukumbu yaliyoko katika Warumi 1:9.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, kifungu cha 1

Maelezo ya aya kwa aya

(12:3) Neema iliyotolewa kwa Paulo inarejaea mamlaka yake ya kitume na kipawa cha ufunuo.

Tunapaswa kunyenyekea kwa sababu kila tulicho nacho tumepewa na Mungu. Mtu aliye na karama za kiroho anapaswa awe mnyenyekevu akitambua kwamba karama hizo zinatoka kwa Mungu bila malipo na ziko kwa kusudi la kutumikia watu wengine.

(12:4-5) Kama vile katika mwili mmoja, tunawahitaji wengine na tuna wajibu wa kuwahudumia watu wengine. Mfano wa mwili unaelezwa katika 1 Wakorintho 12:12-26.

(12:6-8) Aya hizi zinataja huduma mbalimbali. Kila mtu aliyeamini anapaswa kufuata huduma aliyoitiwa na aliyozawadiwa. Kama mtu hana unyenyekevu wa neema, anaweza akatumia muda na nguvu zake nyingi kwa njia iliyo mbaya, (labda akitafuta kupata kibali cha mwanadamu), na akashindwa katika wito wake halisi.

Fedha ya Kirumi

Fedha ya Kirumi ilikuwa inatumika kwenye utawala wa Kirumi, na hata katika Yerusalemu. Iliwezesha uthabiti wa kiuchumi na kiwango cha thamani ambacho kilisaidia biashara kufanikiwa. Yesu alitoa kielelezo kwa kutumia sarafu iliyokuwa na sura ya mfalme. (Luka 20:24).

Watu walio na karama za kiroho wanaonywa wazitumie vizuri. Kwa mfano, mtoaji atoe bila vikwazo, na siyo kwa kusudi la kujipatia heshima yeye mwenyewe. Mwenye kusimamia lazima awe na bidii – makini kwenye mambo ya msingi na yanayotegemewa wakati wote. Mtu anayesaidia watu wengine katika mahitaji yao hapaswi kufanya hivyo kwa kiburi au mtazamo wa chuki ambao humdhalilisha mpokeaji.[70]

► Je, ni kwa jinsi gani Wakristo wanatumia karama zao za kiroho tofauti na jinsi watu wa dunia wanavyotumia uwezo wao?

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, Kifungu cha 2

Maelezo ay Aya-kwa-Aya

(12:9) Pendo lisiwe na unafiki bali liwe katika ukweli na uaminifu. Lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema. Kuongezeka kwa upendo kumeunganishwa na kuboreka kwa ufahamu kuhusu ni jambo gani lililo jema (Wafilipi 1:9-10).

[70] Picha: "Roman coin hoard: 1 Gold solidus of Valentinian I", imepatikana kutoka The Portable Antiquities Scheme/The Trustees of the British Museum, https://finds.org.uk/database/images/image/id/1023830/recordtype/artefacts, imepewa leseni chini ya CC BY 2.0, imeshushwa rangi na kukatwa kutoka kwenye asili.

(12:10) Kanisa ni familia ya Mungu, ikiwa na ndugu wengi. Tunapaswa tuwe tayari kwa heshima kwenda kutembelea wengine badala ya sisi wenyewe tu.

(12:11) Tusiwe walegevu kwenye majukumu yetu. Mkristo anapaswa awe mfano wa kuigwa kwenye maadili mazuri ya kazi. Hapaswi awe na muda mwingi wa kupoteza kama anaishi kwenye kusudi la Mungu. Anapaswa awajibikie majukumu kama anayefanya kazi kwa ajili ya Mungu (Waefeso 6:6-7).

(12:12) Furaha yetu haitegemei hali tulizo nazo, kwa sababu tunayo matumaini kwa ajili ya uzima wa milele. Kuwa mvumilivu maana yake ni kuvumilia katika imani. Mtu ni lazima awe na tabia isiyobadilika ya kumtegemea Mungu, na awe tayari kuomba wakati wote.

(12:13) Kusaidia watu wengine walioamini katika haja za mahitaji yao ya kimwili. Ukarimu maana yake ni kukutana na mahitaji ya watu wengine kwa ajili ya chakula na malazi.

(12:14) Usiwatendee watu wanaokuudhi kama wanavyostahili, lakini watendee kama ambavyo Kristo angewatendea. Kuwafanyia watu kile kitu ambacho unafikiri ndicho wanachostahili ni kuhukumu kwa kiwango kikubwa, ambalo ni jukumu la Mungu lililohifadhiwa.

(12:15) Kuwa tayari kushiriki huzuni pamoja na wanaolia, na vivyo hivyo kushiriki furaha pamoja na wengine wafurahio.

(12:16) Usiwe ni mtu wa kusumbuka na vyeo. Tusiwe na upendeleo kwa watu wa daraja la juu la mafanikio. Kuwa mwenye heshima hata kwa watu ambao ni maskini. Usitafute njia nyingine za kujiweka juu ya watu wengine.

(12:17) Siyo jambo sahihi kumwumiza mtu mwingine kisa tu kwa sababu amekuumiza wewe. Hatujaitwa kwa ajili ya kuwapa watu adhabu au kulipa uovu kwa uovu bali kusamehe.

Onesha kwamba wewe ni mwaminifu. Kama unataka uheshimiwe, dumisha sera ambazo zinaonyesha uaminifu kwa kila mtu kuona. Haitoshi wewe na Mungu kujua kwamba wewe ni mwaminifu. Ni rahisi zaidi kudumisha sifa nzuri kuliko kuijenga upya baada ya kuwa imeharibika.

(12:18) Kwa kiwango chochote kile ambacho kitakutegemea wewe, ishi kwa amani na kila mtu. Amani inapokuwa mahali pake halisi inakuwa ni uhusiano wenye mpangilio mzuri. Wakati mwingine amani inahitaji msamaha, hata kwa kosa lisilo la kukusudia. Mara nyingine inahitajika upendo kukabiliana na mtenda maovu, ili kwamba kile kinachozuia uhusiano wako kiweze kutatulika. Aidha kama utakataa kuomba msamaha au kukabiliana inapokuwa inahitajika, maana yake haufanyi kile kinachowezekana katika kudumisha amani.

(12:19) Msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu. Kama mtu anataka awe ndiye mlipiza kisasi, inaonesha hajaamini kwamba Mungu anaifanya kazi yake kwa njia sahihi.

(12:20) Fanya mambo yaliyo mema kwa watu wengine, kuliko kujaribu kuwafanyia mambo wanayostahili kutoka na yale waliyokutendea. Kupalia makaa ya moto kichwani haimaanishi

ni kulipiza kisasi kwa njia ya hila zaidi, kwa kuwa mtazamo huo utachanganya jambo kuu lililoko kwenye aya hii. Kwa kufanya hivyo, itawezekana ikawa ni ishara itakayoweza kuuyeyusha moyo na mwenendo wa huyu mtu.

(12:21) Usishindwe na ubaya hata ukatoa nafasi ya kushindwa kiroho. Hata hivyo, usitake kushinda ubaya kwa mabaya, bali ushinde ubaya kwa wema. Kuwa na uchungu na kutaka kushinda kwa njia ya ubaya ni hali ya kushindwa kiroho, hata kama utashinda katika mgogoro huo.

► Jaribu kufikiria kuhusu jinsi ambavyo mtu hataweza kufanya vizuri katika maelekezo haya kama hajajitoa kabisa kwa Mungu. Je, ni kitu gani katika maisha yako unategemea kiwe na mabadiliko kutokana na maelekezo haya?

Kutafsiri Barua za Mtume

Barua za Paulo ziliandikwa kukidhi hali maalumu zilizokuwepo: Kwa kawaida hali yenyewe inaweza ikawa ni aina fulani ya tabia ambayo ilihitaji irekebishwe, au kosa la mafundisho ya imani ambalo lilihitaji maboresho yaliyo sahihi, au kutokuelewana ambako kulihitaji mwanga zaidi."[71] Barua zenyewe haziko katika mfumo wa teolojia inayofuata utaratibu fulani, bali teolojia iliyotokana na kukabiliana na hitaji, Teolojia hii ni ya vitendo kutokea mwanzo. Haijaanzishwa na kutengwa ikae upweke kutoka katika maisha halisi.

Nyaraka za Agano Jipya hazikuwa ni maandishi yaliyoandikwa kwa ajili ya jamii yote kwa ujumla wake, bado yalikusudiwa kwa zaidi ya wapokeaji mmoja na kwa zaidi ya maombi ya papo hapo. Paulo aliwaamba Wakolosai kwamba wanapaswa wabadilishane hizo nyaraka ili zisomwe pia na Walaodikia na hii iwe ni kwa kila waraka uliopokelewa kutoka kwake (Wakolosai 4:16). Mapema kabisa kanisa lilikuwa limeanza kukusanya nyaraka za Paulo na kuzisambaza kwa pamoja. Kwa hiyo, tunajua kwamba waliziona hizo nyaraka zikiwa zinafaa kutumika kwa kanisa katika maeneo yote na kwa nyakati zote.

Ingawaje kuna pengo la muda na utamaduni lililopo kati yetu sisi na wapokeaji wa mwanzo, nyaraka hizi ziliandikwa kwa ajili ya Wakristo wa Agano Jipya waliokuwa wanakabiliwa na matatizo yanayofanana na ya kwetu tuliyo nayo. Kwa hiyo, nyaraka za Paulo ni rahisi kutumika kwenye kanisa la sasa kuliko aina nyingine zozote za maandishi au fasihi kutoka katika Maandiko. Nyaraka hizi hazikuandikwa mahususi kwa ajili ya taifa la Kiyahudi, au hazikuelekezwa kwa watu waliokuwa chini ya sheria ya Agano la Kale.

Hali ya asili ya mwanzo ya uandishi inampa mtafsiri mahali pa kuanzia kwa ajili ya matumizi ya wakati huu wa sasa. Kanuni ya kutafsiri ni kwamba tunaweza tukaelewa maandishi vizuri zaidi kama tutamjua ni nani mwandishi, nani alipokea, na kwa nini kiliandikwa. Nyaraka zinampa mtu anayetafsiri faida ya kujua utambulisho wa mwandishi na wapokeaji wake.

Kitabu cha Warumi ndicho kilicho mahususi na rasmi zaidi katika maandishi ya Paulo. Kinafuata mtiririko uliopangika. Takribani kitabu chote kiko katika tasnifu ya kiteolojia.

[71] Gordon Fee and Douglas Stuart, *How to Read the Bible for All Its Worth*, (Grand Rapids, MI: Zondervan, 1993) 48.

(Maandiko au makala zenye kuhusu mada moja.) Paulo hakutaja makosa maalumu katika kanisa la Rumi. Hakuzungumzia kuhusu hali zozote maalumu, kama alivyofanya kwenye nyaraka zake kwa makanisa mengine aliyokuwa ameyaanzisha na kuyatembelea.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, Kifungu cha 3

Jambo Kuu katika Warumi 13:1-7

Watu walioamini wanapaswa wazitii serikali za kiraia kwa sababu serikali zimewekwa na Mungu.

Maelezo kwa kiongozi wa darasa: Pengine kutakuwepo na mjadala zaidi na kutokukubaliana kadri kikundi kitakapokuwa kwenye mafunzo ya kifungu kitakachofuata. Unatakiwa awatake kikundi chako kiruhusu kifungu kisahihishe maoni yao.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 13:1-7 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(13:1-2) Mungu alianzisha serikali. Hiyo haina maana kwamba kila mtawala ni mwenye haki, lakini Mungu anataka mamlaka ya binadamu ianzishwe. Kukataa kuwa chini ya mamlaka ya binadamu ni kumwasi Mungu. Kama vile ambavyo kiukweli tunakuwa hatumpendi Mungu pale tunapokuwa humpendi ndugu tunayemwona, vivyo hivyo hatuwezi tukadai kwamba tuko chini ya mamlaka ya Mungu wakati huku tunakataa kujiweka chini ya mamlaka ya binadamu inayoonekana. Mkristo hapaswi kuwachukulia vibaya watawala wa kisheria kwa kuwavunjia heshima.

(13:3-4) Moja ya kusudi la serikali ni kuwaadhibu watenda maovu. Wakati serikali inapofanya kazi yake kwa ukamilifu, watenda maovu hupata hofu. Katika mazingira ya kawaida Wakristo hawapaswi kuleta mgogoro na serikali kwa sababu sifa ya Ukristo inamfanya Mkristo awe raia mwema. Hata hivyo, mara nyingi katika historia, watawala wamekuwa wakijaribu kudai kupewa heshima ambayo anastahiki Mungu peke yake, na kisha hugeuka kuwa watesaji wa Wakristo.

Serikali ambayo inafanya kazi vizuri na katika misingi ya haki na usawa, iko sawasawa na mamlaka ya Mungu. Aya ya 4 inatuambia kwamba serikali ina mamlaka kutoka kwa Mungu katika kuimarisha sheria ikibidi hata kama ni kuwanyonga watenda maovu.

Wakristo katika baadhi ya Wamataifa duniani wanaamini kwamba ni makosa kwao kuwa na nafasi yeyote ya uongozi katika serikali, hasa nafasi ambayo itaweza kuhitaji wao kutumia nguvu. Wakristo wengi walio na imani hiyo wanaishi katika nchi ambazo serikali zimewatesa na kuwauwa Wakristo na zimesheheni watawala wala rushwa. Hata hivyo, kama serikali inafanya kazi vizuri na katika misingi ya haki na usawa, siyo kosa kwa Mkristo kutumikia nafasi katika serikali kwa sababu serikali imethibitishwa na Mungu.

(13:5) Mkristo anapaswa aitii mamlaka iliyo kuu siyo kwa sababu ya kuogopa ghadhabu ya serikali, bali kwa ajili ya dhamiri nyeupe. Kufanya uasi dhidi ya serikali au kukataa kutii

sheria zake ni sawa na kukataa jukumu la serikali. Siyo maamuzi yote yatakayoweza kuamuliwa na watu binafsi ikibidi kuwepo na serikali ya aina yeyote. Uhuru wa mtu binafsi ni lazima uwe chini ya mamlaka ya serikali ambayo inapaswa ilinde haki za watu binafsi, hata kama siku zote hatukubaliani na jinsi ulinzi wa uhuru wetu unavyofanyika.

(13:6-7) Mkristo anapaswa kulipa kodi halali za serikali. Fuata njia za kitamaduni za kuonyesha heshima.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, Kifungu cha 4

Jambo Kuu katika Warumi 13:8-10

Upendo hukamilisha sheria kwa sababu inamhamasisha mtu aliyeamini kufanya kile kilicho cha haki kwa ajili ya watu wengine.

Aya hizi zinathibitisha kwamba sheria haziwezekani zikawa hazina maana kwa mtu aliyeamini. Mtu aliyeamini hutimiza sheria, kwani kwa neema anaweza kuwa na upendo unaoelezwa hapa. Neema haiko kwa ajili ya kufunika uvunjaji wa sheria. Neema inachanganya kwa pamoja kazi ya Mungu ndani yetu ili kukamilisha mapenzi yake ndani yetu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 13: 8-10 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(13:8) Kuwiwa deni katika mantiki hii ni kushindwa kutoa kile ambacho unadaiwa na mtu mwingine. Baadhi ya aina za majukumu zimeorodheshwa kwenye aya iliyotangulia. Siyo kosa kukopa na kulipa katika muda muafaka, kama hiyo ndiyo njia inavyoonekana inafaa katika kukamilisha majukumu yaliyopo. Tunaagizwa, kama ilivyo katika aya ya 7, kumlipa kila mtu haki yake kadri tunavyowiwa kutoka kwetu.

► Je, kunakuwepo na matokeo gani wakati Mkristo anaposhindwa kulipa deni alilokopa?

(13:9-10) Kama kweli unampenda mtu mwingine kama unavyojipenda mwenyewe, hutaweza kumwibia, kumdanganya, kutamani kile alicho nacho, au kumvurugia ndoa yake. Urafiki na upendo tu wa kawaida, kama vile ulivyo wa kawaida katika dunia hii, siku zote haviwezi kuzuia matendo haya maovu; lakini upendo wa Kristo ndani yetu utatuzuia sisi katika kutenda maovu hata kwa wageni, kwa wale wanaotuudhi, au kwa wale wanaoweza kutufanyia maovu dhidi yetu.

Tamaduni nyingi na madhehebu hufundisha kwamba tunadaiwa kiasi cha upendo, labda katika familia zetu na jamii zetu katika kabila. Lakini wanafikiri kwamba kwa wanadamu wengine wote waliobakia, hakuna upendo wa aina yeyote unaodaiwa. Wanaweza wakaona ni ruhusa kuwaibia wageni au waajiri wao na kuwa wakatili kwa watu wasiowajua.

Kristo anatuagiza sisi kuuendeleza upendo wetu kwa kila mtu tunayejikuta tuko naye.

Katika Luka 10:25-37, ili kuonyesha mfano wa jinsi ya kumpenda jirani yako, Yesu alielezea mfano wa Msamaria aliyemsaidia Myahudi aliyeumizwa.

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, Kifungu cha 5

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 13:11-14 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ay Aya-kwa-Aya

(13:11) Wokovu kwenye aya hii ni marejeo ya wokovu wa mwisho wakati wa kuja kwake Kristo. Hatupaswi tuishi kana kwamba dunia hii itadumu milele. Tunatakiwa tuishi kama watu wanaotegemea kwamba mambo yaliyopo yatapita upesi sana.

(13:12) Usiku ni msemo ambao unaelezea wakati unaoelekea kwenye kuja kwa Kristo (Ona pia 2 Petro 1:19). Giza kwa mujibu wa Agano jipya ni kuhusika katika matendo ya dhambi (Ona pia 1 Wathesalonike 5:4-8 na Waefeso 5:11-14).

(13:13) Hapa maisha ya mwenye dhambi mzembe yanaelezwa. Huyu ni mtu ambaye hajali lolote kuhusu wakati ujao, na zaidi sana hafikirii jambo lolote kuhusiana na umilele. Anaishi maisha ya kujifurahisha bila kujali mambo ya maadili. Maisha ya Mkristo ni kinyume kabisa na mambo hayo.

(13:14) Usiruhusu mambo ya tamaa mbaya yakuingilie. Usitumie asili yako ya ubinadamu kama kigezo cha kuomba radhi kwa ajili ya kutenda dhambi. Ishi kwenye maisha ya nuru na usiruhusu chochote kipenyeze ndani yako ambacho kitakuaibisha.

Kifungu cha Kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, Kifungu cha 5

Wakati wote kutakuwa na masuala ya muhimu ambayo waamini watatofautiana. Warumi sura ya 14 inatoa maelekezo kuhusu jinsi wakrsito wanaotofautiana katika baadhi ya mambo wanayoamini na wanayoyaishi lakini bado wanatakiwa kupendana na kuheshimiana, kuabudu na kutumika pamoja.

► Mwanafunzi anapaswa kusoma Warumi 14:1-23 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ay Aya-kwa-Aya

(14:1) Ndugu mdhaifu ni yule anayejihisi kuwa na hatia katika kitendo ambacho kiuhalisisia hakijawahi kukatazwa na Mungu (ona 1 Wakorintho 8:7-12). Ndugu aliye na nguvu ni yule anayafanya kitendo bila kujihisi kuwa na hatia kwa sababu anajua kwamba kitendo anachokifanya kiuhalisia hakihusiki kabisa katika kukosa utii kwa Mungu.

(14:2-3) Sheria ya Kiyahudi ilikuwa imeunganishwa na masharti yaliyohusiana na mambo ya vyakula. Katika kanisa kulikuwepo na Wakristo wengi wa Kiyahudi na Wamataifa ambao walikuwa wameshajifunza kuhusu sheria za Kiyahudi. Mtu aliyekuwa anajisikia yuko huru kutokana na vizuizi vya aina yeyote vilvyohusiana na mambo ya vyakula alikuwa anaweza kushawishika kumnyanyasa mtu mwingine ambaye alijihisi hana uhuru wa kula aina fulani ya chakula na anajisikia kimekatazwa. Yule anayejaribu kufuata sheria kuhusu mambo ya

vyakula anaweza akashawishika kuwahukumu wasiofungamana na sheria hiyo kama wenye dhambi.

(14:4) Mungu atawahukumu watumishi wake mwenyewe na kuwapatia ile neema wanayohitaji. Usiwahukumu watu wengine kwa mambo ambayo hayako wazi kwenye Maandiko.

Duniani kote kuna tofauti kati ya watu walioamini kuhusiana na mambo kama ya ubatizo, jinsi ya kuhudumia Meza ya Bwana, chaguo la tafsiri ya Biblia, mavazi, na sherehe. Ndani ya mwili wa Kristo, tunapaswa kudumisha umoja wa Kikristo lakini tusitazamie kila mtu kuwa sawa na mwenzake. Dhima yetu inapaswa iwe: "Katika mambo ya msingi, umoja; katika mambo yasiyokuwa ya msingi, uhuru; lakini katika mambo yote, upendo!"

(14:5-6) Kulikuwa na siku nyingi za kuadhimisha sherehe za Kiyahudi, zikiambatana na tamaduni maalumu kwa kila moja. Kuhusiana na siku ya Sabato hili pia lilikuwa ni suala lililoleta utata. Badala yake kanisa lilianza kukutana na kuabudu katika Siku ya Bwana (Mdo 20:7; 1 Kor 16:2; Ufu 1:10) na baadaye jumapili ikazoeleka kuwa kama sabato ya kikristo. Kanuni ya mapumziko kwenye siku ya Sabato hata sasa ina faida zake ambazo ni wajibu wetu tuzitunze, kwa kuwa ni kanuni ya uumbaji na siyo tu utamaduni ulioanzishwa wakati ilipotolewa sheria ya Musa.

"…Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe" (14:5) inaonesha kwamba maoni ya uhakika ni ya umuhimu. Mtu hapaswi kuwa na mashska katika yale mambo anayoyaamini. Uvumilivu wa maoni au mawazo ya watu wengine haimaanishi kwamba hatujui maoni yetu ni yapi au kwamba tunapuuzia ushahidi na mantiki.

(14:7-9) Hakuna mtu aishiye kwa nafsi yake mwenyewe. Kila aina ya maisha inapaswa imwadhimishe Kristo. Kifo cha Kristo na kufufuka kwake kilitukomboa sisi, na sisi ni mali yake.

(14:10-12) Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Kwa hiyo, maoni yetu kuhusiana na mtu mwingine hayana umuhimu wowote.

(14:13-15) Ni jambo muhimu sana kwetu kwamba mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha kumwangusha. Kwa Mkristo, hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake kwa sababu kila kitu ni mali ya Mungu. Lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi na kama ataamua kukitumia, atakuwa ametenda dhambi kwa sababu amechagua kufanya jambo baya. Tunamfanya mtu ajikwae ikiwa tunamshawishi afanye jambo analofikiri si sahihi (Andiko lingine kuhusiana na suala hili liko katika 1 Wakorintho 8).

(14:16) Mkristo anaweza kuwa na mafundisho mazuri ya imani na bado akaleta madhara kwa sababu ya kutojali ushawishi wake dhidi ya watu wengine.

(14:17) Ukristo hauna aidha sheria au masharti kuhusiana na mfumo wa maisha au uhuru wake. Ukristo ni ushindi wa kiroho na maisha ndani ya Roho Mtakatifu.

(14:18-19) Mungu huwa anafurahia wakati tunapokabidhi kila kitu tunachofanya kwa Kristo na kufanya lolote linalowezekana katika kuwaimarisha watu wengine.

(14:20-23) Kila kitu ni mali ya Mungu, na mtu yeyote anayekumbuka hivyo anaweza kuwa huru. Hata hivyo, kama mtu akitenda jambo fulani analolifikiria kwamba ni baya, anatenda dhambi kwa kuchagua kufanya hivyo. Ndugu anayejisikia yuko huru anapaswa awe na mpaka wa uhuru wake ili kujizuia asisababishe watu wengine kuanguka.

Hakuna maelekezo yeyote yaliyotolewa kwa ajili ya ndugu aliye dhaifu, isipokuwa tu kwamba hapaswi kumhukumu mtu mwingine aliye na uhuru wake zaidi. Mtu mdhaifu amefungwa na dhamira yake na hawezi akabadili tabia yake, lakini ndugu aliye na nguvu ana chaguo.

Inawezekana kukawepo na majadiliano zaidi wakati wa kushughulikia kukamilisha kifungu kilichotangulia, lakini kuna baadhi ya maswali ya kutafakari yafuatayo:

- Kuna mambo gani ambayo kanisa letu linawaachia washirika wake waamue kila mtu kwa binafsi yake?
- Je, tunaona tofauti gani kwa waamini wengine kuhusu kile ambacho tulipaswa kuonesha kuvumiliana zaidi?
- Je, tunawezaje kuwa waaminifu katika kutumia kanuni za kifungu hiki kwenye maoni yetu na katika kushirikiana na watu wengine?

Kuwatambua wanaotetea ufuatwaji wa sheria za Kiyahudi.

Wayahudi hawkuwa tu ni wafuasi wa Uyahudi, ambayo ni dini ya wayahudi. Hawa ni Wayahudi waliojinadi kuwa wao ni Wakristo lakini wakafikiri kwamba Wakristo ni lazima pia watekeleze matakwa ya dini ya Uyahudi. Halikuwa ni tatizo kwa Wayahudi waliokuwa wameokoka kuendelea katika kutumikia mambo ya Uyahudi. Wengi walifanya hivyo, hasa wakati wa kizazi cha kwanza cha kanisa la Agano Jipya. Tatizo lilikuwa ni wakati Wayahudi hao walipojinadi kwamba wameokoka wakati hawakuwa wanaielewa injili ya neema.

Wayahudi waliokuwa ndani ya kanisa walifikiri kwamba ilikuwa ni muhimu kwa mtu wa Wamataifa aliyeokoka akubaliane na masharti yote ya dini ya Kiyahudi, ikiwemo Kutahiriwa, ili aweze kukamilika kuwa ameokoka. Hawakuhubiri injili kwa watu waliopotea; bali walihubiri mambo mengine kwa wengine waliookoka wakisababisha mtafaruku na mgawanyiko. "Ushindi" wao mkubwa tunauona katika kitabu cha Wagalatia, ambapo walipotosha kanisa lote. Barua ya Paulo kwa Wagalatia ilikusudiwa kuwarejesha wote kwenye ukweli wa injili.

Suala hili la sheria za kiyahudi liliwakilishwa kwenye baraza la uongozi la kanisa, kama ilivyonukuliwa katika Matendo 15. Mitume walitambua kwamba kufuata njia ya Wayahudi waliokuwa ndani ya kanisa ingekuwa ni kuikana injili ya neema ambayo ilikuwa inatolewa kwa kiwango sawa kwa Wamataifa. Maamuzi ya baraza la uongozi yalikuwa ni kuwasahihisha waamini wa kweli ambao kwa ukweli walikuwa wamepotoshwa na

hawakuweza kuwazuia wale wote waliokuwa na malengo potofu. Paulo aliwachukulia Wayahudi waliokuwa ndani ya kanisa kama maadui wa injili.

Warumi 14:1-15:12 inahusika na ukweli wa injili ambao Paulo alikuwa ameuelezea kwenye barua yake yote kuhusiana na suala hili la sheria za wayahudi. Watu waliokuwa wameamini hawakupaswa kumhukumu mtu mwingine kutokana na kujishughulisha katika kuzingatia kanuni za kidini za Kiyahudi. Sehemu hiyo ilimalizika kwa msisitizo kwamba injili ni kwa ajili ya dunia nzima

Vifungu vingine kwenye somo hili ni pamoja na Warumi 4; Matendo 15; Wagalatia 2, 3, 5; na Wakolosai 2:11-23.

Kifungu cha Kujifunza – Warumi Sehemu ya 6, kifungu cha 6

Mwendelezo wa maelezo ya Aya-kwa-Aya

(15:1-4) Wale wenye nguvu, ambao wanajiona huru, wanapaswa kuwa tayari kuacha baadhi ya haki zao ili kuwasaidia wale walio dhaifu katika imani na ambao hawajihisi huru kutokana na vizuizi vya ziada.

(15:5-7) Aya hizi zinakamilisha kifungu. Lengo ni umoja wa Kikristo. Upendo wa Kristo ni mfano wetu.

Simulizi inayohusu Umoja, Uamsho na Umisheni.

Katika mwaka a 1722 mmiliki mmoja wa ardhi raia wa Ujerumani aliyekuwa akiitwa Zinzendorf aliwaalika waamini wa Kimoraviani waliokuwa kwenye mateso wahamie kwenye eneo lake la makazina akajenga hapo himaya yake. Hatimaye, watu kwa mamia kadhaa walikuwepo kwenye ile jumuiya. Walijitahidi kupambana na mgawanyiko wa mafundisho kadhaa ya kiimani na taratibu za kuabudu: lakini katika mwaka wa 1727 wakaanzisha "Makubaliano ya Udugu" (ambayo kwa sasa yanaitwa "Agano la Wamoraviani kwa ajili ya Maisha ya Kikristo") ili kusaidia kuanzisha umoja.

Katika mwaka huo huo, wakaanza kufanya uamsho. Walikuwa na mikusanyiko ya maombi ya usiku na ibada za kuabudu za masaa marefu wakiwa na hisia isiyokuwa ya kawaida ya uwepo wa Mungu, ikiwa ni pamoja na mzungumzaji kulala chini kwa hofu ya Mungu. Wakati wa ibada ya kula sakramenti ya Bwana, Roho Mtakatifu alitembea katikati ya watu katika njia ambayo baadaye katika siku hiyo Zinzendorf alikuja kuona kama ni siku ya Pentekoste ya kufanywa Upya Kanisa la Moraviani. Watu waliokuwa wamegawanyika waliunganishwa tena kwa hisia kuu, na Zinzendorf akongoza sala ya kukiri mafarakano ndani ya kusanyiko. Walianza mkesha wa maombi, waamini mbalimbali wakipeana zamu, na wakaendelea hivyo kwa miaka 100.

Jumuiya ya Kimoraviani ikatokea kuwa ni kusanyiko kubwa sana la kupeleka wamisionari kwa muda wote. Kuanzia mwaka 1733-1742, wamisionari 70 walitumwa kutoka katika jumuiya ya watu 600. Wengi wao walikufa kutokana na kupewa mateso na hali nyinginezo

ngumu. Hadi kufikia mwaka 1760, baada ya miaka 28, wamisionari 226 walikuwa wameshatumwa; na idadi ya Wamoraviani duniani ikaongezeka kwa maelfu.

Maswali ya Mapitio Somo la 11

(1) Elezea mfano wa dhabihu iliyo hai.

(2) Je, nini lazima itokee kwetu ili tuweze kuwa waminifu kwa Mungu?

(3) Je, ni kwa nini inatupasa kuwa wanyenyekevu?

(4) Elezea msemo wa *ndugu aliye dhaifu* na *ndugu aliye na nguvu*.

(5) Nani walikuwa wanaotetea ufuatwaji wa sheria za Kiyahudi?

Kazi ya kufanya Somo la 11

(1) Andika ukurasa mmoja ukatumia baadhi ya maelekezo ya vitendo yanayopatikana katika Warumi 12:1–15:7 kwa Wakristo wa leo.

(2) Jiandae kwa ajili ya mtihani wa mwisho kwa kujifunza orodha ya maswali yaliyoko kwenye Kiambatisho "A" cha kozi hii. Ni lazima ufanye mtihani huo bila ya kupata msaada kutoka kwa mtu mwingine yeyote na bila ya kuangalia kwenye kumbukumbu zilizoandikwa.

Somo la 12
Maono kwa Ajili ya Umisheni

Maelezo kwa kiongozi wa darasa

Panga mtihani wa mwisho na hakikisha kikundi kimejianda kwa hilo.

Tamaduni Kuu Tatu

Tamaduni kuu tatu ziliutengeneza ulimwengu uliokuwa umepokea injili kwenye karne ya kwanza. Mungu aliuandaa ulimwengu uwe katika hali ya kupokea injili itakayokuwa ya mafanikio makubwa sana.

Utamaduni wa Wayunani

Iskanda Mkuu aliitawala dunia ya ujima na akatengeneza himaya yake. Kwa makusudi alieneza utamaduni wa Kiyunani, kwa sababu aliamini ulikuwa ni wa juu na bora zaidi kuliko tamaduni nyingine zote na kwa sababu ingesaidia katika kuunganisha himaya yake. Alimtaka kila mtu azungumze lugha ya Kiyunani na kuishi katika mila za Kiyunani. Hali hii ilifanya maandalizi kwa ajili ya Injili kwa sababu wamishenari waliweza kuhubiri injili kwa kutumia lugha ya Kiyunani katika himaya yake yote.

Mawazo ya Wayunani yaliwafanya watu wajione kama watu huru binafsi badala ya kundi la kikabila au familia. Kwa hiyo, walikuwa wazi zaidi katika kufanya maamuzi binafsi kuhusiana na mambo ya dini. Watu walijitambua kwamba ilikuwa rahisi kwao kubadilisha dini yao.

Wayunani walijiona wenyewe kama ndio raia wa dunia hii, badala ya raia tu wa nchi yao ndogo. Walitambua kwamba kuna ukweli unaotumika kwa watu wote, badala ya kila kikundi cha watu kuwa na ukweli wao wenyewe. Hali hii iliwafanya watambue kwamba ukweli unaweza kuja kwao kutoka mahali pengine popote na siyo lazima kutoka kwenye utamaduni wao wenyewe.

Wanafalsafa wa Kiyunani walijaribu kujibu maswali kuhusu maana ya maisha na ulimwengu. Waliamini kwamba majibu yapo ambayo yanaweza kuelezea kuhusu maisha kwa kila mtu.

Wanafalsafa wa Kiyunani walijaribu kutumia akili kuonesha kwamba dini za zamani zilikuwa potofu. Pia walisababisha watu kutoridhika na hadithi za miungu. Miungu ilikuwa ni maelezo ya kibinadamu yaliyotiwa chumvi mno kwa makosa ya kibinadamu, ukosefu wa maadili na matendo ya uovu.

Wanafalsafa wa Kiyunani walipendekeza maelezomapya kuhusiana na maisha na ukweli. Kila falsafa mpya ilifanyiwa mdahalo, na hakuna falsafa iliyofanikiwa katika kujibu maswali yote kwa ukamilifu. Waligundua na kujadili maswali muhimu tu lakini hawakuweza kujibu yote.

Falsafa haiwezi kukidhi mahitaji ya kiroho ya kibinadamu.

Ukristo unajibu maswali yote yanayoulizwa na falsafa na pia hutosheleza mahitaji ya kiroho.

► Je, Ni kwa jinsi gani utamaduni wa Kiyunani uliweza kuibadilisha dunia na kuandaa kuenea kwa injili?

Utamaduni wa Kirumi

Himaya ya Kirumi ilianza baada ya kuanguka kwa himaya ya Kiyunani katika maeneo au nchi mbalimbali chini ya himaya moja. Warumi walishinda na kutawala mataifa mengi, lakini utamaduni uliokuwa ukitumika zaidi ni ule wa Kiyunani.

Ushindi wa Warumi ulisababisha watu wengi kupoteza imani yao kwa miungu yao mingi iliyokuwa haina uwezo wa kuwasaidia. Watu walikuwa na ari zaidi ya kusikia kuhusu Mungu mwenye nguvu, wa ulimwengu wote.

Warumi waliamini katika miungu mingi na walikuwa na hadithi nyingi kama zilivyokuwa mithiolojia (hadithi zinazoelezea asili ya watu na matukio) za Wayunani. Warumi wengi waliokuwa wanazuoni kwa uhakika hawakukubaliana na miungu lakini waliitumikia dini kama sehemu ya utamaduni wao.

Sheria ya Kirumi ilileta dhana zilizo wazi zaidi kuhusu haki. Mahakama za Kirumi zilizingatia ushahidi katika njia nzuri zaidi. Hii ilisaidia katika kuweka msingi wa mafundisho ya imani kuhusiana na mtu kuwa na hatia na kupewa haki.

Umiliki wa Warumi ulimaliza vita ndogo ndogo kati ya mataifa, wakileta kitu kilichoitwa *Pax Rumina*, yaani Amani ya Warumi. Hali hii ilifanya kuwepo na usafiri wa amani, na wamisionari waliweza kuvuka mipaka ya nchi mbalimbali bila matatizo.

► Je, ni kwa jinsi gani utamaduni wa Kirumi uliweza kuibadilisha dunia na kuandaa kuenea kwa injili?

Utamaduni wa Kiyahudi

Wayahudi walikuwa wameenea kwenye ulimwengu wote wa maendeleo, na kila mahali walianzisha masinagogi na kufundisha imani yao. Mitume Waligundua kwamba "Musa anahubiriwa katika kila mji" (Matendo 15:21). Uaminifu wa Wayahudi kwa dini yao ya Israeli, ulikuwa na ushawishi katika Rumi.

Dhana ya Uyahudi ya Mungu mwenye mamlaka na mtakatifu iliheshimika zaidi kuliko mithiolojia za Wayunani za miungu ya upotovu na isiyokuwa na maadili. Hali ya juu ya maadili ya dini ya Uyahudi ilikuwa ni kivutio kwenye dunia ya machafuko ya kimaadili. Ukristo ulishirikishwa maadili haya, ukayakuza, na kuhubiri uwezo wa neema ya kubadilisha mwenye dhambi na kumfanya aishi maisha matakatifu.

Dhana ya Uyahudi ya kusudi la Mungu katika historia na matazamio ya Masihi yalileta matumaini kwa ajili ya baadaye. Matumaini hayo yalikuwa ni Mungu kuingilia kati, na siyo

suluhisho za kibinadamu. Ukristo ulitanagaza kwamba Masihi ameshafika na kwamba enzi mpya imeshaanza.

► Je, ni kwa jinsi gani utamaduni wa Kiyahudi uliweza kuibadilisha dunia na kuandaa kuenea kwa injili?

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 7

Katika kifungu hiki, mtume nanaelezea ni kwa nini anaandika hii barua. Anataka kuwatembelea, kisha apokee msaada kutoka kwao ili aweze kuanza safari yake ya kwenda Hispania. Hili kusudi la barua linaongoza muundo wake kwa sababu Paulo alieleza injili ni nini, kwa nini kila mtu anaihitaji, kwa nini wajumbe wa injili ni muhimu, na kwa nini alikuwa na sifa za kwenda katika safari hiyo. Alionesha kwamba umisheni wa dunia nzima siku zote ulikuwa ni mpango wa Mungu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 15:8-33 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(15:8) Yesu alikamilisha ahadi za kimasihi zilizokuwa zimetolewa kwa mababu wa Kiyahudi na kujidhihirisha kupitia taifa la Kiyahudi na dini.

(15:9-12) Kupitia nukuu kadhaa za Agano la Kale, mtume anaonesha kwamba siku zote Mungu alikusudia injili iende kwa Wamataifa. Katika Maandiko Paulo ananukuu Manabii walikuwa wametabiri kwamba:

- Watu wa Mataifa watakuwa watu wa kumwabudu Mungu
- Masihi atatawala juu ya watu wa Mataifa.
- Watu wa Mataifa watamtumainia Masihi.

(15:13-14) Mtume anatoa maombi ya baraka kwa kanisa la Rumi na kusema kwamba anaamini kwamba washiriki wake wameimarika kiroho. Kwenye aya zinazofuata, atawaita kwa ajili ya kazi ya umishenari. Hata kanisa lililobarikiwa kuwa na nguvu za kiroho litakuwa halijakamilika kama halina maono na kuhusika na kazi ya umishenari.

► Je, kunatokea nini kama kanisa halina nia ya kusaidia kazi ya umishenari kwa ajili ya maeneo yaliyo mbali?

(15:15-16) Mtume anawaambia kuhusu wito maalumu anaopaswa waubebe kwa ajili ya injili kwa Wamataifa. Mungu amempa karama maalumu za kiroho kwa ajili ya kazi hii. Matamanio yake ni kwamba makanisa yanayotokana na Wamataifa yawe matakatifu na ya kweli, yanayompendeza Mungu.

(15:17-19) Mungu alishampa mafanikio katika huduma yake. Wamataifa wengi wamekuwa watiifu kwa Neno la Mungu. Mojawapo ya matokeo muhimu sana ya huduma ni kwamba watu wanatubu na kuishi katika kumtii Mungu. Hakuna alama nyingine ya mafanikio kama hiyo. Anasema kwamba huduma yake imeambatana na miujiza ya Mungu. Alisambaza injili kwenye maeneo yote makuu ya nchi.

(15:20-22) Jaribio lake lilikuwa ni kuhubiri mahali ambapo injili haijawahi kuhubiriwa tena kabla. Hatua kwa hatua alikamilisha maeneo yote ya nchi. Kipaumbele hicho kilikuwa ndiyo sababu hakuweza kusafiri kwenda Rumi, kwa sababu injili alikuwa tayari imeshahubiriwa huko.

(15:23-24) Alikuwa ameshahubiri injili kwenye kila eneo lililokuwa karibu naye. Alitaka kanisa la Rumi limsadie afanye ziara ya umishenari nje yao aingie Hispania. Safari hiyo itampa nafasi ya kuhubiri na kufanya ushirika pale Rumi, na pia asaidiwe kufika katika mikoa ambayo alikuwa bado hajawahi kuihubiria injili.

► Elezea ni kwa jinsi gani kila Mkristo na kila kanisa lina deni la kuunga mkono upelekaji au uenezaji wa injili. (Kama itahitajika, ona kumbukumbu iliyoko katika Warumi 1:15, kwenye somo la kwanza.)

(15:25-29) Kwa kuanzia, atafunga safari ya kwenda Yerusalemu ili akachukue sadaka kutoka kanisa la watu Wamataifa na kwenye kanisa la Wayahudi. Sadaka hii ilikuwa ni muhimu sana. Kwa kuituma hiyo sadaka, Wamataifa walikuwa wanakiri dhamana waliyo nayo kwa Wayahudi kwa sababu Wayahudi waliogeukia Ukristo ndio waliowaletea injili. Kwa kuipokea ile sadaka, Wayahudi wanakiri kwamba Wamataifa walikuwa sawa na wao katika kanisa moja. Hakutakuwepo na mgawanyo wa dini za Kikristo. Ndiyo maana Paulo aliwataka waombe kwamba waamini wa Kiyahudi wapokee sadaka zao.

(15:30-33) Aliwataka waombe kwamba aokolewe kutoka katika hatari ya wale Wayahudi wasioamini katika Yerusalemu, ili kwamba aweze kufika Rumi. Maombi yake yalijibiwa, ingawaje siyo katika njia aliyokuwa ameichagua. Paulo aliwasili Rumi kama mfungwa baada ya kukamatwa huko Yerusalemu na kuwekwa mahabusu na watawala wa Kiyahudi, akachukuliwa na gavana wa Kirumi, na mwishowe akapelekwa Rumi kwa mashtaka. (Taarifa hii iko katika kitabu cha Matendo, kuanzia 21:26 hadi mwisho wa kitabu cha Matendo.) Hatujui tena baada ya hapo kama Paulo alikuja kufanya safari ya kwenda Hispania.

► Ni kwa jinsi gani tunaona utoaji wa Mungu kwenye matukio ya maisha ya Paulo, hata kama safari yake ya kwenda Hispania haikufanyika tena kama alivyokuwa amepanga?

Kifungu cha kujifunza – Warumi Sehemu ya 8

Muhtasari wa sura ya 16

Kuna salamu nyingi kwa majina yao katika waraka huu kuliko kwenye maeneo mengine yote aliyoandika Paulo. Inawezekana ikawa hivyo kwa kuwa alikuwa hajawahi kukaa Rumi, anawataja watu wote aliokuwa amezoeana nao waliokuwepo pale kwa ajili ya kusaidia kuanza uhusiano wake na kanisa.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 16 kwa ajili ya kikundi.

Maelezo ya Aya-kwa-Aya

(16:1-2) Fibi yumkini alikuwa miongoni mwa wale waliobeba barua hii. Paulo aliwaambia wamsaidie dada huyu katika huduma yake kwa sababu alikutana na mahitaji ya watu wengi. Mtu mzuri wa kuweza kumsaidia ni yule ambaye tayari amefanyika kuwa ni baraka kwa watu wengine.

(16:3-4) Priska na Akila walidiriki kuhatarisha maisha yao kwa ajili ya Paulo. (Ona Mdo 18:1-3, 24-26 kwa historia zaidi kuhusiana nao).

(16:7, 11, 21) Jamaa za Paulo zimetajwa katika aya hizi.

(16:13) Mwanamke anayetajwa hapa inawezekana labda siyo mama yake na Paulo. Inawezekana Rufo alikuwa mtoto wa Simoni wa Krete ambaye alibeba msalaba wa Yesu, kwa sababu katika Marko 15:21 jina lake limetajwa kama aliyekuja kujulikana kwa kanisa baadaye.

(16:17-18) Kuna watu ambao wanajaribu kuwatenga wenzao kutoka kwenye misingi ya ukweli ya kanisa ili waweze kujenga mambo yao wenyewe ya watu kuwafuata wao. Watu hawa hawamtumikii Kristo, bali matamanio yao wenyewe. Ujumbe wao ni tofauti kabisa na mafundisho sahihi ya imani kuhusiana na wokovu. (Ona 3 Yohane 1:9-10 na 2 Petro 2:1-3.)

(16:19) Tunapaswa tujifunze kwa kiasi kikubwa kadri inavyowezekana kuhusu ukweli. Hatupaswi tujue mengi kuhusiana na mambo ya uovu. Watu ambao wanajifunza kuhusu mambo ya uovu wanakabiliwa na hatari ya mvuto wa uharibifu na upotoshaji wa kufikiri kwao.

(16:20) Kanisa ni lazima mwishowe litashinda dhidi ya Shetani kupitia kazi ya Kristo (Mwanzo 3:15).

(16:22) Tertio hakuwa mwandishi wa waraka huu, bali ni mtu aliyeandika yale ambayo Paulo alikuwa anamzungumzia yeye ili ayaandike.

(16:25-27) Aya hizi zinarejea kwenye mada muhimu za barua hii. Angalia maneno "injili yangu" na "kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo." Anaelezea tena kwamba injili ni ufunuo wa sasa wa ile siri iliyositirika na ujumbe wa mitume. Anamalizia na kurejea mara ya mwisho kuhusu mambo ya umisheni, akiwakumbusha wote kwamba ujumbe ni kwa ajili ya mataifa yote. Lengo la kazi ya umisheni ni sawa na kama Yesu alivyoagiza katika Agizo Kuu (Mathayo 28:19-20): kuwaleta watu kwenye utii kwa Kristo. Hii inamalizia barua kama ilivyoanza, kama 1:5 anasema: kwamba sababu ya huduma ni kuwaleta Wamataifa wote kwenye kumtii Mungu.

Uwasilishaji wa Injili kutoka kwa Warumi

Injili inaweza kufafanuliwa kwa kutumia aya pekee kutoka katika kitabu cha Warumi. Uwasilishaji huu wa injili mara nyingine unaitwa "Barabara ya Kirumi."

Sentensi ya kwanza ya ufafanuzi kwa kila kitu kinachorejewa ni muhimu sana kukikumbuka.

Warumi 3:23

"kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

Kila mtu ametenda dhambi kwa kufanya mambo ambayo wanajua ni makosa. Aya hii inaonyesha kwamba kuna tatizo kubwa la ukweli ambalo watu wanalo. Hawajamtii Mungu; kwa makusudi kabisa wamekataa kumtii Mungu. Hakuna hata mtu mmoja ambaye hahusiki. Hakuna mtu ambaye anaweza kukubalika na Mungu kwa misingi ya kwamba siku zote amekuwa akitenda yaliyo sahihi.

Kwa msisitizo wa ziada kuhusiana na jambo hili, unaweza kutumia Warumi 3:10 (Hakuna mwenye haki hata mmoja") na 5:12 ("na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi").

Warumi 6:23

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

Wenye dhambi wamevuna kifo cha milele, lakini Mungu anatoa uzima wa milele kama zawadi kupitia kwa Yesu.

Aya hii inaonyesha ni kwa nini dhambi ni mbaya sana, adhabu ya dhambi imepitishwa kwa kila mtu. Ni kifo cha milele, hukumu ya Mungu ambayo kila mwenye dhambi anastahili.

Tofauti na kifo ambacho tumeshakipata, Mungu anatoa karama ya maisha, jambo ambalo tulikuwa hatujastahili.

Warumi 5:8

"Bali Mungu aonesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."

Karama ya Mungu ilitolewa kwa kifo cha Yesu Kristo kwa ajili yetu.

Mungu hakuwa tayari kutuachilia tupokee hukumu tuliyokuwa tumestahili. Kwa kuwa anatupenda, alitoa njia mbadala ya kupokea rehema. Yesu alikufa kama dhabihu ili tuweze kusamehewa. Mungu hakungojea tufanye jambo fulani ili tustahili wokovu – ilikuja kwetu wakati bado tuko wenye dhambi. Wokovu hautolewi kwa watu wazuri, bali kwa wenye dhambi.

Warumi 10:9

"ukimkiri Yesu … na kuamini … utaokoka."

Hitaji peke yake kwa ajili ya wokovu ni kwa mwenye dhambi kukiri kwamba ni mwenye dhambi na kuamini ahadi ya Mungu ya msamaha.

Vipi kuhusu kutubu? Kama mtu atakiri kwamba amefanya makosa na anataka kusamehewa, anaonyesha kwamba anataka kwa hiari yake mwenyewe kuondokana na dhambi zake.

Warumi 10:13

"Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka."

Utoaji wa wokovu ni kwa kila mtu. Hakuna mtu hata mmoja aliyetengwa. Hakuna sifa nyingine zinazohitajika.

Warumi 5:1

"Tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu."

Kuamini ahadi ya Mungu kunatufanya tuwe marafiki wa Mungu, na hatuendelei kuhesabiwa wenye hatia tena.

Kuwa na amani na Mungu ni kumaanisha kwamba sisi siyo maadui wake tena; tumepatanishwa. Dhambi ambayo imetutenganisha na Mungu inaondolewa na kutupwa. Kuhesabiwa haki inamaanisha kuhesabiwa kwamba huna hatia tena. Kuhesabiwa haki kwa imani inamaanisha kwamba kumwamini Mungu na ahadi zake ndicho kitu peke yake kinachohitajika kwa ajili ya msamaha wetu.

Warumi 8:1

"Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu."

Kwakuwa tumeunganishwa kwa Kristo, hatuko tena kwenye hukumu ya dhambi tulizozitenda.

Kristo aliishi maisha yasiyokuwa na dhambi na akakamilisha mahitaji yote ya haki kwa njia ya kifo chake juu ya msalaba. Kwa imani tunajitambulisha naye na pamoja naye tunakubaliwa na Mungu Baba. Mungu anatuchukulia kama ambao kamwe hatujawahi kufanya dhambi.

Hitimisho

Elezea kwamba mwenye dhambi anaweza akaokoka kwa kumwomba Mungu, akikiri kwamba ni mwenye dhambi, na akiomba msamaha kwenye msingi wa dhabihu ya Yesu kwa ajili yake.

Kwa Kujifunza na Kutendea kazi

Njia bora zaidi ya kujifunza na kufanya mazoezi ya njia hii kwanza ni kuweka alama ya kila aya iyakayotumika katika Warumi kwa kuzungushia au kupiga mstari chini yake. Kisha,

weka namba pembeni ya kila aya ukionyesha mtiririko wa matumizi yake. kwa mfano, pembeni mwa mastari ambao ndio utakaoanza kutumika kwanza, weka namba 1.

Kisha fanya zoezi la kuwasilisha injili. Soma kila aya na toa maelezo yanayoendana nayo. Hakikisha kuingiza dhana ambazo ziko kwenye sentensi ya kwanza baada ya kila aya (hapo juu). Kisha, ongezea maelezo mengine yeyote yatakayohitajika, kwa kutumia sentensi nyingine kama zitaonekana zina msaada. Siyo lazima kutumia maneno yale yale yaliyotumika au yaliyotolewa katika somo hili.

Fanya mazoezi hadi ujione kwamba unaweza kufanya mwenyewe bila ya kuangalia mahali pengine popote isipokuwa Biblia yako.

Maswali ya Mapitio Somo la 12

(1) Elezea jinsi tamaduni kuu tatu zilivyotayarisha ulimwengu kwa ajili ya kuenea injili katika karne ya kwanza.

(2) Je, mtu anaoneshaje kuwa Mungu wakati wote alipanga injili iende kwa Wamataifa?

(3) Je, ni kwa nini sadaka ya kanisa ilikuwa muhimu sana Yerusalemu?

(4) Je, Paulo alifikaje Rumi?

Maswali ya Mapitio ya Masomo na Mtihani wa Mwisho

Somo la 1

(1) Je, kwa nini Paulo aliandika waraka kwa Warumi kwa waamini wa Rumi?

(2) Je, kwa nini Paulo alipanga kwenda Rumi?

(3) Je, Maana ya msemo *Yesu Krsito Bwana wetu* una maana gani katika nyaraka za Agano Jipya?

(4) Je, ufufuo unathibitishaje uungu wa Yesu?

(5) Elezea msemo *wasio wayunani* (Warumi 1:14).

(6) Kwa nini Mwinjilisti Paulo ana deni la kuhubiri injili?

(7) Je, ni kitu gani kikuu na ukweli muhimu katika kitabu cha Warumi?

(8) Je, kifo kina maana gani katika kitabu cha Warumi?

(9) Kulingana na Warumi, ni nani analindwa asipate hukumu ya Mungu?

Somo la 2

(10) Je, ni kwa njia gani watu hupokea ufunuo wa Msingi?

(11) Je, watu wote wanajuaje kuhusu Mungu hata bila Maandiko?

(12) Je, Ufunuo maalumu ni nini?

(13) Je, kuabudu sanamu ni nini?

(14) Taja njia mbili ambazo zinaleta madhara ya upotovu wa fikira kwa watu

Somo la 3

(15) Je, Maandiko yanayohusu siku za mwisho yanaelezaje?

(16) Je, kwa nini Wayahudi walitarajia kupata Upendeleo?

(17) Je, mtu anahesabiwaje haki?

(18) Je, mtu huoneshaje kwamba anayo imani iokoayo?

(19) Je, tohara ina umuhimu gani kwa Myahudi, na ina mfano gani kwa Mkristo?

Somo la 4

(20) Elezea dhana ya Calvin ya "neema ya kawaida".

(21) Elezea dhana ya Wesley ya "neema ya awali" yaani neema inayotangulia.

(22) Katika Warumi 3:19, maneno "kila kinywa kufumbwe" yana maanisha nini?

(23) Je, ni manufaa gani mabwa yanatajwa kwa Wayahudi katika Warumi 3?

(24) Je, aina mbali mbali za kuabudu zinatunufaishaje?

(25) Je, Warumi 3:10-18 inaonesha nini?

(26) Je, ni nani aliyeko chini ya sheria? (Warumi 3:19-20)

Somo la 5

(27) Je, Mtu aliye na imani iokoayo anaamini nini?

(28) Je, ni tatizo gani lilitatuliwa na upatanisho?

(29) Ni jinsi gani upatanisho ulitatua tatizo?

(30) Je, kuhesabiwa haki ina maana gani?

(31) Je, ni kwa njia gani mtu anaiheshimu sheria kama kipimo cha kuhesabiwa haki?

(32) Je, ahadi ya Mungu ya neema kwa Abraham ilikuwa ni nini?

(33) Je, Daudi alisemaje kuhusu kuhesabiwa kwa imani?

(34) Je, nani ni watoto wa kiroho wa Ibraham?

(35) Tunajua nini kutoka katika Warumi 5:15 kwamba wokovu hutolewa kwa kila mmoja?

Somo la 6

(36) Je, kwa nini ni muhimu kuelewa dhambi ni nini?

(37) Je, maana ya dhambi ya kukusudia ni nini?

(38) Ni dhana gani potofu ambayo Paulo anaijibu katika Warumi 6?

(39) Je, kuifia dhambi ina maana gani?

(40) Je, ina maana gani kuwa chini ya neema?

(41) Je, kuwa chini ya sheria ina maana gani?

(42) Je, kwa nini ni haiwezekani kumtumikia Mungu na dhambi?

(43) Je, msemo wa utu wa kale maana yake ni nini?

Somo la 7

(44) Taja sababu mbili zinazonesha kuwa sheria za ibada na sheria za kiraia za Agano la kale bado zina umuhimu.

(45) Je, ina maana gani kufa katika sheria?

(46) Je, neno *katika mwili* lina matumizi gani mawili?

(47) Je, sheria inafanyaje dhambi iwe mbaya Zaidi?

(48) Kwa nini sheria inafaa kwa uinjilisti?

Somo la 8

(49) Kwa nini haiwezekani sheria iwe ni njia ya wokovu?

(50) Je, ina maana gani kusema mwamini hatawaliwi tena na mwili?

(51) Je, ni kwa jinsi gani sheria inaelekeza maisha ya mkristo?

(52) Je, ushuhuda wa Roho ni nini?

(53) Wokovu wa mwisho ni nini?

(54) Je, kama watu watakana ufufuo wa mwili matokeo yake ni nini?

(55) Je, ni nini usalama wa mwamini?

Somo la 9

(56) Je, tunajuaje kuwa Mungu anataka tuelewe anavyotenda haki?

(57) Je, ni kwa nini ni muhimu kwetu kuona kwamba Mungu ni wa haki?

(58) Je, mtazamo wa kibiblia kuhusu ukuu wa Mungu ni upi?

(59) Je, jambo kuu katika Warumi 9 ni nini?

(60) Je, manufaa ya kiroho ya Israel ni nini?

(61) Je, kuna mahusiano gani matano kati ya Ukristo na Uyuda?

(62) Je, Warumi 9 inasemaje kuhusu Mungu kumchagua Yakobo?

(63) Je, kwa nini tunafurahia ukuu wa Mungu?

Somo la 10

(64) Je, jambo kuu katika Warumi 10 ni nini?

(65) Je, ni jinsi gani Wayahudi walijaribu kujihesabia haki?

(66) Je, tunajuaje kuwa watu walioishi kabla ya Kristo kuja walikuwa hawaokolewi kwa njia ya matendo?

(67) Je, ina maana gani kuwa wokovu uko mioyoni na midomoni mwetu?

(68) Je, ni kwa nini ujumbe wa mishenari ni wa haraka?

(69) Elezea mfano wa matawi ya mti katika Warumi 11.

(70) Orodhesha aina tatu za ahadi za Agano la Kale.

Somo la 11

(71) Elezea mfano wa dhabihu iliyo hai.

(72) Je, nini lazima itokee kwetu ili tuweze kuwa waminifu kwa Mungu?

(73) Je, ni kwa nini inatupasa kuwa wanyenyekevu?

(74) Elezea msemo wa *ndugu aliye dhaifu* na *ndugu aliye na nguvu*.

(75) Nani walikuwa wanaotetea ufuatwaji wa sheria za Kiyahudi?

Somo la 12

(76) Elezea jinsi tamaduni kuu tatu zilivyotayarisha ulimwengu kwa ajili ya kuenea injili katika karne ya kwanza.

(77) Je, mtu anaoneshaje kuwa Mungu wakati wote alipanga injili iende kwa Wamataifa?

(78) Je, ni kwa nini sadaka ya kanisa ilikuwa muhimu sana Yerusalemu?

(79) Je, Paulo alifikaje Rumi?

Usomaji Unaopendekezwa

Alford, Henry. *The Greek New Testament.* Chicago: Moody Press, 1968. Pia inapatikaa katika: https://studylight.org/commentaries/eng/hac.html

Greathouse, William. "Romans" in *Beacon Bible Commentary*. Kansas City: Beacon Hill Press, 1968. Pia inapatikaa katika: https://archive.org/details/beaconbiblecomme0000grea/page/n19/mode/2up

Kinlaw, Dennis. "Lectures on Romans " Audio series. Wilmore, KY: Francis Asbury Society.

Wesley, John. *Explanatory Notes Upon the New Testament.* London: Epworth Press, 1976. Pia inapatikaa katika: https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html

Wesley, John. *Wesley's Works. Hususani zifuatazo:*

- "Justification by Faith" https://holyjoys.org/justification-by-faith/
- "Predestination Calmly Considered" https://holyjoys.org/predestination-calmly-considered/
- "Dialogue between a Predestinarian and His Friend" https://holyjoys.org/john-wesleys-dialogue-between-a-predestinarian-and-his-friend/
- "The Origin, Properties, and Use of God's Law" https://holyjoys.org/john-wesley-on-the-origin-properties-and-use-of-gods-law/
- "The Law Established by Faith: Discourse I" https://holyjoys.org/the-law-established-through-faith-discourse-1/
- "The Law Established by Faith: Discourse II" https://holyjoys.org/john-wesley-on-the-law-established-through-faith-discourse-2/
- "First Dialogue between an Antinomian and His Friend" https://holyjoys.org/first-dialogue-between-an-antinomian-and-his-friend/
- "Second Dialogue between an Antinomian and His Friend" https://holyjoys.org/second-dialogue-between-an-antinomian-and-his-friend/

Yocum, Dale. *Dr. Yocum Teaches the Epistles of Paulo*. Salem, OH: Schmul, 1992.

Kumbukumbu ya Mazoezi ya Kufanya

Jina la Mwanafunzi _____

Somo	Mazoezi ya kufanya Kuandika
1	
2	
3	
4	
5	
6	
7	
8	
9	
10	
11	

Mahubiri/Mazoezi ya Somo	
Tarehe	Aina ya Kikundi
Somo la 9 **Mazoezi ya kuzungumza**	
Mtihani wa Mwisho wa kupata Daraja	

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Rais wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).